# UCHUNGUZI WA MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA UFUNZAJI NA UJIFUNZAJI WA SHULE ZA CHEKECHEA KATIKA MANISPAA YA WEBUYE, KENYA

NA

LIAMBILA N. MARTHA

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA TAALUMA YA ELIMU YA KISWAHILI
(M.ED IN KISWAHILI)

IDARA YA ELIMU YA LUGHA NA FASIHI CHUO KIKUU
CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA CHA MASINDE MULIRO

APRILI, 2010.

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi asilia na wala haijawasilishwa na kutahiniwa katika chuo kikuu kingine. Ni marufuku kutolesha au kuchapisha sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini na ridhaa yangu au chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Sahihi Tarehe

Liambila Martha Nakhumicha.

EDK/G/01/05

## IDHINISHO

Tunayakinisha kuwa kazi iliyo humu imefanywa na mtahiniwa kwa kuridhiwa nasi kama wasimamizi wa chuo kikuu cha sayansi na teknolojia cha Masinde Muliro.

_____________ _________________

Sahihi Tarehe

**Dkt. Godwin Siundu**

**Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi**

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

Kakamega.

_____________ _________________

Sahihi Tarehe

**Dkt. Bob J. Mbori**

**Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi**

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

Kakamega.

_____________ _________________

Sahihi Tarehe

**Dkt. Hannington E. Oriedo.**

**Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi**

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

Kakamega.

## TABARUKU

Kwa wanangu wapendwa Ian, Vallen, Joyce, Patience, Prudence na Josiah.

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima na fursa hii adimu ya kuendeleza kisomo changu. Vilevile ninawashukuru waelekezi wangu Dkt. Godwin Siundu na Dkt Bob Mbori bila kumsahau marehemu Dkt. Hannington Oriedo ambao walijitolea mhanga katika kuisoma kazi yangu, kunielekeza na kunishauri bila kuchoka.

Shukrani zangu za kipekee ziwaendee Prof. Inyani Simala na Bi.Susan Choge, walionizamisha katika bahari ya utafiti. Siwezi kamwe kumsahau mume wangu mpendwa Innocent Munyefu. Yeye alinipa nafasi ya kujiendeleza kimasomo na hata kunipa msaada kila nilipohitaji. Shukrani ziwaendee wahadhiri wangu wote wa Idara ya lugha na fasihi hasa Prof. Isaac O. Ipara, na Bi. Salim Rukia. Tajriba zao zilinifaa kuijenga kazi hii.

Sitawasahau walimu wote wa chekechea wa Manispaa ya Webuye na wasimamizi wao, waliokubali kushirikishwa kwenye utafiti huu na wakachangia pakubwa kunipa habari zote nilizohitaji kuhusu mada ya utafiti. Mwisho, ninatoa shukrani zangu kwa wazazi wangu walioienzi elimu, sitatamatisha bila kumtaja mwalimu George Wanjala aliyeipigisha chapa kazi hii.

## IKISIRI

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza matumizi ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea. Utafiti ulifanywa katika Manispaa ya Webuye katika Wilaya ya Bungoma Mashariki, Mkoani Magharibi nchini Kenya. Sampuli ya watafitiwa iliteuliwa kwa kutumia mbinu za mfumo sahili na njia nasibu sahili. Idadi ya wasimamizi 19, walimu 19 na wazazi 19 wa shule za chekechea walikuwa sehemu ya sampuli.

Data ilikusanywa kupitia hojaji, masaili na kiongozi cha uchunzaji. Data ilichanganuliwa kiidadi na kimaelezo. Michoro, chati na grafu zilitumiwa kuwasilisha data iliyokusanywa, utafiti uliongozwa na nadharia ya uamilifu ya Halliday (1970). Nadharia inafafanua kuwa lugha ndiyo nguzo muhimu katika ufunzaji na ujifunzaji.

Utafiti uligundua kuwa lugha ya Kiingereza na lugha ya Kienyeji zilitumika katika muktadha mmoja na lugha ya Kiswahili. Pia ilifichuliwa kuwa hakukuwa na nyenzo na vielelezo katika lugha ya Kiswahili. Vilevile hakukuwa na maandalizi ya semina katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Utafiti ulifichua kuwa wazazi wengi wa chekechea hawakuunga mkono matumizi ya lugha ya Kiswahili. Japo kulikuwa na vikwazo, Kiswahili ndiyo lugha iliyokuwa maarufu katika shule za chekechea. Mtafiti anapendekeza kuwa jumuiya nzima ya chekechea izingatie sera rasmi ya lugha ambayo inasisitiza matumizi ya lugha sambazi.

Lugha ya Kiswahili inastahili kuimarishwa, kukuzwa kama lugha ya kufundishia katika shule za chekechea za miji. Iwapo ni lazima lugha nyingine kutumika, ni sharti iwe katika miktadha tofauti. Jumuiya nzima ya chekechea inapaswa kuunda nyenzo na vielelezo vyenye maandishi katika lugha ya Kiswahili. K.I.E ipange semina juu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili, kwa sababu walimu watavumbua mikakati mipya itakayoendeleza lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea.

## ABSTRACT

The main purpose of this study was to investigate the use of Kiswahili in teaching and learning at the Preschool level. The research was carried out in Webuye Municipality, Bungoma East District of Western Province in Kenya. The study sample was selected through systematic and simple random sampling techniques. The sample comprised of 19 preschool managers, teachers and parents. This number was uniformly used in the above groups. The pre- unit nursery children in all the 19 preschools were incooperated in the sample.

Data was collected by use of questionnaires, interview and observation schedules. Data was analysed through descriptive statistics. Tables, bar graphs as well as pie charts were used in presenting the data. The study was guided by the functionalism theory as advocated by Halliday (1970). This theory explains that language is the main facilitator of learning and teaching.

The study revealed that Kiswahili was used alongside English language and the pupils mother tongue during instruction. There was no seminar held for the preschool teachers on the use of Kiswahili language. It was further established that most of the parents did not advocate the use of Kiswahili language in teaching and learning of their children at the preschool level. However, Kiswahili was the most popularly used language during instruction.

In light of the study findings, it is recommended that the language of the catchment area should be emphasized. In multilingual areas, a language common to all should be used during instruction. Preschools should come up with workable strategies to create teaching aids with Kiswahili wordings. K.I.E should also organize seminars on the use of Kiswahili language, for this will inspire teachers to discover new strategies on the use of Kiswahili language in teaching and learning at the preschools.

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **B** | - | Binafsi |
| **BVLF** | - | Bernard Van Leer Foundation |
| **KIE** | - | Kenya Institute of Education |
| **KNEC** | - | Kenya National Examination Council |
| **MMUST** | - | Masinde Muliro University of Science and Technology |
| **NACECE** | - | National Centre for Early Childhood Education |
| **U** | - | Umma |
| **Uk.** | - | Ukurasa |
| **Taz.** | - | Tazama |

**YALIYOMO**

**Mada** **Ukurasa**

Ikirari ---------------------------------------------------------------------------------------- i

Idhinisho ------------------------------------------------------------------------------------ii

Tabaruku ------------------------------------------------------------------------------------iii

Shukrani ---------------------------------------------------------------------------------iv

Ikisiri ------------------------------------------------------------------------------------------ v

Abstract ---------------------------------------------------------------------------------vi

Vifupisho ------------------------------------------------------------------------------vii

Yaliyomo ------------------------------------------------------------------------------viii

Orodha ya Majedwali ------------------------------------------------------------------ xii

Orodha ya Vielelezo ---------------------------------------------------------------- xiii

Ufafanuzi wa Dhana Zilizotumika ------------------------------------------------- xiv

**1.0 SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ----------------------------------------- 1**

1.1 Usuli wa Utafiti --------------------------------------------------------------------- 1

1.2 Suala la Utafiti ------------------------------------------------------------------- 6

1.3 Madhumuni ya Utafiti -------------------------------------------------------------8

1.4 Maswali ya Utafiti ------------------------------------------------------------ 8

1.5 Misingi ya Uteuzi wa Utafiti ---------------------------------------------------- 9

1.6 Umuhimu wa Utafiti--------------------------------------------------------------- 12

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti------------------------------------------------------ 14

1.8 Nadharia ya Utafiti---------------------------------------------------------------15

**2.0 SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI YA MADA YA UTAFITI ---19**

2.1 Utangulizi ---------------------------------------------------------------------------19

2.2 Maandishi Kuhusu Matumizi ya Lugha Katika Shule za Chekechea ------19

2.3 Matumizi ya Kiswahili katika Shule za Chekechea----------------------------- 21

2.4 Sababu za Matumizi ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea -------------23

2.5 Watumiaji wa Kiswahili Katika Shule za Chekechea -------------------------29

2.6 Changamoto za Kiswahili Katika Shule za Chekechea ----------------------34

2.7 Tafiti za Hivi Karibuni Kuhusu Mada ya Utafiti ---------------------------------38

2.8 Hitimisho ---------------------------------------------------------------------------40

**3.0 SURA YA TATU: NJIA NA MBINU ZA UTAFITI -----------------------------41**

3.1 Utangulizi --------------------------------------------------------------------------41

3.2 Mpangilio wa Utafiti ---------------------------------------------------------------41

3.3 Eneo la Utafiti --------------------------------------------------------------------42

3.4 Watafitiwa --------------------------------------------------------------------------43

3.5 Uteuzi wa Sampuli -----------------------------------------------------------------44

3.6 Nyenzo na Mbinu za Kukusanya Data -------------------------------------------47

3.6.1 Hojaji ------------------------------------------------------------------------------47

3.6.2 Dodoso ----------------------------------------------------------------------------49

3.6.3 Uchunzaji Darasani -------------------------------------------------------------51

3.7 Majaribio ya Vifaa Nyanjani -----------------------------------------------------53

3.8 Utafiti Halisi ------------------------------------------------------------------------54

3.9 Maadili Yaliyofuatwa Wakati wa Kukusanya Data ----------------------------55

3.10 Udhabiti wa Vifaa vya Utafiti ---------------------------------------------------56

3.11 Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti ----------------------------------------------------56

3.12 Matatizo Wakati wa Kukusanya Data -----------------------------------------57

3.13 Utaratibu wa Uchanganuzi wa Data --------------------------------------------57

3.14 Hitimisho --------------------------------------------------------------------------58

**4.0 SURA YA NNE: UWASILISHAJI WA DATA NA MJADALA --------------59**

4.1 Utangulizi ----------------------------------------------------------------------------59

4.2. Usuli wa Shule za Chekechea ---------------------------------------------------60

4.3. Namna Kiswahili Kinavyotumika Katika Shule za Chekechea -------------60

4.3.1 Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea --------------60

4.3.2 Jinsi Kiswahili Kinavyotumika katika Shule za Chekechea ----------------61

4.3.3 Matumizi ya Kiswahili Katika Mafunzo ya Shule za Chekechea ---------62

4.4.0 Watumiaji wa Kiswahili Katika Shule za Chekechea ------------------------64

4.4.1 Miktadha ya Matumizi ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea ---------67

4.4.2. Umilisi wa Walimu Katika Lugha ya Kiswahili --------------------------------69

4.4.3. Mikakati ya Kuendeleza Lugha ya Kiswahili ----------------------------------69

4.5 Changamoto za Matumizi ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea --- 72

4.6 Sababu za Matumizi ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea ------------79

4.7 Maswala Ibuka --------------------------------------------------------------------------89

**5.0 SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO-------91**

5.1. Utangulizi -----------------------------------------------------------------------------91

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafit i---------------------------------------------------92

5.3 Hitimisho.------------------------------------------------------------------------- --98

5.4 Mapendekezo ya Mada ya Utafiti---------------------------------------------------99

5.4.1 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zaidi----------------------------------------------100

**MAREJELEO------------------------------------------------------------------------------102**

**VIAMBATISHI ---------------------------------------------------------------------------112**

KIAMBATISHI I: Barua ya Utafiti---------------------------------------------------112

KIAMBATISHI II: Hojaji kwa Walimu----------------------------------------------113

KIAMBATISHI III: Utaratibu wa Kiongozi cha Uchunzaji------------------------118

KIAMBATISHI IV: Dodoso kwa Wasimamizi wa Chule za Chekechea ------119

KIAMBATISHI V: Dodoso kwa Wazazi wa Shule za Chekechea--------------120

KIAMBATISHI VI: Ramani ya Wilaya Bungoma Mashariki---------------------121

KIAMBATISHI VII:Ramani ya Shule za Chekechea Manispaa ya Webuye -122

KIAMBATISHI VIII: Orodha ya Majina ya Shule za Chekechea----------------123

KIAMBATISHI IX: Barua ya Kuidhinisha Kufanywa kwa Utafiti-----------------124

KIAMBATISHI X: Kibali cha Utafiti--------------------------------------------------125

## ORODHA YA MAJEDWALI

**JEDWALI** **UKURASA**

Jedwali 1: Idadi ya shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye -------------- 47

Jedwali 2: Aina ya shule idadi na nambari ya watafitiwa---------------------------------- 60

Jedwali 3: Namna Kiswahili kinavyotumika katika Shule za Chekechea -------------- 62

Jedwali 4: Matumizi mbalimbali ya Kiswahili katika Shule za Chekechea------------ 63

Jedwali 5: Miktadha ya matumizi ya Kiswahili katika Shule za Chekechea---------- 68

Jedwali 6: Mikakati ya Kuendeleza Kiswahili katika Shule za Chekechea---------- - 71

Jedwali 7: Changamoto za Matumizi ya Kiswahili katika Shule za Chekechea----- 73

Jedwali 8: Sera ya Lugha na Maoni ya Wasimamizi wa Chekechea ----------------- 78

Jedwali 9: Muhtasari wa Sababu za Matumizi ya Lugha ya Kiswahili. ---------------- 80

Jedwali 10: Nyenzo zenye Maandishi katika Lugha ya Kiswahili -------------------------88

## ORODHA YA VIELELEZO

**VIELELEZO**

Kielelezo 1: Watumiaji wa lugha ya Kiswahili----------------------------------------------66

Kielelezo 2: Umilisi wa walimu katika lugha ya Kiswahili--------------------------------70

## UFAFANUZI WA DHANA ZILIZOTUMIKA

**Lugha ya eneo** : Ni lugha ya matumizi mapana katika eneo la utafiti.

**Sera** : Ni tamko au uamuzi rasmi unaotolewa na serikali, kuhusu jinsi ambavyo shughuli fulani, inafaa kuendelezwa kote nchini. Pia ni hali rasmi ya kutoa mwongozo kuhusu namna jambo linafaa kuendelezwa.

**Chekechea** : Ni neno linalotumiwa kuashiria asasi za elimu za watoto wadogo zilizo tofauti na mazingira ya nyumbani.

**Shule za Kibinafsi** : Shule zinazomilikiwa na kusimamiwa na watu binafsi au shirika la watu binafsi.

**Shule za umma** : Shule ambazo zinasimamiwa na kufadhiliwa na jumuiya.

**Lugha mama** : Hufafanua lugha ambayo mtoto alijifunza kwanza. Ni lugha ambayo huzungumzwa na watu wa eneo moja.

**Ujifunzaji wa lugha** : Hurejelea hatua ya kuongeza au kupata maarifa, ujuzi katika lugha kupitia kwa kusoma tajriba au kufunzwa.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia mambo yafuatayo: usuli wa utafiti, suala la utafiti lenyewe lengo la utafiti, maswali ya utafiti, misingi ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti na nadharia ya utafiti.

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Suala la matumizi ya lugha limezua mijadala anuwai kutoka kwa wataalamu na waandishi (Akhusama, 1984, Simala, 2006). Utata wa mjadala huu unajitokeza wakati wa kupigia debe lugha inayostahili kutumiwa katika mafundisho. Nchini Kenya Lugha za Kienyeji, Kiingereza na Kiswahili ni lugha zitumiwazo katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea. Wanafunzi wa chekechea waliozaliwa na kukulia nje ya miji huzungumza lugha yao ya kwanza, kando na lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Wajiungapo na shule za chekechea, hufunzwa Kiswahili na Kiingereza kama lugha yao ya pili. Kwa mujibu wa utafiti huu, nimejikita katika shule zilizopo katika Manispaa ya mji wa Webuye.

Tafiti zilizofanywa na makala yaliyoandikwa yametudokezea kuwa sera ya lugha nchini Kenya ni ya kulegalega. Haya yanadhibitishwa wakati ambapo Ipara (2001) anapodahili kuwa hakuna mpaka mahsusi kimatumizi, kati ya lugha moja na nyengine katika shule za chekechea. Japo Kiswahili ni lugha mojawapo ya mafunzo, Barasa (1997) anatoa kauli kuwa lugha ya Kiswahili haiwezi kutegemewa kama lugha ya mafundisho, ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza ambayo ilipewa msingi tangu zama za ukoloni mkongwe.

Matundura (2008) anashadidia wazo la Barasa (1997), anaposema kuwa lugha ya Kiswahili haijapewa hadhi katika ufunzaji na ujifunzaji kwenye asasi za elimu.

Mvutano uliopo kuhusiana na matumizi ya lugha hizi, unatokana na umuhimu unaotekelezwa nazo katika jamii. Lugha hizi ndizo zitumiwazo kwa wingi katika asasi za elimu ijapokuwa katika viwango tofauti. Kembo-Sure (1991) katika mojawapo ya utafiti wake, aligundua kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo inayotumiwa kwa wingi katika asasi za elimu kuliko lugha ya Kiingereza. Anatilia nguvu hoja hiyo kwa kusema kuwa, umuhimu wa lugha ya Kiswahili, hauwezi kulinganishwa na lugha ya Kiingereza au lugha za Kienyeji. Mojawapo ya malengo ya shule za chekechea, ni kuandaa mwanafunzi katika lugha ya maeneo. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mafunzo ya shule za chekechea, yanaweza kueleweka vyema tutazamapo sera rasmi ya lugha ya wizara ya elimu, ambayo hupendekeza lugha inayotumiwa sana katika maeneo husika.

Broughton (1980) anatudokezea vipengee vya kuzingatiwa katika kuamua lugha ya mafunzo navyo ni; Sifa za lugha za mafundisho, upataji wa stadi mahususi kama vile kuzungumza, kusoma na kuandika. Kwa mujibu wa vipengele vilivyoorodheshwa, lugha ya Kiswahili ni faafu kwa vile ni mojawapo ya lugha za mafunzo katika shule za chekechea, ni lugha inayotumiwa katika eneo kwa vile inaeleweka vyema na wakazi wa eneo la mtafiti.

Suala la lugha ya mafundisho liliangaziwa na Tume ya Gachathi (1976). Pendekezo nambari 101 kuhusu sera na mipango ya lugha nchini Kenya lasema kwamba, lugha inayotumiwa sana katika eneo la shule ya chekechea, iwe ndiyo itakayotumika kufundishia shule za chekechea na madarasa matatu ya mwanzo katika shule za msingi. Kuanzia darasa la nne, Kiingereza kilipaswa kuchukua nafasi kubwa kama lugha ya kufundishia

Tume ya Mackay (1981) ilinyanyua hadhi ya lugha ya Kiswahili kwa kupendekeza kuwa lugha ya Kiswahili kuwa somo la lazima katika chuo kikuu cha pili cha Moi. Pendekezo hili lilitokana na ung'amuzi kwamba, wanafunzi waliokuwa wanamaliza vyuo vikuu hawakuwa na uwezo wa kuwasiliana vyema kwa kutumia Kiswahili. Licha ya umuhimu wa pendekezo hili, halijatekelezwa mpaka sasa. Maswali ambayo tulilazimika kujiuliza, ni kwa nini ilipendekeza Kiswahili kuwa somo la lazima katika chuo kikuu cha pili cha Moi? Changamoto katika matumizi ya lugha ya Kiswahili huenda chanzo chake ni shule za chekechea. Majibu ya maswali haya yalikuwa muhimu kwa utafiti huu, kwa sababu yalituwezesha kuchunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye msingi wa elimu ambao ni chekechea. Hivi punde, nchini Kenya na hasa katika sehemu za miji, mtoto wa chekechea ambaye huwa kati ya miaka 3-6 anatarajiwa kupokea elimu ya chekechea kwa miaka miwili au mitatu kabla hajajiunga na shule ya msingi. Wanapokuwa katika shule hizi hufunzwa masomo kama vile Hesabu, Ubunifu, Lugha, Mazinigira, Sayansi, Michezo ya nje na ya ndani kwa lugha eneo ambayo yaweza kuwa Kiswahili, Kiingereza au mseto wa lugha hizi mbili.

Ngugi (1987) anadai kuwa lugha zetu, ndizo vyombo muhimu vya kujengea Bara lenye utamaduni na maisha ya Kiafrika. Anatoa kauli kuwa ni rahisi mno watoto kujieleza, kuelewa dhana, na hata kutangamana katika lugha ya maeneo kwa vile zama zao kabla hawajaanza shule, kondeni au malishoni palikuwa kama shule za chekechea, ambapo walipata fursa ya kutambiana hadithi walizoganiwa na wakubwa wao.

Ukosefu wa sera madhubuti miongoni mwa shule za chekechea za mijini, unaweza ukayumbisha matumizi ya lugha ya Kiswahili shuleni kama wanavyodai (Mazrui na Mazrui, 1995). Kutokuwepo kwa sera maalum, huashiria kulegalega kwa hali ya matumizi ya lugha, hivyo kutoa msingi mbovu wa lugha ya Kiswahili. Mulama (1994) akimunukuu aliyekuwa mwenyekiti wa chama cha walimu nchini Kenya, Bw. Ng'ang'a, alichangia kuwa wazazi wengi hupendelea watoto wao kufundishwa kwa lugha ya Kiingereza. Maoni sawa na haya huonyesha kuwa lugha ya Kiswahili imepewa hadhi ya chini.

Lugha ya Kiswahili nchini Kenya ina sifa za mawasiliano mapana. Kwenye eneo la utafiti mjini Webuye, Kiswahili hutumiwa katika mitagusano na mawasiliano miongoni mwa wana jamii. Hivyo kuna uwezekano kwamba, watoto wanapozaliwa, na hata kufikia umri wa kuweza kufikiria na kuzungumza, huwa hawana chaguo ila kuwasiliana na wanajamii katika lugha sambazi ambayo huwa ni Kiswahili.

Watoto waingiapo shule za chekechea hutumia lugha wanayoielewa katika miktadha ya darasani, michezoni na hata wakati wa mankuli. Sababu ya kufanya hivi ni kuwa, watoto hujieleza kwa urahisi, wanapohamisha mandhari ya lugha ya nyumbani na kuyaleta shuleni. Tukiyarejelea maoni ya Ngugi (1987) kuhusu mada hii, anadai kuwa watoto huhamisha ufahamu wa dhana kutoka lugha ya kwanza, hadi lugha ya pili. Anapendekeza wafundishiwe katika lugha ya pili, punde wanapokuwa na ufahamu mwafaka wa lugha eneo.

Lugha hutumiwa kutegemea jinsi inavyyovutia wazungumzaji wake. Lugha hutumiwa kwa wingi au uchache, kulingana na majukumu ambayo lugha imepewa (Wardhaugh, 1987). Mtafiti alitaka kufahamu nafasi ambayo lugha ya Kiswahili imetwikwa katika shule za chekechea kwenye eneo la utafiti.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili yameathiriwa pakubwa na viwango vilivyotofautiana vya matumizi ya lugha katika shule za chekechea za binafsi na za umma. Matumizi haya yamechochewa na kasumba za kikoloni na ukosefu wa mikakati ya watekelezaji mitaala rasmi ya chekechea. Kutokana na nafasi bora na majukumu anuwai ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya, ni jambo linalofaa iwapo tutajizatiti kujenga msingi wa lugha ya Kiswahili, utakaoanzia shule za chekechea na utakaompa mwanafunzi uwezo wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika vyema katika Kiswahili. Wanasaikolojia wanaamini kuwa katika umri huu, ndipo watoto hujifunza kwa kasi mno kinyume na wakati mwingine wa maisha ya binadamu (Kembo, 2002). Hii ndiyo mojawapo ya sababu zilizoibua maswali katika fikra za mtafiti, kwa vile matumizi ya Kiswahili yasiyokuwa na msingi mwema ambao ni

chekechea, huweza kuathiri ufasaha wa lugha ya Kiswahili, na kuzua uwezekano wa Kiswahili kutotumika au kupewa nafasi duni. Ili lugha ya Kiswahili ijengwe kwa msingi wa ufasaha, ni sharti watoto wa chekechea wapewe mazoezi katika stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.

### 1.2 Suala la Utafiti

Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji kwenye asasi za elimu ni ya kusikitisha. Matokeo ya mitihani ya kitaifa katika somo la Kiswahili ya darasa la nane na kidato cha nne yameendelea kudidimia. Malalamishi ya waziri wa elimu kupitia vyombo vya habari katika hotuba yake yalithibitisha kutoridhika kwake. Hii ilikuwa baada ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne wa mwaka 2007 kutangazwa. Ipara (2001), alilalamikia kuzorota kwa hadhi ya lugha ya Kiswahili katika asasi za elimu. Hali hii anavyoeleza Ipara, hudhihirika wanafunzi washindwapo kujieleza katika lugha ya Kiswahili.

Ingawa sera ya lugha katika shule za chekechea hupendekeza matumizi ya lugha za maeneo, mandhari ya lugha katika shule za chekechea ni ya wingi lugha. Hili linatokana na mashindano baina ya lugha hizi, na umaarufu wa lugha ya Kiingereza dhidi ya lugha za Kiswahili na Kienyeji. Hii inamaanisha kuwa kuna pengo kubwa kati ya sera rasmi ya lugha ya kitaifa na hali halisi nyanjani. Kutanda kutoka kwa lugha ya Kiswahili kwa Kiingereza, Kiingereza kwa Kiswahili na Kiswahili kwa Kibukusu katika mandhari ya chekechea huashiria ukosefu wa ufasaha. Tukizingatia hali ya lugha kwenye shule za chekechea katika eneo la utafiti, tunagundua kuwa walimu na wanafunzi

wana uhuru wa kuchagua lugha ya kutumia wakati wa ufunzaji na ujifunzaji, hili humaanisha kuwa hakuna juhudi zozote katika kujifunza lugha mahususi kwa undani.

Lugha ambayo haijapewa msingi faafu haiwezi ikategemewa kuzalisha kizazi kitakachotumia lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji. Wazo hili ndilo lililomchochea mtafiti kuchunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea. Shauku ya kutaka kujua nafasi ya lugha ya Kiswahili katika mandhari ya wingi lugha, ndiyo iliyokuwa kichochezi kikubwa, kwani lugha ya Kiswahili isipowekewa msingi mzuri ambao huwa ni katika shule za chekechea huathiri ufunzaji na ujifunzaji katika viwango vya shule za msingi hadi vyuo vikuu.

Makala yaliyoandikwa na Barasa (1997) na Ipara (2001) kuhusu nafasi ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye shule za sekondari, yalionyesha kuwa kiwango kinachowekewa msingi ambacho huwa ni shule ya chekechea hakijashughulikiwa ipasavyo, mapengo yaliyojitokeza katika kazi za wawili hawa yalinipa msukumo wa kuchunguza matumizi ya Kiswahili katika shule za chekechea.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza matumizi ya Kiswahili kwa mafunzo ya shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye. Ili kutimiza lengo hili, tuliongozwa na madhumuni mahususi yafuatayo:

a) Kubainisha namna Kiswahili kinavyotumika katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea.

b) Kutambua sababu zinazochochea matumizi ya Kiswahili katika shule za chekechea.

c) Kuainisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za chekechea.

d) Kukadiria changamoto zinazokumba matumizi ya Kiswahili katika mafunzo ya shule za chekechea.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

a) Kiswahili kinatumika vipi katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea?

b) Ni sababu zipi zinazopelekea kutumika kwa Kiswahili katika mafundisho ya shule za chekechea?

c) Watumiaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea ni akina nani?

d) Matumizi ya Kiswahili katika shule za chekechea yanakumbwa na changamoto gani?

### 1.5 Misingi ya Uteuzi wa Utafiti

Kuna tafiti zilizofanywa juu ya matumizi ya lugha. Baadhi ya tafiti hizo ni zile zilizofanywa nchini Kenya na Karega (2001) na Chieni (2001). Mtafiti alipochunguza tafiti hizi, aligundua kuwa zilishughulikia matumizi ya lugha katika viwango vya sekondari na shule za msingi, katika mikabala tofauti. Tofauti kati ya tafiti hizo na huu ni kuwa, utafiti huu ulishughulikia matumizi ya Kiswahili katika mafunzo ya msingi wa elimu ambao ni shule za chekechea.

Pili, uchunguzi wa maandishi mbalimbali alioufanya mtafiti, umedhihirisha kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea haujafanywa tangu miaka ya tisini wakati ambapo serikali ilianza kudhamini shule za chekechea. Uchache wa tafiti hasa zinazohusu matumizi ya lugha ya Kiswahili, utaupa utafiti huu nafasi ya kukadiria nafasi ambayo Kiswahili kimepewa katika shule za chekechea.

Tatu, matumizi ya lugha huchochewa na mazingira yanayomzunguka mtoto na hudhihirisha mielekeo ya wanajamii kuhusiana na umaarufu wa lugha lengwa. Ni jambo linalokubalika kuwa, wakazi wengi wa miji ya wilaya ya Bungoma huzungumza Kiswahili.

Nne, mtafiti aling'amua kuwa Kiswahili kimepata hadhi lakini lugha hii inatishwa na matatizo ya ushindani na lugha zingine za mafundisho. Kwa hivyo Kiswahili kama somo na lugha ya kufundishia inahitaji uangalifu mkubwa kutoka kwa wadau wote kama serikari, wazazi na wanafunzi kwa sababu ya nafasi zao.

Tano, kuna tafiti chache ambazo zina ushahidi kuhusu umuhimu wa matumizi ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji. (Barasa, 1997) na (Muruguru, 2000), kwenye asasi za elimu nchini Kenya. Kutokana na mapitio ya maandishi yaliyopo, hakuna utafiti wowote ambao umefanywa kuhusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea. Kwa hivyo, vigezo hivi vilikuwa toshelevu vya kusababisha utafiti wa aina hii kufanywa.

Sita, Kiswahili ni lugha ya mafundisho katika shule za chekechea hadi madarasa ya kwanza matatu katika shule za msingi. Hivyo somo ambalo ni maarufu katika ngazi zote za elimu lazima lina umuhimu wa kipekee. Kembo-Sure (1994) anashadidia hoja hiyo anaposema kuwa, Kiswahili kinapendwa na wanafunzi badala ya Kiingereza. Sababu ni kuwa kinaweza kutumika katika mandhari rasmi na yasiyo rasmi.

Saba, umuhimu wa lugha za Kiafrika unashadidiwa na Nabwire (2002), alipodahili kuwa Kiswahili husababisha mshikamano wa kitaifa kwa kuunganisha watu wa aila mbalimbali kimawasiliano. Kimsingi lugha ya Kiswahili ni moja wapo ya lugha za Kiafrika ambayo hutekeleza majukumu ya kuunganisha umma. Hivyo, msingi mzuri wa matumizi ya lugha ya Kiswahili ukiwekwa katika shule za chekechea, utaimarisha upataji na matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa kizazi kijacho. Matumizi ya Kiswahili ni muhimu katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea, hivyo watoto wa chekechea wanapopewa msingi unaofaa katika lugha hii, hujenga daraja ya ufasaha wa

lugha. Ukuaji wa lugha ya Kiswahili hutegemea matumizi yake ya kila siku katika mandhari ya ufunzaji na ujifunzaji lugha katika shule za chekechea.

Nane, Halliday (1970) anatoa kauli kuwa kati ya umri wa miaka 3-6, watoto hushika mambo kwa haraka, kinyume na umri mwengine katika maisha ya binadamu. Watoto wengi wa chekechea huwa kati ya miaka 3-6. Hivyo wanapoandaliwa vyema katika matumizi ya Kiswahili, wanaweza kuinua kiwango na ufahari wa lugha ya Kiswahili.

Mapitio ya maandishi ya Ipara (2001) na Kembo (2000) yanaonyesha kuwa wanafunzi wengi wa chekechea hutagusana katika lugha ya Kiswahili, mojawapo ya lugha za ufunzaji na ujifunzaji. Hata hivyo matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mandhari ya shule za msingi na za sekondari hayadhihirishi msingi faafu wa matumizi ya lugha hiyo katika shule za chekechea. Utafiti huu ulikuwa faafu kwa vile matokeo yake yangeangazia pengo lilopo kati ya tafiti za awali kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili na utafiti huu. Nilitarajia kuwa walimu na wanafunzi wa chekechea wangeboresha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika miktadha ya ufunzaji na ujifunzaji darasani. Kutokana na maoni ya wataalamu hawa, kuna uwezekano mkubwa wa kutumia Kiswahili katika mafundisho, iwapo msingi unaofaa ambao huwa ni katika shule za chekechea utashadidiwa kupitia kwa stadi ya kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Ni matarajio ya mtafiti kwamba, utafiti huu unaweza kuwasaidia walimu wanao hudumu kujisaili na kujisaka, ili kuboresha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji. Hili litatokea tu iwapo watatilia maanani matokeo ya utafiti huu.

Matumizi ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji, utakiandaa kizazi kilicho na umilisi wa lugha. Kwa vile wanasaikolojia wanaamini kuwa katika umri wa miaka 3-6, ambao hushirikisha watoto wengi wa shule za chekechea, hujifunza lugha kwa kasi mno kinyume na wakati mwingineo katika maisha ya binadamu.

Utafiti huu ni muhimu kwa vile utatuwezesha kuelewa vigezo vinavyochochea matumizi ya lugha hii katika shule za chekechea. Walimu wataweza kunufaika, kwa vile wataweza kuelewa vipengele vya kutilia mkazo katika matumizi ya lugha. Vilevile utafiti huu utamwezesha mwalimu kuzingatia matumizi ya stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika, wakati anapotumia lugha ya Kiswahili katika mafundisho ya shule za chekechea.

Wakuza mitaala wataweza kunufaika kutokana na matokeo ya utafiti huu, kwa kuwa watawezeshwa kuteua vipengele vinavyofaa, mbinu na nyenzo za kufundishia lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu kumekuwepo na malalamishi kutoka kwa watekelezaji mitaala kuhusu lugha za mafundisho.

Matokeo ya utafiti huu yatanufaisha serikali na wizara ya elimu kudhibiti sera ya lugha katika shule za chekechea, za binafsi na umma. Haya yametokana na kuchipuka kwa sera zisizo rasmi, hasa katika shule za chekechea za kibnafsi kama tunavyodokezewa na (Ipara, 2001).

Data iliyokusanywa inaweza kurejelewa na walimu wa chekechea na hata katika vyuo mbalimbali vya chekechea, vinavyozingatia sera rasmi ya lugha kutoka wizara ya elimu. Katika muktadha huu, walimu na wanafunzi wa Kiswahili watafunzwa kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Idara ya lugha na fasihi katika chuo kikuu cha Masinde Muliro, itafaidika kutokana na utafiti huu, kwa vile wanafunzi watafiti watapata marejeleo ya data itakayotumika katika kuwafunza walimu na wanafunzi wa lugha ya Kiswahili.

Kanuni za matumizi ya lugha ya pili ni sawa kimsingi. Hivyo mchango wa utafiti huu utafaidi lugha zingine kama vile Kiingereza, Kifaranza na hata Kijerumani katika matumizi ya lugha katika miktadha ya ufunzaji na ujifunzaji katika shule za chekechea na katika asasi za juu za elimu.

Utafiti huu unanuia kuboresha matumizi ya Kiswahili katika asasi za elimu, hasa tukirejelea lugha tamkwa na andishi ya Kiswahili ambayo hujengewa msingi katika shule za chekechea. Mwishowe, tafiti za Kiswahili ni chache mno na kwa hivyo, utafiti huu utachangia pakubwa na kufanya ziongezeke.

### 1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Mtafiti aliangazia tu eneo la kijiografia la Manispaa ya Webuye, katika Wilaya ya Bungoma Mashariki, kwa vile wakazi wengi wa eneo hili ni watu mseto wanaotumia Kiswahili katika mawasiliano na mitagusano yao. Hivyo mtafiti alichukulia kuwa eneo hili lingempa fursa nzuri ya kuchunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika miktadha ya ufunzaji na ujifunzaji.

Utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya Kiswahili katika mafundisho ya shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye. Ili kufikia upeo tuliokusudia, tulichunguza namna Kiswahili kinavyotumika, watumiaji wa lugha hii, sababu za kuitumia, na changamoto zinazokabili lugha hii. Hatukujishughulisha kamwe na vipengele mahususi, kama vile umilisi wa lugha ya Kiswahili wakati wa ufunzaji na ujifunzaji.

Eneo la utafiti linaonekana finyu likilinganishwa na nchi nzima. Hata hivyo mtafiti anatarajia kuwa kina cha utafiti huu kitaweza kuibua data halisi ambayo inaweza kuangazia yale ambayo yanaweza kuwa yanatendeka katika Manispaa zingine zenye sifa kama Manispaa ya Webuye nchini Kenya.

Utafiti huu haukushughulikia shule zote za chekechea katika Manispaa hii, bali shule 19 kati ya 62 zilizosajiliwa. Mtafiti pia alijishughulisha na kitengo cha tatu cha chekechea, ambapo wanafunzi huwa wamepata ujasiri wa kutangamana vyema baina yao na walimu. Pia wazazi na walimu wote wa chekechea hawakuhusishwa bali asilimia thelathini ya idadi jumla ya walimu 19 na wazazi 19.

## 1.8 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika nadharia ya uamilifu wa lugha iliyoasisiwa na Halliday (1970). Ameorodhesha vitengo vya uamilifu wa lugha kama vile: mzungumzaji, ujumbe, msikilizaji, muktadha, msimbo na mkondo. Kwa mujibu wa Halliday (1970) kitengo cha muktadha hufanya uamilifu wa kiurejeleo ambao ndio muhimu kulingana na muktadha. Uamilifu wa kujieleza humlenga mzungumzaji.

Uamilifu wa kishirikishi hudhamiria kuhifadhi mawasiliano baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Nao uamilifu wa kifahamivu unahakikisha kuwa msimbo unaofahamika kwa pande zote unatumiwa. Mwisho, uamilifu wa kiburudani hulenga ujumbe wenyewe bila ya kuhuhusisha na kitu cho chote. Halliday (1970) vile vile anafafanua vitengo vitatu vikuu vya uamilifu wa lugha ambavyo ni; Uamilifu wa kiuwakilishi, ambapo mzungumzaji huwasilisha tajriba yake, ile ya jumuiya lugha na mazingira yake. Pili uamilifu wa kihusishi ambapo maelezo ya kibinafsi na mitagusano ya kijamii kama vile wazungumzaji hujiingiza katika kauli ya hali na kauli ya hali tendo na mwisho, uamilifu wa kimatini ambapo lugha huwa matini, inayojihusisha yenyewe na muktadha ambamo inatumiwa. Lugha sharti itumiwe kulingana na muktadha wake wa hali. Pasipo kitengo cha kimatini cha maana, hatuwezi kutumia lugha kwa vyovyote vile.

Nadharia hii inasema kuwa, mzungumzaji ambaye anaifahamu lugha au aina ya lugha nyingi anaweza kuchagua aina ya lugha kati ya hizo, ambayo inafaa katika muktadha wa hali fulani. Kusudi kubwa la lugha yoyote ni mawasiliano

baina ya mzungumzaji na msikilizaji/wasikilizaji. Kwa kuzingatia mwelekeo huu, mtafiti alichukulia kuwa lugha ya Kiswahili katika muktadha wa shule za chekechea za eneo la utafiti inajulikana vyema miongoni mwa wazungumzaji ambao ni walimu na wanafunzi wa shule hizi. Kutokana na ufaafu wa lugha hii, inaweza kutumiwa katika ufunzaji na ujifunzaji.

Mawasiliano hubainika tu wakati msikilizaji ameathiriwa na mazungumzo ya mzungumzaji. Wakati mwalimu na wanafunzi wanapokuwa darasani, msimbo ukiwa lugha ya Kiswahili, mawasiliano hudhihirika wakati ambapo wanafunzi na walimu hutagusana wakati wa ufunzaji na ujifunzaji. Ithibati ya pekee kwamba pande zote zinaelewa lugha, ni uwezo walio nao walimu na wanafunzi wa kujibu maswali katika lugha ya Kiswahili.

Nadharia ya uamilifu ilihusishwa katika utafiti huu, kwa vile ilimsaidia mtafiti kudhihirisha ikiwa walimu na wanafunzi wana uwezo wa kuwasiliana katika lugha ya Kiswahili. Data tuliyoikusanya ilionyesha kuwa ni mojawapo ya lugha za mafunzo, Tulitarajia kutumia nadharia ya uamilifu katika kuchunguza na kujibu maswali yafuatayo: Je, kuna mipaka ya matumizi ya kila lugha? Kwa nini Kiswahili kinatumika? Je, lugha ya Kiswahili hutumiwa kwa namna gani? Watumiaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea ni nani? Ni changamoto zipi zinazoikumba lugha ya Kiswahili? Je, ni mambo gani yanayomfanya mzungumzaji aamue kutumia lugha fulani badala ya nyengine?

Nadharia hii ilichangia kuchunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili baina ya walimu na walimu, walimu na wanafunzi na miongoni mwa wanafunzi wa chekechea. Pia tuliweza kukadiria matumizi ya Kiswahili katika mandhari ya darasani, na hata katika michezo ya nje. Ili mitagusano ifaane baina ya walimu na wanafunzi wa chekechea, ni sharti kuwe na kiungo ambacho ni lugha kinachowaunganisha, nayo kwa mujibu wa utafiti huu ni lugha ya Kiswahili.

Nadharia ya uamilifu inajumuisha vielelezo kadhaa. Kwanza, inajumuisha kielelezo cha Fishman (1965, 1972) katika Kennedy (1989). Alieleza kuwa, ili tuelewe matumizi ya lugha, inatupasa kujua anayezungumza, anazungumza na nani na kwa madhumuni gani. Nadharia hii ilitusaidia kuchunguza ikiwa walimu na wanafunzi wa chekechea, walizingatia vipengele vya matumizi ya lugha walipotumia Kiswahili katika miktadha ya mafundisho na iwapo kwa kufanya hivyo walizingatia kujenga msingi bora wa lugha ya Kiswahili ndani mwao.

Kwa mujibu wa utafiti huu, lugha zinazotumiwa katika mafundisho kwenye shule za chekechea ni Kiswahili, Kiingereza na lugha za kienyeji. Kati ya lugha hizi, tulikusudia kufahamu iwapo lugha ya Kiswahili, imeathiriwa na hali ya daiglosia katika eneo la utafiti. Kwa hivyo, tulitumia vipengele vya nadharia ya uamilifu kama vile wazungumzaji, wasikilizaji, ujumbe, miktadha msimbo na mikondo katika utafiti wetu. Kwa mujibu wa nadharia yetu, wazungumzaji na wasikilizaji ni wanafunzi/walimu wa chekechea. Mandhari ya mafundisho katika shule za chekechea huhamishwa, wakati mwingi wamo darasani au

michezoni. Ujumbe ni funzo lililoandaliwa huku msimbo ukiwa ni lugha ya Kiswahili, ilhali mikondo ikiwa mbinu za ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

# SURA YA PILI

## 2.0 UHAKIKI WA MAANDISHI YA MADA YA UTAFITI

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inarejelea mapitio yanayolenga maandishi yanayohusiana na matumizi ya Kiswahili katika mafundisho ya shule za chekechea. Mapitio haya yaliangazia namna Kiswahili kinavyotumika, sababu za kutumia Kiswahili, watumiaji wa lugha ya Kiswahili na changamoto zinazokabili matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea.

### 2.2 Maandishi Kuhusu Matumizi ya Lugha katika Shule za Chekechea

Filmore (2000) anataja kuwa walimu wanaowahudumia watoto wa chekechea ni sharti wawe waangalifu kuhusu mazingara wanayoandaa kupitia lugha watumiayo wakati wa mafunzo. Ingawa hakurejelea lugha ya Kiswahili, maoni aliyoyatoa Filmore (2000) yanafaa mno utafiti huu, kwa vile matumizi ya lugha kwenye shule za chekechea huangazia mno mwalimu ambaye huigwa na wanafunzi. Mtafiti anatazamia kuwa walimu wanaoandaa mazingira mabovu ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea, huweza kuathiri umilisi wa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili.

Kabiru na Birich (1995), wanasema kuwa mtoto wa chekechea atumiapo lugha hupanua msamiati na hasa anapowasilisha mahitaji yake kupitia lugha tamkwa. Wataalamu hawa wanatoa nasaha kwa wazazi na walimu watumie lugha sanifu wakati wanapotagusana na wanafunzi. Ingawa mapendekezo yalikuwa mazuri, lakini suala la usanifu wa lugha ni changamano na linapaswa kuchunguzwa kwa makini. Ingawa walilenga lugha ya Kiswahili,

umuhimu wa lugha tamkwa ulifaa mno utafiti huu kwa vile tulichunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika miktadha halisi. Hata hivyo, kwa upande mwingine, Mkwizu (2002) anashikilia kuwa, kiwango cha elimu cha mwalimu ndicho huashiria uwezo na umilisi wa kutumia lugha. Mchango wa wataalamu hawa unaonyesha kuwa mwalimu ndicho kiungo cha kati kinachotegemewa kufaulisha matumizi ya lugha katika shule za chekechea. kwa mujibu wa utafiti huu tuliangazia nafasi ya mwalimu wa chekechea katika matumizi ya lugha ya Kiswahili wakati wa ufunzaji na ujifunzaji.

Ingawa nafasi ya mwalimu ni muhimu katika ufunzaji na ujifunzaji, Pluckrose (1987) japo hakulenga lugha ya Kiswahili, anatoa kauli kuwa matumizi ya lugha huchochewa pakubwa na matumizi ya nyenzo, vielelezo kama vile maumbo ya watu, magari, wadudu, maandishi kwenye mikebe na chupa. Vitu hivi huteka nathari ya mwanafunzi haraka mno, kiasi kwamba huvutiwa kusoma maneno yale mara kwa mara. Wazo muhimu la Pluckrose ni kuwa yapasa mwalimu afundishe kwa kutumia nyenzo. Tukirejelea utafiti huu, matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea yanapaswa kuandamana na nyenzo. Kwa vile wanafunzi wa chekechea humaizi mada vyema iwapo watafundishwa huku wakionyeshwa kuliko stadi ya kusikiliza. Uelewa wao hurahisishwa wanapotumia nyenzo kwa vile humwezesha mwalimu kunata uwezo wa wanafunzi wa kusikiliza na hivyo kuelewa dhana haraka.

## 2.3 Matumizi ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea

Namna lugha ya Kiswahili inavyotumika ni muhimu kwani huchochea mawasiliano. Obura (1990) anapendekeza matumizi ya nyimbo, hadithi na ushairi katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea. Sababu anazotoa ni kuwa, lugha ni kiungo cha kati katika shule na madarasani. Mandhari ya shuleni yamejaa lugha tamkwa na andishi; kwenye vibandiko, ubao, nyenzo, vielelezo na hata vitabuni. Madai haya yanaenda sambamba na Chimerah (1988), anaposema kuwa walimu madarasani huzungumza kwa asilimia sabini kumaanisha kuwa ufunzaji na ujifunzaji hauwezi kufanyika pasipo lugha. Linalojitokeza kutokana na maoni ya wawili hawa ni kuwa, walimu wanapaswa kuwa vyombo vya kuigwa na wanafunzi wa chekechea, wanapozungumza lugha ya Kiswahili katika mandhari ya chekechea. Utafiti ulilenga kugundua namna lugha ya Kiswahili inavyojitokeza katika mandhari ya ufunzaji na ujifunzaji, katika shule za chekechea.

Kimui (1988) anadahili kuwa, matumizi ya nyenzo kwa kiwango kikubwa hutegemea umilisi na upatikanaji wake shuleni, kwani maneno pekee huchosha akili ambazo hazijakomaa za watoto ambao huwa katika shule za chekechea. Matumizi ya nyenzo za kufundishia zenye maandishi katika lugha ya Kiswahili, zinaweza kuwa muhimu katika muktadha wa ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea.

Utafiti uliofanywa na Gibbons (1989) Katika Kennedy, (1989) ulifichua ya kuwa shule zilizopaswa kufundishia katika lugha ya Kiingereza hazikuzingatia hili, bali mazungumuzo yao yalitanda kutoka Kiingereza hadi Kichina.

Matokeo ya utafiti wa Gibbons, yakilinganishwa na hali ya lugha katika shule za chekechea katika eneo la utafiti, yalimchochea mtafiti kutaka kujua matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea kwenye Manispaa ya mji wa Webuye. Broughton (1980) anachangia kuwa, lugha haifunzwi kwa kuizungumzia bali kwa kuitumia katika mawasiliano. Mawazo ya Broughton ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile yaliangazia miktadha halisi ambamo lugha hutumika. Utafiti huu ulichunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea, kwa kuzingatia miktadha halisi ambapo jumuiya ya chekechea ilishirikishwa katika mawasiliano. Chimerah (1988) anatoa kauli kuwa mtoto anapokuwa kwenye kundi linalozungumza lugha fulani huzoea lugha hiyo. Maoni yaliyotolewa na msomi huyu ni kwamba mazingira yanaathiri lugha ya mtoto. Mawazo ya Chimerah yanahusu lugha kwa jumla, hajalenga lugha mahsusi. Katika utafiti huu, mtafiti aliangalia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea.

Kembo-Sure (1991) anadahili kuwa hakuna mpaka mahsusi kati ya upataji wa lugha na matumizi yake. Michezo miongoni mwa watoto, sifa yao ya udadisi huchochea matumizi ya lugha, kwa vile watoto huweza kuzua msamiati mpya kutokana na mitagusano yao na vile vile wapewapo fursa ya kutalii mazingira waliyomo kwa kuchora, kuandika majina kwenye vitu halisi kama vile mawe, mikebe na vibandiko. Utafiti huu, ulijikita katika kuchunguza miktadha halisi ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mandhari ya chekechea. Utafiti ulinuia kuchunguza uhalisia wa matumizi ya lugha ya kiswahili; Katika michezo, nyimbo na hata katika mitagusano. Utafiti ulidhihirisha kuwa, matumizi ya Kiswahili katika shule hizi yalijitokeza hasa katika mitagusano, hata hivyo

kipengele cha ubunifu kilikosekana kutokana na nyenzo haba za maandishi katika lugha ya Kiswahili.

Kembo-Sure (1994) anataja kuwa mara tu watu wagunduapo kuwa hawajawekewa masharti kuhusiana na lugha ya mawasiliano katika mandhari mbali mbali, kuna uwezekano kuwa sheria zinazotawala lugha zinaweza kupuuzwa. Charlotte (2001) anatoa maoni kuwa matumizi mabaya ya lugha, yamepenyeza kwa wasomi na wasiosoma na hata darasani. Mawazo haya yalikuwa muhimu kwa utafiti huu, kwa vile tuliwezeshwa kuelewa kwa undani iwapo shule za chekechea zimeathiriwa na matumizi mabovu ya lugha ya Kiswahili. Mchango wa Meerkotter (2002) ulishadidia hoja ya Charlotte alipotoa kauli kuwa kuchanganya na kubadili msimbo ni jambo la kawaida madarasani, ambalo huwasaidia wanafunzi na walimu kufafanua dhana kwa wepesi. Maoni ya Meerkotter (2002) na Kembo-Sure (1994) yanaonyesha kuwa matumizi mabovu ya lugha ya Kiswahili yana uhalisia.

## 2.4 Sababu za Matumizi ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea

Lugha ya Kiswahili ina sifa za matumizi mapana kwa vile inaweza kutumiwa kufundishia masomo mengine kwenye mtaala. Haya yamethibitishwa na Omulando (2002) aliyefanya utafiti wa kubainisha athari ya lugha ya Kiswahili kwa Kiingereza katika mafundisho ya shule za upili katika wilaya ya Bungoma. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa lugha ya Kiswahili imeanza kuchukua nafasi kama lugha ya kufundishia katika shule za mashambani na pia ni lugha ambayo inatumiwa kwa mapana zaidi. Ingawa utafiti huo ulijikita katika shule za sekondari, kulikuwa na kushabihiana

kukubwa na utafiti huu, kwa vile tulichunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji katika mandhari ya shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye.

Bunyi (1986) alifanya utafiti wake katika eneo la Dagoretti, Nairobi. Alitaka kuchunguza matumizi ya lugha darasani kwa kuzingatia lugha za Kiswahili, Kiingereza na Kikikuyu. Haja yake kubwa ilikuwa ni kutathmini kama sera ya serikali kuhusu lugha ilikuwa inatekelezwa. Aligundua na kuripoti katika kazi yake kuwa sera ya lugha katika darasa la nne ambapo ufundishaji wa lugha za kikabila hukomea haikuwa inatekelezwa. Utafiti wa Bunyi ulizingatia lugha zote tatu; Kiswahili, Kiingereza na Kikikuyu. Pia ulitubainishia kuwa sera rasmi ya lugha haikuzingatiwa. Utafiti huu unachunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia namna lugha ya Kiswahili inavyotumika, watumiaji wake, sababu za matumizi na changamoto inayokumba matumizi yake katika shule za chekechea.

Merrit (1987) anaonyesha kuwa watoto huelewa dhana bayana wanapofunzwa katika lugha ya maeneo kwa vile ina ukwasi wa msamiati. Maoni haya yanaweza kuaminika, kwa vile lugha wanayoweza kujieleza sawa sawa katika mazingira ya nyumbani na katika shule, ni ile lugha sambazi. Kiswahili ndiyo lugha inayofaa katika mafundisho hasa katika maeneo ya miji ambapo hutumika kama lugha ya kwanza. Ufaafu wa lugha ya maeneo, unaungwa mkono na Classen na Stephen katika Ayoti (1994) walipodokeza kuwa lugha ya Kiswahili inaeleweka na asilimia sitini ya watoto wenye asili ya kibantu. Hata wale ambao si wabantu, lugha hii hueleweka

kwa vile ni lugha ya maeneo wanakoishi. Meerkotter (2002) anashadidia hoja hii kwa kusema kuwa:

> Kiswahili ndiyo lugha inayotumika kwa upana zaidi ya yoyote barani Afrika hasa tukizingatia idadi ya wale wanayoisema lugha hii. Inakisiwa kuwa zaidi ya watu milioni mia moja huzungumza lugha hii barani Afrika (uk4).

Mchango alioutoa Meerkotter (2002) ni muhimu katika utafiti huu, kwa vile anatuthibitishia umuhimu wa lugha ya Kiswahili, iliyo na sifa za matumizi mapana na inayofaa kutumiwa kama chombo cha mafundisho katika shule za chekechea.

Adedeji (1982) katika mapendekezo yake ya matumizi ya lugha ya Kiyoruba, alisema kuwa matumizi ya lugha bora ni lazima yaanzie kwenye viwango vya chini vya shule ya malezi, ambapo watoto wanahitaji kupewa mazoezi katika stadi ya kusikiliza na kuzungumza. Ingawa hakulenga lugha ya Kiswahili, mchango alioutoa ulikuwa na mantiki kwa vile Kiswahili ndiyo lugha ya matumizi mapana ambayo inaweza kukuzwa kimatumizi kuanzia shule za chekechea. Watoto wengi katika shule za chekechea huwa na umri wa chini ya miaka sita, ambapo wanasaikolojia huamini kuwa akili hushika mambo kwa haraka. Hivyo wapewapo msingi bora katika lugha huwa ni wa kudumu. Licha ya lugha ya Kiswahili kupendekezwa kutumiwa, inakumbwa na ushindani si haba. Matokeo ya utafiti uliofanywa na Rubagunya (1994) ulionyesha kuwa Kiswahili hakiwezi kutegemewa kama lugha ya mafunzo. Kauli sawa na hii ilitolewa na Barasa (1997), aliposema kuwa lugha ya Kiswahili haijakuzwa kutosheleza mahitaji katika mtaala wa elimu.

Maoni sawa na haya yalipingwa na Simala (2006), alipotoa kauli kuwa lugha ya Kiswahili ina utajiri wa msamiati kufundishia masomo hata ya sayansi, ambayo inaaminika imepungukiwa na msamiati faafu katika lugha ya Kiswahili. Makala ya Lang'at (1997) yanashughulikia masuala mazito ya lugha ya Kiswahili yanayojibiwa vyema na Simala, anayetetea matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nyanja zote. Kwa mujibu wa utafiti huu, lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha zinazojitosheleza kimsamiati kufundishia shule za chekechea. Wazo la Simala (2006) ni muhimu katika utafiti huu kwa vile lugha ya Kiswahili ndilo chaguo bora katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea.

Akishadidia umuhimu wa lugha ya maeneo, Broughton (1980) anatoa kauli kuwa lugha inayofaa kufundishia wanafunzi wa madarasa ya chini ni ile lugha ya maeneo. Lugha hii huwasaidia wanafunzi katika kujenga moyo wa kujiamini, kuelewa upesi, kufikiri kwa haraka na kujieleza kwa urahisi. Umuhimu ambao umepewa lugha ya maeneo ndiyo kivutio kikubwa kwa utafiti huu. Lugha ya Kiswahili ni lugha ya maeneo ya utafiti, sifa hii ilitupelekea kuchunguza matumizi yake katika shule za chekechea. Kwa kufanya hivi, wanafunzi hukuza stadi zao za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Kwa upande mwingine, mielekeo ya lugha huchangia pakubwa matumizi ya lugha katika jamii.

Kembo-Sure (1994) katika utafiti wake wa kuchunguza mielekeo ya lugha, matumizi na umilisi, aligundua kuwa asilimia 83.9 ya wanafunzi wa sekondari nchini Kenya walikuwa na mwelekeo chanya kuhusiana na lugha ya Kiswahili.

Mabadiliko haya, yanatokana na hadhi ambayo imetunukiwa Kiswahili kama lugha ya Kitaifa. Anaendelea kusema kuwa, Kiswahili ni lugha inayoeleweka vyema miongoni mwa wanafunzi na pia ilipandishwa daraja kwa kufanywa somo la lazima katika shule za msingi na sekondari. Sababu hizi ndizo zimechangia lugha hii kukubalika miongoni mwa wanafunzi katika shule za nchi hii. Kembo-Sure anaonyesha kuwa lugha ya Kiswahili imeanza kupata hadhi katika asasi za elimu. Kwa sababu shule za chekechea ndio msingi wa elimu kwa msomi, mtafiti alionelea ni vyema kuchunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Kembo-Sure na wenzake (1994), lugha ya Kiswahili ina sifa za kipekee za kupitisha na kuwasilisha maarifa kwa hadhira kubwa zaidi nchini. Waligundua kuwa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania kinyume na ilivyo Kenya, imefanikisha malengo ya elimu ya msingi. Yaliyosemwa na wataalamu hawa yalikuwa ni changamoto kwa taifa la Kenya. Hata hivyo, walirejelea lugha ya Kiswahili kwa jumla, utafiti huu ulichunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea.

Ingawa Kennedy (1989) anarejelea matumizi ya lugha ya Kiingereza, bali kauli anazozitoa zinaoana na sababu za matumizi ya Kiswahili katika shule za chekechea, kwa vile anadai kwamba lugha inayofaa kufundishia ni ile ambayo inakubalika na watumiaji wengi katika jamii. Haya yanaungwa mkono na Msanjila (2005) alipotoa kauli kuwa nchini Tanzania, Kiswahili hutumiwa kufundishia katika viwango vya chekechea hadi vyuo vya walimu. Hoja walizotoa wataalamu hawa zilikuwa muhimu kwa utafiti huu, kwani maoni ya

Msanjila ni ishara tosha kuwa Kiswahili hutumika kufundishia katika nchi hiyo. Nafasi ya Kiswahili ambayo haijabainika katika shule za chekechea ndiyo iliyonipelekea kuingiwa na shauku ya kutaka kujua matumizi yake katika Manispaa ya Webuye.

Akipigia upatu umuhimu wa lugha ya Kiswahili, Mukuria (1995) ana wazo kuwa wasimamizi na watekelezaji wa mitaala zama za wakoloni walishikilia dhana kuwa mtoto huelewa dhana vyema, iwapo anafundishwa katika lugha ya mama. Mawazo sawa na haya yanaendelezwa na Nyaga (1994) alipotoa kauli kuwa kipengele cha elimu kinaweza kupewa hadhi zaidi, iwapo lugha kama vile Kiswahili itatumiwa kufundishia.

Utafiti uliofanywa na Mohammed (1975) kuhusu sera ya lugha nchini Tanzania ulikuwa muhimu kwa utafiti huu, kwa vile alijishughulisha na sera za lugha nchini Tanzania, tangu ukoloni hadi baada ya kupata uhuru. Utafiti wake hasa ulikuwa juu ya uwezekano wa kukifanya Kiswahili kiwe chombo cha kufunzia masomo mengine katika shule za upili katika nchi ya Tanzania. Ameonyesha bayana namna Kiswahili kilivyofaulu kutumika kufundishia katika shule za msingi na vyuo vya elimu ya taifa, na hivyo kuhisi kuwa kukifanya Kiswahili chombo cha kufundishia masomo mengine katika shule ya upili kungeinua viwango vya umilisi na utendaji wa wanafunzi kwa jumla.

Ufaafu wa lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji unafafanuliwa na Kembo-Sure (1991) alipodahili kuwa, watoto nchini Kenya hujifunza Kiingereza kwa sababu za kijamii na kiuchumi zilizohusishwa nacho. Alikisia

kuwa asilimia sitini na tano ya Wakenya walikijua Kiswahili ikilinganishwa na asilimia tano ya waliokifahamu Kiingereza. Matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha umaarufu wa lugha ya Kiswahili na hivyo kuwa na manufaa kwa utafiti wetu. Kembo-Sure aliwahusisha wanafunzi pekee katika sampuli, lakini sisi tuliwajumuisha wasimamizi, walimu, wanafunzi na wazazi wa shule za chekechea.

Obanya (1999) akizungumzia kuhusu umuhimu wa lugha za Kiafrika, anaeleza kuwa, kupata kizazi kitakacholeta mabadiliko katika lugha ya Kiafrika, ni sharti tuanzie shule za chekechea. Mchango wake ulifaa utafiti huu kwa vile Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kiafrika zinazostahili kuwekewa msingi bora ambao huanza katika shule za chekechea. Licha ya mapendekezo yake kuwa mazuri, ni vigumu kuafikiwa katika shule za chekechea, kwa vile watoto wa kiwango hiki mara nyingi huiga wasemavyo wakubwa wao, kumaanisha kuwa wanaweza kuiga Kiswahili kibovu au kizuri.

## 2.5 Watumiaji wa Kiswahili Katika Shule za Chekechea

Matumizi ya lugha ndicho kitovu cha ufunzaji na ujifunzaji katika asasi iwayo yoyote. Kouma (1984) anawalenga walimu wa Kiingereza kwa kuchangia kuwa, utumiaji wa lugha kwa njia inayostahili huanza na mwalimu mwenyewe. Ipara (2001) akisistiza umuhimu wa umilisi wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wale wanaotagusana na watoto wadogo wa shule za chekechea, kwa madhumuni ya kujenga kizazi kitakachoionea fahari lugha yao. Kumaanisha kuwa, uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha kwa njia nzuri unaweza kutokana na jinsi mwalimu anavyomilisi lugha.

Kwa upande mwingine, mtafiti aweza kusema utumiaji wa lugha kwa njia mbovu huwa na athari hasi kwa mtoto wa chekechea. Licha ya maoni ya Kouma (1984) na Ipara (2001) kuwa na mantiki, watumiaji wa lugha ya Kiswahili huathiriwa pakubwa na lugha zilizopo kwenye mazingira ambazo hutumiwa kutegemea umri, uana na kiwango cha elimu. Kazi za wawili hawa, zilitupelekea kuchunguza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mandhari ya chekechea katika miktadha ya ufunzaji na ujifunzaji.

Kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili, Munyua (2002) ana mtazamo kuwa walimu wanahitajika kushughulikia swala la lugha kwa uangalifu, kwa vile kuna haja kwa watumiaji kutambua na kusisitiza usanifu wa lugha ya Kiswahili. Hili linatokana na Kiswahili kibovu kusikika miongoni mwa watu wazima na hata watoto wadogo. Mchango wa Munyua ni muhimu kwa utafiti wetu, kwa vile nafasi ya mwalimu ni nguzo muhimu ya utafiti huu, ambaye anapaswa kuandaa mazingira ya matumizi ya lugha ya Kiswahili wakati wa ufunzaji na ujifunzaji.

Mazingira yanayomzunguka mtoto huathiri matumizi ya lugha kwa njia hasi au chanya. Mbaabu (1996) anadhibitisha kuwa wengi wa wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza hawapati shida ya kutumia Kiswahili, kwa sababu tayari walikwisha isikia lugha na kuitumia katika mawasiliano wakiwa nyumbani na katika shule za chekechea. Maoni sawa na haya yametolewa na Filmore (2000) alipodahili kuwa, watoto hufurahia kutumia lugha ambayo inazungumzwa na jamii yao na iwapo watashurutishwa kutumia lugha ngeni basi mawasiliano hukatizwa. Hivyo anapendekeza kuwa watoto wanapaswa

kuzungumza, kusoma katika lugha yao ya maeneo itakayowawezesha kupata tajriba ya kujifunza na kisha kuitumia lugha ya pili. Waandishi hawa, walionyesha umuhimu wa wanafunzi kuwa na umilisi wa lugha ya mazingira. Kwa mujibu wa utafiti huu, tuliwezeshwa kuchunguza iwapo walimu na wanafunzi wa chekechea huitumia lugha ya Kiswahili. Tumzuiapo mtoto kutumia lugha yake hudidimiza kipawa cha ubunifu na ukuaji wa akili.

Watumiaji wa lugha katika mandhari ya chekechea wanapaswa kuitumia katika miktadha halisi. Wakishadidia hoja hii, Ruthfalman na wenzake (1985) walidokeza kuwa watumiaji wa lugha katika shule za chekechea sharti waitumie katika miktadha yenye maana. Mfano mwalimu anaweza kusema 'vua viatu' au 'leta kidude chako cha chakula' Matumizi ya lugha katika shule za chekechea, hutegemea pakubwa mazingara ya kijamii yanayomzunguka mtoto. Ruthfalman na wenzake (1985) wanatoa mchango kuwa matumizi ya lugha yanaweza kuchochewa kupitia vitu halisi. Mtoto aulizwapo apewe maziwa, kisha babake akamletea glasi ya maziwa, tendo hilo humpa msukumo wa kutumia maneno ili apate anachodhamiria. Ingawa ni kweli kuwa watumiaji wa Kiswahili katika shule za chekechea wanastahili kuitumia katika miktadha yenye maana, mitagusano huru baina ya wanafunzi huendeleza lugha ya Kiswahili kwa vile huwa hawajadhibitiwa na walimu wao. Bagunywa (1980:50) anatilia nguvu hoja hiyo kwa kusema kuwa:

> Mambo muhimu katika jamii hupitishwa kwa mtoto kutumia lugha ya jamii yake. Mtoto hujifunza utamaduni na mambo yote yanayodhaminiwa na jamii yake. Watu wanapodai kuwa lugha fulani ni yao, huashiria jinsi inavyotumiwa kuelezea utamaduni wao, mazingira na maisha yao. Hali hii hutambulisha jamii, eneo na taifa.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili huchochea uwezo wa mwanafunzi wa kumaizi mambo na hamu ya mtoto ya kujieleza kwa urahisi kinyume na haya, mwanafunzi hulazimika kusema mambo machache, au kutosema chochote kabisa. Kutokana na hali hii, fikra za mwanafunzi haziwezi kutanuka kumaanisha kuwa ufaraguzi wa kubuni misamiati hukwama na hivyo hukosa kukua.

Ngugi (1987) akisisitiza umuhimu wa lugha ya maeneo katika mafundisho, alieleza kuwa walitambiwa hadithi katika lugha mama na ilikuwa rahisi kwao kurudia hadithi ile ile wakati wa mchana kwa mahirimu wao kondeni. Aliendelea kufafanua kuwa mazingira ya nyumbani na kondeni yalikuwa kama shule za chekechea, kwa vile hakukuwa na shule rasmi ya kiwango hicho. Kilicho muhimu kama anavyosema Ngugi, ni kutumia lugha moja ya mawasiliano inayoeleweka kwa wote kupitia utambaji wa hadithi, vitendawili na methali.

Maoni ya Ngugi (1987) yalikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwa vile yalitudhihirishia umuhimu wa kutumia lugha ya Kiswahili kufundishia shule za chekechea. Tuliweza kufahamu dosari inayoweza kujiri iwapo watoto watanyimwa uhuru wa kujieleza katika lugha eneo wanapokuwa shuleni. Chimerah na Nabea (1997) wakituthibitishia umuhimu wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wake, wanadahili kuwa:

> … Hakuna yeyote anayeweza kujiendeleza kufikia ufanisi kwa kutumia lugha asiyoweza kuimudu kikamilifu.Watu huweza tu kuyaeleza na kuyafafanua mambo ya msingi katika utamaduni wao kwa kutumia lugha ambayo aghalabu huwa ni lugha yao ya kiasili…

Ili ufunzaji na ujifunzaji uendelee katika shule za chekechea, walimu na wanafunzi wanahitaji kutagusana na kuwasiliana katika lugha inayoeleweka. Lugha ya Kiswahili ni chaguo bora kwa vile katika sehemu za miji ni lugha mama. Hoja sawa na hii imetolewa na Kembo (2000) anaposema kuwa hakuna elimu inayoweza kupatikana iwapo lugha inayotumiwa haieleweki. Mtafiti anadahili kuwa ukuaji wa lugha yoyote ile hutegemea matumizi ya kila siku ya lugha ya lugha lengwa. Ni dhahiri kuwa kutoimarika kwa lugha za Kiafrika kunatokana na mifumo na sera mbovu za lugha katika jamii. Hivyo, ikiwa lugha ya Kiswahili itapewa msingi unaofaa na watumiaji wake, bila shaka ufaafu wake utakita mizizi.

Walimu hutumia mseto wa Kiingereza na Kiswahili wanapoendeleza ufunzaji na ujifunzaji darasani, huku wakinakili mambo muhimu katika madaftari kwa lugha ya Kiingereza, (Obura, 1990). Haya yametokana na mwalimu kuwa na ufasaha katika lugha ya Kiswahili huku akitumia msamiati wa Kiingereza uliopo vitabuni kunakili. Uvumbuzi huu unatupelekea kuamini kuwa ni rahisi kujieleza kwa lugha mama ambayo ni Kiswahili kwa wakazi wa Manispaa ya mji wa Webuye. Mawazo haya pia yanaonyesha kuwa tatizo la kuchanganya msimbo ni sugu katika muktadha wa ufunzaji na ujifunzaji katika mazingira ya asasi za elimu.

Athari ya mazingira imefafanuliwa na Chimerah (1988) anapotudokezea kuwa, mtoto anapokuwa kwenye kundi linalozungumza lugha ya Kiswahili huzoea lugha hiyo. Hivyo kukuza stadi ya kuzungumza ambayo huboreshwa ikiwa mwalimu atawaongoza wanafunzi katika mazoezi ya mazungumzo

kupitia michezo ya kuigiza na kukariri ushairi, nayo stadi ya kuandika yaweza kukuzwa kwa mazoezi zaidi ya kuandika. Kwa upande mwingine, Williams (1992) anapozungumzia umuhimu wa athari ya wazazi kwa watumiaji wa lugha, anataja kuwa watoto hujifunza kutoka kwa wazazi na katika jamii alikozaliwa mzungumzaji. Kwa mujibu wa utafiti huu, nafasi ya mazingira ni muhimu mno kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea.

Bowers (1968) anatoa vigezo vitatu kwa wazungumzaji wa lugha. Ingawa alizungumzia moja kwa moja lugha ya Kiingereza, alitaja matumizi ya abjadi, sarufi, msamiati na nyenzo za kufundishia kama vile machapisho na vifaa vingine. Vigezo hivi vilifaa utafiti huu kwa vile uliwatarajia watumiaji wa lugha ya Kiswahili watilie maanani nyenzo wakati wa ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea

## 2.6 Changamoto za Kiswahili Katika Shule za Chekechea

Lugha ya Kiswahili ina sifa za lingua-franca kwa vile inaweza kutumiwa kufundishia masomo mengine kwenye mtaala. Hata hivyo inakumbwa na changamoto chungu nzima.

Chieni (2001) anadahili kuwa katika shule za mjini, kuna sheria isiyo rasmi ambayo hairuhusu Kiswahili kuzungumzwa wala kufundishiwa, katika miktadha mingine adhabu hutolewa. Anaendeleza mjadala wake kwa kusema kuwa, matumizi ya lugha ya Kiingereza kufundishia shule za chekechea za mijini inaungwa na washika dau wa shule hizi. King'ei (1997) anachangia kuwa, msisitizo wa lugha ya Kiingereza umezuia wanafunzi kupata fursa ya

kutumia misamiati mipya katika lugha ya Kiswahili. Haya husababisha kuzorota kwa usanifu wa lugha ya Kiswahili. Kutokana na mchango wa King'ei (1997) na Chieni (2001), tunapata ufahamu kuwa lugha ya Kiswahili inapata ushindani mkubwa kutoka kwa lugha zingine za mafundisho. Pasipo kuweka mikakati imara ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika msingi wa kiakademia ambayo ni shule za chekechea, lugha hii itakosa udhamana wake kama lugha ya taifa.

Ipara (2001) anachangia kuwa Kiswahili kimetumiwa kwa ufanisi katika madarasa ya chini ya shule za msingi. Wengi wameyakubali haya shingo upande na wanapinga matumizi yake katika kiwango zaidi ya hiki. Uhuru wa matumizi ya lugha ya kufundishia umetokana na uwezo walio nao washika dau wa kuamua lugha ya mafundisho. Baadhi ya shule za chekechea hutumia lugha sambazi ambayo ni Kiswahili, ilhali wengine hutumia mseto wa Kiingereza na Kiswahili. Hata hivyo, Kiswahili kikitumika katika mafunzo, huweza kuweka msingi bora wa lugha hii kukua kwa vile Kiswahili kwa baadhi ya watoto wa chekechea ni lugha mama. Ufaafu wa lugha ya Kiswahili unapendekezwa na Ngugi (1987) waliposema kuwa chombo cha kufundishia au mawasiliano iwe lugha inayofahamika na mwanafunzi. Katika muktadha huu, lugha iliyo na sifa zinazofaa maelezo haya ni lugha ya Kiswahili, kwa vile ni lugha ya matumizi mapana.

Ingawa wapenzi wa lugha ya Kiswahili hupendekeza matumizi yake, kuna changamoto zinazoikabili kama vile mazingira yanayopendelea lugha ya Kiingereza. Mbaabu (1991) anatudokezea kuwa, watu huamini kwamba

hakuna haja ya kutumia Kiswahili kufundishia watoto kwa vile tayari wanaifahamu. Mawazo sawa na hayo yanajitokeza kupitia kwa utafiti wa Barasa (1997) alipotoa kauli kuwa, Kiswahili kimepata hadhi katika nyanja za elimu, kimepungukiwa na hivyo si toshelevu kama lugha ya kufundishia. Maoni yaliyotolewa na Barasa (1997) yanawakilisha mielekeo ya wale wadunishao Kiswahili. Tuhuma kwamba hakina msamiati toshelevu, ni lugha ya maskini na ni ngumu kutumika katika miktadha rasmi si sahihi na hayawezi. Mawazo sawa na haya ni hatari kwa vile kitovu cha lugha ya Kiswahili ni pwani mwa Kenya. Hata hivyo, mchango alioutoa Kihore (1983: 54) ulifaa utafiti huu kwa vile anasema hivi:

> Kutumia lugha ngeni hasa katika shule za msingi kunaweza kuathiri vibaya ukuaji wa akili za mwanafunzi. Hamu ya mtoto kujieleza mwenyewe huwa inatatizwa. Hata iwapo anaweza kuongea Kiingereza, hawezi kusimulia tajriba zake kwa urahisi. Kutokana na hali hii, fikra za mtoto haziwezi kutanuka; Ufaraguzi hukwama, huwa na uhakika duni na hisia zake husalia kuwa butu.

Maelezo haya yanaenda sambamba na mawazo ya Simala (2006) kuwa lugha ya Kiswahili ina utajiri wa msamiati. Kwani kuna visawe vingi vinavyorejelea nomino moja. Athari ya mazingira kwa lugha ya mtoto ni muhimu (Child, 1973). Katika utafiti alioufanya, ijapo hakulenga lugha ya Kiswahili moja kwa moja, bali alizungumzia kuhusu mazingira ya kiisimu anayokulia mtoto ambayo huchangia pakubwa kukua kwa lugha yake. Anaendelea kudahili kuwa lugha ambayo imebeuliwa katika jamii inayomzunguka mtoto haidhaminiwi. Haya yalidhihirika kupitia kiongozi cha uchunzaji kilichoibua ukweli kwamba nyenzo zilizoambatanishwa na maandishi katika lugha ya Kiswahili zilikuwa chache mno, badala yake nyingi

zilikuwa katika lugha ya Kiingereza. Walimu walipoulizwa sababu, walisema kuwa kutayarisha nyenzo katika lugha ya Kiswahili ni tata mno.

Bamgbose (1991) anataja vizuizi viwili dhidi ya matumizi ya lugha katika shule za chekechea, mathalani serikali kutojihusisha moja kwa moja katika maswala ya shule za chekechea, kwa vile ni mali ya watu binafsi, mashirika na washika dau wakiwemo wazazi. Washika dau kuamua lugha inayopaswa kufundishiwa watoto wa chekechea. Vikwazo vivi hivi ndivyo vinavyoathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya, kwa vile wazazi wa shule za chekechea za mijini hujishughulisha na masuala muhimu, mojawapo likiwa ni lugha ya kufundishia. Baadhi ya wazazi hupendekeza lugha ya Kiingereza kutumika katika mafundisho.

Ingawa kumekuwa na mijadala mingi kutoka nchi za nje na hata wataalamu wa humu nchini kuhusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika asasi za elimu, sheria za Kenya hazina kifungu chochote kinachopendekeza wala kuzungumzia kwa uwazi umuhimu wa kutumia lugha za Kienyeji katika mafundisho. Chumbow (2003) akishadidia umuhimu wa lugha ya mazingira, anataja kuwa hurahisisha uelewa wa watoto wakati wa ufunzaji na ujifunzaji. Mtafiti anakubaliana na maoni ya Chumbow kwa vile matumizi ya msimbo usioeleweka na wanafunzi huwa kizingiti kwa mafundisho darasani, hivyo lugha ya Kiswahili ikitumika katika mafundisho huchochea uelewa.

## 2.7 Tafiti za Hivi Karibuni Kuhusu Mada ya Utafiti

Sehemu hii inaangazia matokeo ya baadhi ya tafiti kuhusiana na lugha ya Kiswahili katika viwango mbalimbali vya elimu. Tafiti nyingi zimeangazia matumizi ya lugha katika elimu. Mojawapo ya tafiti hizi ni ule wa Cleghorn (1987) aliyechunguza matumizi ya lugha katika ufunzaji wa sayansi katika shule za msingi nchini Kenya. Katika utafiti huo, alinuia kuchunguza hulka za walimu wa darasa la saba wakati wanapotumia lugha ya Kiingereza kufafanua dhana za kisayansi. Ingawa utafiti wa Cleghorn (1987) ulifanywa katika shule za msingi, unafaa utafiti huu kwa vile shule za msingi ndiko kunakoendelezwa msingi wa chekechea.

Hivyo kuna uwezekano kwamba matokeo ya utafiti huo yaliashiria yale yafanyikanayo katika shule za chekechea. Ingawa utafiti wa Cleghorn ulishughulikia lugha ya Kiingereza, matokeo yalidhihirisha kuwa walimu walishuhudia ugumu katika kufafanua dhana katika lugha ya Kiingereza. Mtafiti alipata mshawasha wa kutaka kujua hali ya matumizi ya Kiswahili baina ya walimu na wanafunzi katika shule za chekechea. Tofauti iliyopo ni ya kimazingira, kwani utafiti huu ulifanywa katika Manispaa ya mji wa Webuye katika Wilaya ya Bungoma Mashariki ilhali ule Cleghorn ulijikita katika shule za msingi.

Merrit (1987) alitafitia lugha ya mafundisho na mafundisho ya lugha katika baadhi ya shule za msingi nchini. Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kutoa maelezo ya kichanganuzi kuhusu matumizi ya lugha katika shule. Matokeo ya utafiti huo yaliashiria kuwa, walimu walishindwa kutoa maelezo kwa kutumia

msimbo mmoja. Badala yake hawakuzingatia kaida rasmi za sera ya lugha ya kitaifa kwa kutumia lugha zaidi ya moja katika muktadha mmoja. Utafiti huo unashabiana na huu kwa vile mtafiti alijikita katika shule za msingi, huku huu ukilenga shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye Wilayani Bungoma Mashariki.

Omulando (2002) akitafitia athari ya lugha ya Kiswahili, kwa matumizi ya lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari Wilayani Bungoma nchini Kenya. Alitufichulia kuwa, lugha ya Kiswahili ilitumika kwa mapana katika mitagusano kwenye mandhari nje ya darasa. Japo utafiti wa Omulando ulijikita katika shule za sekondari, bali vigezo vinavyorejelewa vinaoana na utafiti huu, kwa kuwa alishughulikia nafasi ambayo Kiswahili kinaathiri Kiingereza huku mtafiti akishughulikia matumizi ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea.

Chakava (1996) akizungumzia umuhimu wa lugha sambazi, anataja kuwa iwapo machapisho au vitabu vitaandikwa katika lugha eneo au lugha inayoeleweka na msomi, bila shaka machapisho hayo yatakuwa kivutio kikubwa katika asasi za elimu. Kiswahili ni lugha ambayo inazungumzwa kwa mapana katika eneo la utafiti, hivyo iwapo machapisho mengi katika shule za chekechea yataandikwa katika lugha ya Kiswahili, yatasomwa na wengi.

## 2.8 Hitimisho

Kwa kuhitimisha, tafiti zilizo na mshabaha na utafiti huu zilikuwa muhimu kwa vile kila utafiti ulizalisha matokeo tofauti, sababu mojawapo ni kuwa data zilikusanywa katika maeneo na asasi mbalimbali za kielimu (McDonough, 1995). Katika kutamatisha, kwa mujibu wa utafiti huu na mapitio ya maandishi, kulikuwa na sababu tosha ya utafiti huu kutekelezwa. Sura inayofuatia ya tatu inasheheni njia na mbinu za utafiti.

## SURA YA TATU

## 3.0 NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia njia na mbinu ambazo zilitumika na kufanikisha madhumuni ya utafiti, muundo wa utafiti, eneo la utafiti, watafitiwa, kiunzi cha sampuli, vifaa na utaratibu wa ukusanyaji data na utekelezaji wa majukumu. Uthabiti na uaminifu wa nyenzo za utafiti, majaribio ya utafiti na matatizo yalomkabili mtafiti wakati wa kukusanya data vilevile yameshughulikiwa. Tarakimu zilizotumiwa katika uchanganuzi wa data pia zimeshughulikiwa. Data iliyokusanywa, ililenga kuthibitisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea za Manispaa ya Webuye.

### 3.2 Mpangilio wa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa kutumia muundo wa usoroveya elezi, ambao ulihusisha kuchunguza matumizi ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye. Kerlinger (1995) akieleza kuhusu utafiti wa aina hii, anatudokezea kuwa muundo huu hunuia kuelezea hali ilivyo katika mfumo wa kijamii kama vile asasi za elimu.

Mtafiti alitumia usoroveya elezi, kwa sababu ulimuwezesha kukusanya data haraka, kuelewa Mandhari katika eneo la utafiti na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea. Prasad na Reddy (1983) wakichangia kuhusu muundo elezi, wanataja kwamba muundo wa namna hii una uwezo wa kufafanua hali ilivyo, wakati huo kuhusu watu, vitu, matukio na hata mwelekeo wa watu. Prasad na Reddy (1983) wanasistiza kuwa muundo wa

aina hii unafaa, kwa vile unaweza kubainisha na kubashiri sifa za vipengele muhimu katika utafiti. Kwa kutumia muundo huu, mtafiti aliwezeshwa kuelewa undani wa vipengele muhimu vya lugha ya Kiswahili na namna vinavyoathiri matumizi yake katika mafunzo ya shule za chekechea. Oppenheim (1992) akimnukuu Good (1972) anasema kwamba ni vigumu kupata data kutoka kwa watafitiwa ambao hawaelewi mada. Ili kujiepusha na hali hii, mtafiti alitumia vifaa vingi ilikukusanya data kuhusu jambo moja kwa lengo la kujaliza mapengo ambayo yangeleta udhaifu kwenye data iliyokusanywa.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Manispaa ya Webuye kwa sababu inajumulisha watu mseto ambao lugha yao ya mawasiliano ni Kiswahili. Manispaa ya webuye ina mseto wa shule za chekechea za kibinafsi na umma. Aina hizi za shule ni bora kwa vile hutoa uwakilishi unaofaa, Best na kahn (2003).

Wilaya ya Bungoma Mashariki imeegemea kwenye latitudo $25.3^{o.}$ Kaskazini na 53.3’ Kusini longitudo $34^{o}$ 31.4’ Mashariki, 35 $^{o}$04’ Magharibi (Taz. kiambatishi vi). Wilaya hii imegawanywa katika taarafa nne ambazo ni Ndivisi, Bokoli, Webuye na Milo. Eneo la utafiti linapatikana katika taraafa ya Webuye. Manispaa ya Webuye ina jumla ya mseto wa shule 62 za chekechea za Umma na Kibnafsi; nyingi Yazo zikiwa za Kibinafsi. Eneo la Manispaa ya Webuye inawakilishwa katika ramani ya uk.121

Mtafiti alichagua Manispaa ya Webuye kwa sababu kadhaa, Kwanza, eneo la mtafiti linafahamika vyema kwa mtafiti. Ufahamu wa eneo unaungwa mkono

na Tuckman (1978) anapodai kuwa wakati mwingine, uzoefu wa eneo la utafiti humpa mtafiti kibali miongoni mwa wakazi wa eneo husika. Wazo hili linatiliwa nguvu na Singleton (1993) anapochangia kuwa, eneo linalofaa kwa utafiti ni lile linalofikiliwa kwa urahisi na mtafiti na linaloweza kukubali mwingiliano kati ya mtafiti na wahojiwa. Vilevile Singleton anatoa kauli kuwa, katika eneo ambalo mtafiti hakaribishwi, basi utafiti hauwezi kufanikiwa. Hivyo ufahamu wa eneo la utafiti ulituwezesha kuendelea na utafiti katika shule za chekechea za Manispaa ya Webuye.

Mtafiti alichagua sehemu hii, kwa vile eneo hili lina mchanganyiko wa makabila mbalimbali na matokeo ya utafiti yangefaa maeneo mengine ambayo yana sifa kama za eneo la utafiti. Kwa upande mwingine, tafiti nyingi maktabani zilidhihirisha kuwa hapana yeyote aliyeshughulikia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mafunzo ya chekechea, bali nyingi zimejikita katika vipengee kama vile mtaala, mwelekeo wa walimu kuhusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa tafiti zilizopo.

### 3.4 Watafitiwa

Watafitiwa ni walimu wa shule za chekechea za Manispaa ya Webuye, wasimamizi wa shule za chekechea, wazazi pamoja na wanafunzi wa kitengo cha mwisho cha chekechea. Maoni yaliyotolewa na Sedlack na Stanley (1992) yalidhihirisha kuwa ni sharti watafitiwa waeleweke kimalengo na kimazingira. Kutokana na kumbukumbu katika afisi ya mkuu wa elimu, Manispaa hii ina jumla ya shule zikiwemo za kibinafsi na za umma. Orodha ya shule zilizohusishwa katika utafiti huu inapatikana katika uk. 123. Mtafiti

aliamua kuwatumia wasimamizi wa shule kwa sababu wao ni miongoni mwa washika dau walio na uwezo wa kutekeleza sera ya lugha.

Walimu wa chekechea walikuwa nguzo muhimu katika utafiti huu kwa vile wao ndio walio na mitagusano ya karibu na wanafunzi. Pia huwa na athari hasi au chanya, kupitia mielekeo yao kuhusiana na lugha ya Kiswahili na namna wanavyoitumia. Wazazi walikuwa miongoni mwa watafitiwa kwa vile huathiri matumizi ya lugha katika miktadha ya kufundishia watoto katika shule za chekechea. Wanafunzi walitupa picha halisi nyanjani iliyotuwezesha kufahamu matumizi ya Kiswahili katika shule za Manispaa hii, kwa vile katika asasi iwayo yoyote, huwa na nafasi ya kati kwa masuala ya lugha. Kwa hivyo habari zilizotolewa nyanjani zilimsaidia mtafiti kukadiria matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mafunzo ya shule za chekechea.

### 3.5 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli ni uchaguzi wa sehemu fulani ya watu au kitu kizima. Haya ni kwa mujibu wa Dalen (1979). Anaongezea kwamba uteuzi wa sampuli ni uchaguzi wa sehemu fulani ya watu au kitu kuwakilisha watu au kitu kizima. Si rahisi kuchunguza idadi nzima ya watu inavyostahili kwani wakati na gharama ni kizingiti kikubwa. Badala yake, hulenga idadi fulani ambayo huitwa sampuli (Peil, 1995). Idadi lengwa iliyotumiwa katika utafiti huu ni walimu 19, idadi ya wasimamizi, wazazi ikiwa sambamba na ya walimu. Shule hizi ziliwakilisha 30% ya shule zinazopatikana katika Manispaa ya Webuye. Mtafiti alitumia njia mbili za kuteua sampuli kama inavyopendekezwa na Peil (1995), mbinu ya

kwanza aliyoitumia mtafiti ni mfumo sahili ilhali ya pili ni njia nasibu sahili, Mugenda na Mugenda (2003: 68) wanasema kwamba:

> Sampuli iliyoteuliwa kwa njia nasibu haina mapendeleo, kwani hakuna yeyote katika idadi ya jumla anayeweza kupata nafasi zaidi ya kuchaguliwa kuliko mwingine. (Tafsiri yangu)

Jumla ya idadi iliyolengwa, ni walimu wa chekechea wafunzao kitengo cha tatu (pre-unit) katika shule za kibinafsi na za umma. Walimu walioshirikishwa katika utafiti huu walichaguliwa kwa njia nasibu, kwa sababu katika maandalizi yao hakuna yeyote anayeandaliwa katika masomo mahususi. Shule ziligawanywa katika makundi mawili, yaliyohusisha shule za umma na kibinafsi, zilizoorodheshwa kwa kuzingatia abjadi. Kwa vile idadi ya shule za kibinafsi ni kubwa kuliko za umma, 30% kama anavyopendekeza Kothari (2003) zilizingatiwa kwa kila kundi.

Shule za kibinafsi (11) na za umma (8) zilitafitiwa. Njia hizi za sampuli ndizo zinazopendekezwa na wataalamu wengi kama vile Good, (1972), Kerlinger (1973), wanaposema kuwa ni njia za uhalisia zitumiwazo kuteua sampuli pasipo mapendeleo yoyote. Mtafiti alihitaji sampuli ya 30%, ambao ni walimu 19 wa shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye. (Taz. Jedwali 1 uk. 47)

Ili kupata idadi ya walimu na wazazi, mtafiti aliandika nambari za msimbo za kuwakilisha walimu na wazazi katika utafiti. Maandishi haya yaliandikwa kwa vijikaratasi, vilivyokunjwa na kuwekwa kwenye visanduku viwili. Baadaye mtafiti alimuuliza mwalimu mmoja wa chekechea akaokote kwa niaba ya mzazi naye mwanafunzi kwa niaba ya walimu. Vijikaratasi vilivyosalia vilihifadhiwa pale ambapo kungezuka hali ya sintofahamu miongoni mwa

walimu na wazazi walioteuliwa. Mtafiti alimsihi msimamizi wa shule, amujulishe mzazi aliyeteuliwa akakutane na mtafiti kwa mahojiano ya ana kwa ana. Mtafiti alimsihi msimamizi wa shule alichukulie jambo hilo kwa dharura ili angalau wakutane na mzazi baada ya siku mbili.

Idadi hiyo ya sampuli iliyokusudiwa ilikuwa faafu kwa vile idadi zaidi ya walimu wa chekechea kwenye utafiti ingezidisha shule, hivyo kumpa mtafiti wakati mgumu wa kuchanganua matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia; namna Kiswahili kinavyotumiwa, watumiaji wa lugha ya Kiswahili, sababu za kutumia Kiswahili, na changamoto zinazokumba matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mafundisho ya shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye. Wanafunzi wa chekechea kutoka katika shule zilizoteuliwa walishirikishwa kwa njia ya uchunzaji kwa vile mtafiti aliweza kunakili matumizi ya lugha ya Kiswahli katika miktadha ya ufunzaji na ujifunzaji. Lengo lilikuwa ni kuondoa tashwishi na uoga miongoni mwa wanafunzi wa chekechea. Mtafiti hakuwauliza wanafunzi wa chekechea maswali, bali alinakili ujumbe ambao ulikuwa faafu kwa mada ya utafiti moja kwa moja, somo lilipoendelea.

**Jedwali 1: Idadi ya Shule za Chekechea Katika Manispaa ya Webuye**

| Aina ya Shule | Sampuli | Idadi ya sampuli | % ya sampuli |
|---|---|---|---|
| Umma | 26 | 8 | 42.11 |
| Binafsi | 36 | 11 | 57.89 |
| **Jumla** | **62** | **19** | **100** |

Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti.

### 3.6 Nyenzo na Mbinu za Kukusanya Data

Kupata data kutoka kwa watafitiwa kulihitaji matumizi ya vifaa mahsusi. Vifaa vya utafiti huu vilikuwa hojaji kwa walimu, dodoso ya kuongoza mahojiano kwa wasimamizi na wazazi wa shule za chekechea na kiongozi cha uchunzaji kilichotumiwa na mtafiti mwenyewe. Vifaa hivi viliundwa kwa minajili ya kusawazisha majibu kwa vile mtafitiwa akiacha pengo kwenye sehemu fulani ya nyenzo, data ya sehemu hiyo huweza kutokea katika nyenzo nyengine. Hivyo basi matumizi ya nyenzo maridhawa huimarisha uaminifu na kuboresha mitazamo.

#### 3.6.1 Hojaji

Hojaji ni hali ya kupata data kuhusu watu, kwa kuwauliza maswali badala ya kuchunguza tabia zao. Kwa mujibu wa Oppenheim (1992), anaeleza hojaji kama mkusanyiko wa maswali ambayo yametungwa na hupewa mtu ili ayajibu kwa kuandika. Maswali haya hutungwa kwa mantiki fulani ili

kumwezesha mtafiti kupata data anayohitaji. Hojaji kwa mujibu wa Tuckman (1978) hutumiwa kuelezea maswali ambayo hutumiwa kama msingi wa kufanyia utafiti au uchunguzi fulani. Hojaji iliundwa baada ya mada ya utafiti kuchanganuliwa na kuwekwa kwenye visehemu ambavyo vimeorodheshwa kiabjadi.

Kutokana na mgawanyo huu, maswali maalum yanayolenga sehemu mbalimbali yaliandaliwa. Maswali ya aina mbili yalitungwa; wazi na funge. Maswali yaliyo wazi yalimtarajia mhojiwa kutoa maoni yake kuhusu mada iliyotafitiwa. Pia, yalinuia kutafuta maoni, mitazamo na maelezo ya watafitiwa. Kwenye maswali funge, mtafiti huelekezwa kwa namna inayomfunga pakubwa. Mtafitiwa alihitajika kuteua jawabu moja miongoni mwa majibu mbalimbali aliyopewa. Mtafiti alitumia aina hiyo ya maswali ili kupata data aliyohitaji kwa utafiti wake.

Hojaji iligawika katika sehemu tano (A – E) (Taz: Kiambatishi11) katika sehemu ya A ilikusanya habari za jumla zinazohusiana na aina za shuIe; umma na kibinafsi. Sehemu hii ya pili chini ya Kiambatishi 11 ndiyo iliyo pana mno, kwa vile ilijumuisha visehemu vinne. Sehemu ya B chini ya Kiambatishi hiki ilishughulikia namna Kiswahili kinavyotumika. Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu. Maswali haya yalidadisi kuwepo kwa matumizi ya Kiswahili, jinsi lugha hii inavyotumika ukizingatia ufasaha au uchanganyaji msimbo kupitia nyimbo, ushairi, hadithi na mitagusano.

Sehemu ya C ilijikita kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea za Manispaa ya Webuye. Sehemu hii ilikuwa na maswali matano, yaliyonuia kupata ithibati kuhusu nani wanaotumia Kiswahili, mathalani walimu au wanafunzi. Tulidhamiria kufahamu iwapo wanatumia lugha ya Kiswahili kwa wingi. Pia tulikusudia kuelewa miktadha ambamo watumiaji huzungumza lugha ya Kiswahili, vilevile mwalimu alipasa kueleza mikakati iliyowekwa ya kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea. Sehemu ya D ilimhitaji mwalimu kushughulikia sababu za matumizi ya Kiswahili katika shule za chekechea. Sehemu hii ilikuwa na kauli ambazo huenda ni sababu za matumizi ya Kiswahili katika mafunzo ya shule za chekechea. Kauli hizi zilikuwa kumi, hivyo walimu walipaswa kukubaliana na kauli hizi au kupinga. Sehemu ya E ilikuwa na kauli tisa, zilizolenga kipengele kimoja ambacho ni changamoto zinazokabili matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea. Vivyo hivyo msimamo wa watafitiwa ulidhihirika kupitia kukubali au kupinga kauli mahususi.

### 3.6.2 Dodoso

Dodoso ni maswali ambayo mtu anayeulizwa anahitajika kujibu kwa kuzungumza na wala siyo kuandika kama ilivyo hojaji, Mutai (2000). Katika muktadha huu mhoji na mhojiwa hukutana ana kwa ana. Yule anayehoji huandika majibu au hurekodi kwa kutumia kanda ya sauti au video. Njia hii ilikuwa faafu kwa vile ilileta ukuruba kati ya mtafiti na mhojiwa na hivyo kumwezesha kupata habari za kuaminika na za kina. Manufaa ya njia hii huokoa muda, ni rahisi na hakuna mapengo yanayoachwa kama ilivyo katika njia zingine za ukusanyanji data.

Mtafiti aliteua matumizi ya dodoso, kwa sababu ya manufaa mengi yanayotokana na njia hii, kama yalivyorodheshwa na Selinger na Shahomy (1989). Kwa mujibu wa utafiti huu, dodoso ilitumiwa kukusanya mitazamo ya wasimamizi na wazazi wa shule za chekechea, kuhusiana na matumizi ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea. Mtafiti alitayarisha miongozo miwili ya masaili iliyomwezesha kupata data kutoka kwa watafitiwa hawa.

Dodoso ya wasimamizi wa shule (Kiambatishi IV) ilimwezesha mtafiti kuibua data iliyotokana na maswali kuhusu; sera ya lugha na maoni yao kuhusiana na matumizi ya Kiswahili kufundishia shule hizi. Masaili kwa wazazi wa chekechea (Kiambatishi V) yalimwezesha mtafiti kukusanya data kuhusiana na mwelekeo wa wazazi dhidi ya matumizi ya lugha ya Kiswahili na mapendekezo yao.

### 3.6.3 Uchunzaji Darasani

Mtafiti pia alitumia mbinu ya uchunzaji. Uchunzaji ni mbinu ya kupata habari kwa kuhusisha tajriba au maarifa ya mtafiti bila kuuliza watafitiwa maswali yoyote. Uchunzaji huwa na manufaa katika mandhari ambapo watu hawapendi kujieleza kwa kuzungumza. Pia uchunzaji unaweza kutumiwa kuthibitisha taarifa nyengine. Haya yamefafanuliwa vyema na Nkapa (1997) anaposema kwamba:

> Uchunzaji ukishughulikiwa vizuri, huweza kuibua mambo ya ndani ambayo njia zingine haziwezi kupata. Uchunzaji unaweza kuzalisha data asili ambayo inaweza kuaminika kinyume na ilivyo hojaji' data zaidi isiyotarajiwa lakini muhimu inaweza kutokea katika mazoezi ya uchunzaji uk. 26. (Tafsiri yangu).

Udhaifu mkubwa sana wa uchunzaji katika utafiti ni kuwa, watafitiwa hubadili mienendo yao ya kawaida mara tu wagunduapo kuwa wanatazamwa. Licha ya udhaifu huu, mtafiti aliamua kutumia uchunzaji kwa sababu mbili kuu; uchunzaji ulimwezesha mtafiti kuchunguza na kupata taswira halisi kuhusu matumizi ya Kiswahili katika shule za chekechea. Uchunzaji uliweza kuziba mapengo ambayo yalikuwa yakizua shaka akilini mwa mtafiti, kwa kutoa ithibati kwa baadhi ya majibu ambayo yalitolewa katika hojaji ya walimu wa chekechea pamoja na masaili ya wasimamizi na wazazi.

Uchunzaji ulifanyika katika miktadha ya ufunzaji na ujifunzaji. Mtafiti aliweza kuona, kusikia na kisha kukadiria matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mafunzo ya shule za chekechea. Mtafiti alipata fursa ya kuchunguza nyenzo zilizokuwepo, matumizi yake na iwapo zilikuwa zimeambatanishwa maandishi katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti alinuia kuelewa lugha iliyokuwa ikitawala

mazungumzo baina ya walimu na wanafunzi, na iwapo wanafunzi waliimba, karibu ushairi, tamba hadithi na hata kutega vitendawili kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Utaratibu wa uchunzaji unapatikana katika Kiambatisho cha III. Uchunzaji uligawika katika sehemu mbili; matumizi ya lugha ya Kiswahili yakidhihirika kupitia nyimbo, ushairi, hadithi na mitagusano. Pili uchunzaji ulijikita katika kutazama nyenzo na vielelezo vilivyo na maandishi katika lugha ya Kiswahili kwenye mazingira ya shule hizi.

Kipimo cha Likert kilitumiwa kutathmini sababu zinazoaminika huchangia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea. Pia kilitumiwa kukadiria changamoto zinazokabili matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea. Ilikukadiria nguvu za mitazamo iliyoonyeshwa na walimu, tulitumia vipimo vyenye rai tano vilivyobuniwa na Likert. Rai hizi huonyesha nguvu za kukubaliana, kupinga au kutokuwa na uhakika. Maswali yote katika sehemu za D na E, kwenye hojaji iliyobeba malengo mawili ya utafiti: sababu na changamoto za matumizi ya Kiswahili katika mafunzo ya shule za chekechea. Viwango vya kukubaliana au kukataa vilihesabiwa kitakwimu, matokeo yaliyodhihirika kupitia nguvu za mitazamo, ilikuwa rahisi kwa mtafiti kufahamu kwa upana sababu na changamoto zinazopelekea matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mafunzo ya shule za chekechea.

### 3.7 Majaribio ya Vifaa Nyanjani

Majaribio ya awali ya nyenzo humwezesha mtafiti kutambua udhaifu na ubora wa nyenzo zake. Singleton (1993) anatoa kauli kuwa majaribio huwa toshelevu iwapo yatachunguza kwa yakini kile kinachokusudiwa kupimwa. Enon (2005) anadahili kuwa, majaribio ya nyenzo humwezesha mtafiti kugundua unyonge na ubora wake. Udhaifu wa vifaa unaweza kuwa kama vile msamiati usioeleweka au dosari katika utunzi wa maswali. Matatizo yaliodhihirika yalilainishwa kabla ya utafiti. Majaribio ya vifaa vya utafiti yalifanywa kwa siku kumi kabla ya utafiti halisi kuanza. Majaribio haya yalifanywa katika shule nne za chekechea katika Manispaa ya Kimilili, Wilayani Bungoma Kaskazini. Manispaa hii inapakana na ile ya eneo la utafiti. Majaribio yalifanywa katika manispaa ya kimilili kwa sababu haikuwa Manispaa lengwa.

Mtafiti alitumia mbinu ya kimakusudi kuteua shule hizo zilizojumuisha mbili za kibinafsi na zilizosalia za umma. Siku moja moja ilitengewa kila shule, huku mtafiti akimshirikisha mwalimu mmoja mmoja kwa kila shule. Wasimamizi wa shule hizi walihusishwa katika majaribio haya ya utafiti.

Walimu walimsaidia mtafiti kujaza hojaji ilihali dodoso ilijazwa na mtafiti huku akiwa na kikao cha ana kwa ana na kila msimamizi wa shule hizi. Utoshelevu na uaminifu wa vifaa kama vile hojaji, uchunzaji na dodoso ulithibitishwa kupitia kwa wataalamu wa lugha katika idara ya lugha na fasihi chuo kikuu cha Masinde Muliro. Waelekezi wa mtafiti walihusika katika shughuli hii, kwa vile walichanganua vipengele vya hojaji, utaratibu wa uchunzaji na dodoso

kisha wakatoa mapendekezo yao yaliyotumiwa kusahihisha na kuboresha vifaa vya utafiti. Lengo la majaribio haya, lilikuwa ni kujiandaa kwa ajili ya utafiti mkuu katika vipengele vifuatavyo: Kupata uzoevu katika matumizi ya vifaa vya utafiti; utaratibu wa uchunzaji, hojaji na dodoso. Kubainisha utoshelevu na utendakazi wa vifaa hivi na kupata tajriba katika ujuzi na mipangilio nyanjani. Katika majaribio haya ya utafiti, tuligundua ya kuwa Kiswahili huzungumzwa kwa mapana katika shule hizi zilizofanyiwa majaribio.

## 3.8 Utafiti Halisi

Baada ya majaribio ya vifaa nyanjani, mtafiti alivirekebisha vifaa vya utafiti, na kuvilainisha huku mianya kama vile kuwashirikisha wazazi, ilijitokeza ikishughulikiwa ili kuleta muoano wa vifaa na eneo la utafiti. Marekebisho pia yalifanywa katika hojaji ya mwalimu na dodoso kwa wasimamizi wa shule. Baadhi ya vipengele kama vile kulinganisha shule za kibinafsi na umma vilidondoshwa huku maswali yaliyoonekana mengi mno yakipunguzwa. Masaili ya wazazi yaliongezwa kwa vile wanaathari kubwa kwa lugha wanayozungumza wana wao. Mzazi mmoja mmoja aliteuliwa kwa shule zote 19.

Ukusanyaji data ulichukua muda wa miezi miwili unusu. Mtafiti alibuni mpangilio wa kuzuru shule. Kila shule ilitengewa siku moja au mbili kutegemea na ratiba yake.  Wasimamizi wa shule hizi walichukua jukumu la kuwaelezea walimu wao azma na umuhimu na jinsi msaada wao ulivyo nguzo ya utafiti huu. Wasailiwa walifahamishwa kuwa habari zitakazokusanywa zitaboreshwa na kukuza lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea. Hii ni

kwa sababu mtafiti alitaka kuwa na muda wa kutosha na jumuiya nzima ya chekechea.

### 3.9 Maadili Yaliyofuatwa Wakati wa Kukusanya Data

Mtafiti alizuru shule zilizoteuliwa na kushauriana na wasimamizi wa shule hizo. Aliwakabidhi barua kutoka kwa Wizara ya Elimu, iliyowaomba wamruhusu mtafiti azishirikishe shule zao kwenye utafiti. Wasimamizi wa shule waliweza kumjulisha mtafiti kwa walimu wa chekechea waliyoyafunza madarasa yaliyoteuliwa. Mtafiti aliwaeleza walimu kwa muhtasari lengo lake la kufanya utafiti na kuwaomba ushirikiano wao.

Walimu walifahamishwa lengo la utafiti huo ili kuondoa wahka miongoni mwao. Mtafiti aliwaeleza kuwa alihitaji muda wa saa mbili kutagusana na wanafunzi wa chekechea katika madarasa na katika michezo ya nje, ili kubainisha matumizi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwao. Mtafiti vilevile alikagua nyenzo na vielelezo vilivyotumiwa na kubainisha ikiwa vimetajwa katika lugha ya Kiswahili. Muda uliochukuliwa katika kujaza utaratibu wa uchunzaji ni takriban nusu saa hivi. Muda huu ulimpa mtafiti nafasi bora ya kuchunguza na kunakili kwenye vijitabu.

Kwa vile wasimamizi wengine hawakuwa shuleni siku iliyoratibiwa, ilimbidi arejee baadaye ili kukamilisha ukusanyaji data ya utafiti. Mahojiano ya wasimamizi wa shule na wazazi yalifanyika afisini lakini kwa siku tofauti, sababu ilikuwa wazazi walifanyiwa mpango maalum wa kukutana na mtafiti. Muda uliochukuliwa kwa kila kikundi ni kati ya nusu saa hadi dakika arobaine

na tano. Data iliyokusanywa kupitia kwa njia moja ilibainishwa kupitia kwa nyenzo zingine za ukusanyaji data.

## 3.10 Uthabiti wa Vifaa vya Utafiti

Uthabiti wa vifaa vya kukusanyia data huashiria kiwango cha kupima ukamilifu wa kitu kinachotarajiwa kupimwa, Kothari (2003). Mtafiti alizingatia vipengele mbali mbali alipokuwa akiunda vifaa vya utafiti. Croll (1986) anadahili kuwa, ili vifaa viwe toshelevu katika utafiti wowote ule, ni sharti vithibitishwe na wataalamu. Mtafiti akishirikiana na wahadhiri wa idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi wa chuo kikuu cha Masinde Muliro, walichanganua majibu katika majaribio ya vifaa vya utafiti. uchanganuzi wa majibu katika majaribio ya nyenzo, ulimwezesha mtafiti kurekebisha baadhi ya maswali kwa lengo la kulainisha maswali na kuyafanya yawe na mantiki katika utafiti huu. Kwa hivyo, nyenzo na utekelezaji wa majukumu katika utafiti huu ulithibitishwa na wasimamizi wa utafiti.

## 3.11 Uaminifu wa Vifaa

Licha ya vifaa kuwa thabiti, ni sharti pia viaminike (Selinger na Shahomy, 1989). Vifaa vya utafiti huwa na uaminifu iwapo majibu sawa kwa kipindi kingine tofauti yatatolewa. Ili kupima uaminifu wa vifaa, mtafiti alitumia mbinu ya uradidi. Mtafiti aliwapa walimu wawili kutoka shule tofauti hojaji sawa mara mbili kwa siku tofauti kuandika na kujaza. Mtafiti alipima uthabiti wa vifaa kwa kuzingatia kauli zilizozingatiwa kwa vifaa hasa hojaji. Peil (1995) akichangia kuhusu uaminifu wa hojaji, anadahili kuwa hojaji yaweza kupimwa kwa kuhusisha vibadala vyote ambavyo watafitiwa wanaweza kutoa kama jawabu.

### 3.12 Matatizo Wakati wa Kukusanya Data

Utafiti huu ulikumbwa na matatizo kadhaa; muda uliotengwa wa kukusanya data haukuzingatiwa, na hivyo ukusanyaji data kucheleweshwa. Mtafiti alipokuwa nyanjani ilimwia vigumu wakati mwingine kukutana na wasimamizi wa shule za chekechea hasa za umma. Pia muda ambao ulitengwa wa kukutana na wazazi haukuzingatiwa. Matatizo haya hata hivyo haya kukwamiza shughuli za utafiti. Mtafiti alifaulu kukutana nao baadaye na kukusanya data aliyokusudia.

Ratiba za shule, afya ya mtafiti wakati mwingine ilikatiza utafiti. Kwa mfano, mtafiti hakuwa na muda wa kutosha kutagusana na walimu kwa vile walikuwa na shughuli nyengine walizopaswa kutekeleza.Ilimbidi awe na subira kabla ya kuhudumiwa na walimu waliotafitiwa. Mtafiti alikumbana na tatizo la hali ya anga lililoathiri usafiri pamoja na hali mbovu za barabara katika Manispaa hii.

Tatizo lililojitoikeza la baadhi ya walimu na wazazi kupuuza shughuli ya utafiti kwa kutopenda au kudai kuwa mada iliyorejelewa haikueleweka lilikuwa sugu. Baada ya kushauriana nao walisalimu amri walipoelezwa kiini cha utafiti kilikuwa kupata utatuzi kwa changamoto ya mada hiyo bali siyo kutathmini maarifa yao.

### 3.13 Utaratibu wa Uchanganuzi wa Data

Data ilikusanywa kupitia hojaji, masaili na uchunzaji. Ilichanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi elezi wa kitakwimu. Msingi wa kuainisha ulikuwa

kuweka pamoja vipengele ambavyo vilishughulikia lengo moja la utafiti. Kwa sababu utafiti ulikuwa wakimaelezo na kitakwimu, tulichanganua data kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: kuhariri, kukokoteza, kupanga, kuweka katika majedwali michoro; kisha kuihakiki na kuchanganua kwa kutazama idadi ya marudio kwa kila jibu. Data iliyotokana na maoni ya watafitiwa iliandikwa kwa njia ya maelezo.

### 3.14 Hitimisho

Sura hii ilijishughulisha na eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, muundo wa utafiti, nyenzo na mbinu za ukusanyaji data na majaribio ya nyenzo nyanjani. Haya yote yameelezwa katika tasnifu hii. Vifaa vya utafiti vilikuwa; hojaji kwa walimu wa chekechea, masaili kwa wasimamizi na wazazi wa chekechea na kiongozi cha uchunzaji kilichotumiwa katika mandhari ya chekechea. Sura inayofuatia inalenga uwasilishaji, uchanganuzi wa data na majadiliano ya matokeo.

## SURA YA NNE

## 4.0 UWASILISHAJI WA DATA NA MJADALA

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia uchanganuzi, uwasilishaji wa data na majadiliano ya matokeo ya utafiti. Data iliyokusanywa ilitokana na miitikio ya uchunzaji wa darasani, hojaji na dodoso. Uchunzaji wa darasani ulikusudia kupata habari kuhusu matumizi ya Kiswahili katika mandhari ya chekechea, baina ya walimu na wanafunzi, na kuwepo kwa nyenzo na vielelezo vyenye maandishi katika lugha ya Kiswahili. Hojaji kwa walimu wa chekechea, ilinuia kukusanya habari kuhusu matumizi ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea.

Katika sura hii, uchanganuzi wa data umewasilishwa kwa kutumia data za kitarakimu, majedwali ya marudio asilimia, chati, na grafu. Data iliyotokana na maswali huru iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Uchanganuzi wa data umegawanywa katika sehemu zifuatazo; sehemu ya kwanza inashughulikia miitiko ya walimu katika hojaji. Sehemu ya pili inahusu uchunzaji katika mandhari ya chekechea, huku sehemu ya tatu ikiwasilisha matokeo ya dodoso ya wasimamizi na wazazi ambao watoto husomea katika shule za chekechea zilizotafitiwa. Habari hizi zote zilimwezesha mtafiti kupata uelewa wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye.

## 4.2 Usuli wa Shule za Chekechea

Watafitiwa walihitajika kutoa habari kuhusu aina ya shule; data ilikusanywa kutoka shule kumi na tisa zikiwa katika makundi makuu mawili, mathalani shule za chekechea za umma na za kibinafsi. Mwalimu mmoja mmoja kwa kila shule alijaza hojaji. Matokeo yalikuwa ifuatavyo: Shule kumi na moja za Kibinafsi na nane za Umma zilizotafitiwa ziliwakilisha asilimia 30 ya kila kikundi. (Taz jedwali 2 uk. 60)

**Jedwali 2: Aina ya shule, Idadi na nambari ya Watafitiwa**

| Aina ya shule | Idadi ya shule | Idadi ya Watafitiwa |
|---|---|---|
| Shule za kibinafsi | 11 | 11 |
| Shule za Umma | 8 | 8 |
| **Jumla** | **19** | **19** |

Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti

## 4.3 Namna Kiswahili Kinavyotumika Katika Shule za Chekechea

### 4.3.1 Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea

Utafiti ulitubainishia kuwa, kuna matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye. Kwa sababu katika shule zote 19 za chekechea zilizotafitiwa ambazo zinawakilisha

asilimia 100 ya watafitiwa, walitoa kauli kwamba lugha hii hutumika. Haya yanatokana na lugha ya Kiswahili kutawala eneo la utafiti.

### 4.3.2 Jinsi Kiswahili Kinavyotumika Katika Shule za Chekechea

Sehemu hii ilihusu uhalisia wa namna lugha ya Kiswahili inavyobainika katika mandhari ya shule 19 za chekechea zilizotafitiwa. Ilibainika wazi kuwa kuchanganya msimbo kulidhihirika miongoni mwa shule 17 (89.5%) kutoka kwa shule 19 (100%) zilizotafitiwa, katika shule 1 (5.3%) kulikuwa na kubadili msimbo, shule nyengine 1 (5.3%) iliyosalia haikubainisha njia husika. Hata hivyo, takwimu zinatudhihirishia kuwa hakuna shule hata moja miongoni mwa shule 19 kulikopatikana matumizi ya Kiswahili pekee.

Matokeo haya yanaoana na ya utafiti wa Nyaga (1994) aliyechunguza mtindo wa kuchanganya msimbo kati ya Kiswahili, Kiingereza na Kiembu katika shule ya upili ya Kivutiri. Katika utafiti huo, aligundua kuwa kuchanganya msimbo ni jambo la kawaida katika shule za sekondari. Kwa upande mwingine, mtafiti anakubaliana na maoni ya Rubagunya (1994) alipodokeza kuwa, mojawapo ya mikakati inayobuniwa kurahisisha mawasiliano darasani ni kuchanganya msimbo kati ya lugha rasmi ya mafundisho na nyengine inayoeleweka katika mazingira hayo. Kwa mujibu wa utafiti huu, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na na wakati mwengine lugha mama, zilitumika kwa pamoja katika ufunzaji na ujifunzaji ili kurahisisha uelewa wa dhana. Iligunduliwa kuwa njia ya kuchanganya msimbo ilichukuwa sehemu kubwa kuliko njia iwayo yoyote. Kutanda kutoka lugha moja hadi nyingine, kunaweza kuashiria kutokuwa na ufasaha katika lugha moja ambayo hudhihirika kupitia kwa kuchanganya

msimbo. Hata hivyo wakati mwingine kuchanganya msimbo husababishwa na umilisi wa lugha mbili au zaidi kisawasawa. Umilisi wa lugha za mafundisho haukudhihirika. Taswira hii inaashiria ukosefu wa mtindo wa lugha bayana katika shule za chekechea. (Tazama Jedwali 3 uk.62)

**Jedwali 3: Namna Kiswahili Kinavyotumika Katika Shule za Chekechea**

| Namna Kiswahili Kinavyotumika | Idadi ya Miitikio | Asilimia % |
|---|---|---|
| Kuchanganya Misimbo | 17 | 89.5 |
| Kubadili Misimbo | 1 | 5.3 |
| Nyengine | 1 | 5.3 |
| **Jumla** | **19** | **100** |

Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti

### 4.3.3 Matumizi ya Kiswahili Katika Mafunzo ya Shule za Chekechea

Sehemu hii ilihitaji mwalimu kuonyesha njia mbalimbali ambapo Kiswahili huwasilishwa. Matokeo yalidhihirisha kuwa, lugha ya Kiswahili ilitumika kupitia kwa nyimbo, ushairi na mitagusano. Matumizi ya lugha ya Kiswahili yalishuhudiwa mno katika mitagusano, kwa vile watafitiwa 16 (84.2%) waliunga mkono njia hii, ilhali 13 (68.4%) walipendekeza nyimbo, huku watafitiwa 11 (57.9%) wakipigia upatu ushairi, mtafitiwa 1 (5.3%) alitaja njia nyengine ambayo haikubainishwa.

Katika uchunzaji, mtafiti alitarajiwa kushuhudia uhalisia wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji kupitia nyimbo, ushairi na mitagusano. Matokeo katika uchunzaji yalitofautiana na yale ya awali katika hojaji. Katika shule 18 (94.7%) matumizi ya Kiswahili kupitia nyimbo kwenye shule 15 (78.9%) ushairi, shule 6 (68.4%) mitagusano, katika shule 4 (21.1%) matumizi ya Kiswahili yalijitokeza katika vitabu. Maelezo haya yameonyeshwa katika (Jedwali 4.uk, 63)

**Jedwali 4: Matumizi Mbalimbali ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea**

| **Njia ya Matumizi ya Kiswahili** | **Idadi ya watafitiwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Nyimbo | 13 | 68.4 |
| Ushairi | 11 | 57.9 |
| Mitagusano | 16 | 84.2 |
| Nyengine | 1 | 5.3 |

Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti

Kutokana na jedwali 4, matumizi mengi ya lugha ya Kiswahili yalishuhudiwa katika ushairi, nyimbo na mitagusano. Katika mitagusano, ndiko kulikojitokeza matumizi ya kiwango cha juu, kwani watafitiwa16 (84.2%) kati ya 19 (100%) walitumia lugha ya Kiswahili katika miktadha ya ufunzaji na ujifunzaji. Sababu inaweza kuwa, watoto walipata uhuru wa kutagusana bila kudhibitiwa na walimu wao wakati wa ufunzaji na ujifunzaji. Matumizi ya nyimbo na ushairi

katika ufunzaji na ujifunzaji yalifuatia mitagusano kwa vile matumizi ya nyimbo na ushairi hurahisisha ufahamu wa mada wakati wa mafundisho katika shule za chekechea.

Katika kuangalia uchunzaji, matokeo yalitofautiana na ya hojaji katika miktadha ya ufunzaji na ujifunzaji kwa vile, wanafunzi wengi wa chekechea hufunzwa kupitia nyimbo na ushairi. Hata hivyo, matumizi ya lugha ya Kiswahili yalipungua katika mitagusano kwa vile huenda uwepo wa mtafiti na mwalimu uliwatia hofu. Hili ni dhihirisho kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili yanashuhudiwa katika shule za chekechea kwenye Manispaa ya mji wa Webuye. Matumizi haya yametokana na uzoefu wa wakaazi wa eneo la utafiti kutagusana kupitia lugha ya Kiswahili.


Kwa upande mwingine, matumizi ya chini mno 4 (21.1%) yalijitokeza kupitia vitabu, pengine hali hii ilisababishwa na ukosefu wa vifaa hivi katika madarasa ya chekechea. Sababu nyengine ni walimu na wanafunzi wa shule za chekechea katika eneo la utafiti, walibobea katika stadi ya kuzungumza kuliko ile ya kuandika.

### 4.4.0 Watumiaji wa Kiswahili Katika Shule za Chekechea

Walimu walihitajika kutaja watumiaji wa lugha ya Kiswahili katika mandhari ya chekechea. Katika kulishughulikia suala hili, mtafiti alitarajia watafitiwa wakubaliane au wapinge kauli zilizokuwa zimependekezwa na mtafiti kuhusiana na watumiaji wa lugha ya Kiswahili katika mandhari ya shule za chekechea. Ilibainika wazi kuwa walimu 16 (84.2 %) kati ya 19 (100 %)

hutumia Kiswahili katika mitagusano na wanafunzi. Walimu 19 (100 %) walikubaliana kuwa katika shule zote 19 zilizotafitiwa, wanafunzi wote hutumia Kiswahili. Mtafiti aliwataka walimu wataje lugha ambayo wanafunzi wanaweza kujieleza, wakati wa ufunzaji na ujifunzaji. Walimu 15 (78.9%) walitaja lugha ya Kiswahili, waliosalia ambao ni 4 (21.1%) walipinga kuwa wanafunzi wa chekechea hawawezi kujieleza vyema katika lugha ya Kiswahili. Katika swali ilo hilo, walimu 9 (47.4%) walitoa kauli kuwa, wana uwezo wa kujieleza vyema katika lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, ushahidi wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea, ulidhihirika zaidi tulipochunguza majibu yaliyotolewa katika dodoso ya wasimamizi wa shule za chekechea. Walitaja umaarufu wa lugha ya Kiswahili, kama ifuatavyo; wasimamizi 12 (63.2%) walitaja lugha ya Kiswahili, 4 (21%) Kiingereza, ilhali 3 (15.8%) walidahili kuwa ni lugha mama. (Taz. Kielelezo 1 uk. 66)

**Kielelezo 1: Watumiaji wa Lugha ya Kiswahili**




Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti

Kutokana na matokeo haya, twaweza kusema kuwa Kiswahili hutumika kwa kiwango cha juu 19 (100%) kwa wanafunzi, 16 (84.2%) miongoni mwa walimu. Ufichuzi huu unaenda sambamba na aliyosema Mochiwa (1979) kuwa wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza huwa hawapati shida ya kutumia lugha ya kiswahili kwa vile walikwisha isikia na kuitumia wakiwa nyumbani na katika shule za chekechea. Maoni aliyoyatoa yanafaa kwa vile yanaonyesha kuwa mazingira ya chekechea yanayowazunguka husheheni lugha ya Kiswahili. Matokeo haya yanaonyesha kuwa, licha ya Kiswahili kutumika katika mandhari ya chekechea. watafitiwa 4 (21.1%) walikiri kuwa hawana ufahamu tosha. Ufichuzi mwingine ni kuwa, hakuna mipaka mahususi kati ya lugha mama na lugha ya Kiswahili. Sababu ni kuwa kwa wanafunzi wengine lugha mama ni Kiswahili.

Majibu ya wasimamizi yalidhihirisha ukweli kuwa wakaazi wa Manispaa ya Webuye ni watu mseto wanaotagusana kupitia lugha ya Kiswahili. Dhihirisho la umaarufu wa lugha ni wakati lugha inahamishwa kutoka katika mazingira ya nyumbani na kuletwa katika mandhari ya shuleni. Kwa mujibu wa utafiti huu, lugha ya Kiswahili imehamishwa kutoka katika eneo la utafiti hadi shule za chekechea. Licha ya umaarufu wa lugha ya Kiswahili, watumiaji wa lugha ya Kiswahili waliadhiriwa kwa vile hakuna shule hata moja iliyopatikana ikizungumza msimbo wa Kiswahili pekee. Hali hii inadhihirisha kuwa hakuna urasmi unaoambatanishwa na lugha ya Kiswahili katika mazingira ya chekechea.

### 4.4.1. Miktadha ya Matumizi ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea

Walimu walihitajika kutaja miktadha ambamo wao hutumia Kiswahili. Watafitiwa 14 (73.6%) walitaja michezoni, 14 (73.6%) wakati wa mitagusano, watafitiwa 13 (68.4%) darasani, 8 (42.1%) wakati wa maankuli ilhali 2 (10.5%) wakati mwingine. Matokeo kama yanavyobainika katika jedwali 5 yanaonyesha ya kwamba miktadha ya matumizi ya Kiswahili ni katika mitagusano, michezoni na darasani. (Taz. Jedwali 5 uk. 68)

**Jedwali 5: Miktadha ya Matumizi ya Kiswahili katika Shule za Chekechea**

| **Muktadha** | **Ndio** | | **La** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Idadi** | **Asilimia %** | **Idadi** | **Asilimia %** |
| Michezoni | 14 | 73.6 | 5 | 26.3 |
| Darasani | 13 | 68.4 | 6 | 31.6 |
| Wakati wa Maakuli | 8 | 42.1 | 11 | 57.9 |
| Mitagusano | 14 | 73.7 | 5 | 26.3 |
| Wakati Mwingine | 2 | 10.5 | 17 | 89.5 |

Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti

Kutokana na ufahamu huo, lililofichuliwa ni kuwa, walimu wengi walikiri kuwa lugha ya Kiswahili ilitumika kwa asilimia 73.6% katika michezo na katika mitagusano. Katika miktadha yote miwili kuna mwingiliano kwa sababu wakati wa michezo ndipo wanafunzi pia hutagusana. Kuna uwezekano mkubwa kwamba hawakuwa katika miktadha rasmi chini ya usimamizi wa walimu wao, bali walikuwa na uhuru wa kujieleza wapendavyo. Katika muktadha wa mankuli matumizi ya lugha yalikuwa chini mno kwa sababu wanafunzi hawa walikuwa wamedhibitiwa na walimu wao, hivyo hawakuwa na uhuru wa kujieleza. Wakati ule mwingine ambao haujabainishwa, uliashiria matumizi ya lugha nyengine kando a lugha ya Kiswahili. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika miktadha halisi ndio nguzo katika ufunzaji na ujifunzaji kwa vile lugha haizungumziwi bali hutumika katika mawasiliano, haya ni kwa mujibu wa McGregor (1971).


### 4.4.2 Umilisi wa Walimu Katika Lugha ya Kiswahili

Sehemu hii ilihitaji mwalimu kuonyesha iwapo alikuwa na ufahamu mzuri wa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kati ya walimu 19 (100%) waliotafitiwa, tarakimu zinaonyesha kuwa walimu 17 (89.5%) wanaweza kufundishia kwa lugha ya Kiswahili, ilhali 2 (10.5%) walikiri kuwa hawana ufahamu wa kina wa lugha Kiswahili. Umilisi wa walimu katika lugha ya Kiswahili. (Kielelezo 2 uk. 70)

### 4.4.3 Mikakati ya Kuendeleza Lugha ya Kiswahili

Watafitiwa walihitajika kuonyesha ikiwa kuna mikakati yoyote ya kuendeleza lugha ya Kiswahili katika eneo la utafiti. Kati ya watafitiwa 19 (100%) ambao ni walimu wa shule za chekechea, watafitiwa 17 (89.5%) walitaja kuwa hakuna mikakati yoyote iliyowekwa ya kuendeleza lugha ya Kiswahili. Walimu 2 (10.5%) waliosalia walitaja kuwa lugha ya Kiswahili huendelezwa kupitia nyimbo na ushairi. Swali sawa na hilo katika dodoso ya wasimamizi wa shule za chekechea lilifichua kuwa, wasimamizi 12 (68.4%) walitoa kauli kuwa hakukuwa na mikakati yoyote ya kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili. Swali lililofuatia liliwataka wasimamizi wataje aina ya mikakati, watafitiwa 8 (42.1%) walitaja nyimbo na ushairi. Jedwali 6 linaonyesha ya kwamba kuna upungufu wa kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea.

**Kielelezo 2: Umilisi wa Walimu katika Lugha ya Kiswahili**




Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti.

Matokeo haya yanaonyesha kuwa walimu wa shule hizi wanajimudu vyema katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Majibu haya yanaoana na data ya awali iliyoonyesha kuwa wanafunzi ni kati ya watafitiwa waliotajwa kujieleza vyema katika lugha ya Kiswahili. Hivyo ikiwa wanafunzi wana umilisi wa lugha hii, sembuse walimu wao. Ufichuzi huu unaenda sambamba na alivyosema Chimerah (1988) alipodahili kuwa, mtoto anapokuwa kwenye kundi linalozungumza lugha ya Kiswahili, hufanya mazoezi ya kutosha katika lugha hiyo kupitia mazungumzo, michezo na ushairi. Mawazo sawa na mtaalamu

huyu yanashadidiwa na Munyua (2007) alipodahili kuwa, mwalimu ndiye nguzo ya maarifa katika somo. Hivyo basi ni muhimu wapewe mafunzo kikamilifu katika vyuo vya mafunzo ya chekechea, ili kuwawezesha kutumia vyema lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea.

**Jedwali 6: Mikakati ya Kuendeleza Kiswahili Katika Shule za Chekechea**

| **Njia Mbalimbali** | **Miitikio ya Watafitiwa** | **Asilimia %** |
|---|---|---|
| Nyimbo na Ushairi | 15 | 78.9 |
| Nyenzo na Vielelezo | 3 | 15.8 |
| Vitabu na Majarida | 1 | 5.3 |
| **Jumla** | **19** | **100** |

Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti

Kutokana na kielelezo 2 na jedwali 6, inabainika wazi kuwa hakuna mikakati mipya ya kuendeleza lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea, ila nyimbo na ushairi. Hata watafitiwa 8 (42.1%) waliotoa kauli kuwa kuna mikakati walitaja nyimbo na ushairi, ambazo huwa ni njia mojawapo ya kuendeleza ufunzaji na ujifunzaji. Ukosefu wa mikakati ya kuendeleza lugha ya Kiswahili, ulitokana na ukosefu wa ari miongoni mwa wasimamizi wa shule za chekechea ambao ni washika dau wakuu, walio na uwezo wa kufaulisha mikakati ya kuendeleza lugha ya Kiswahili. Tukizingatia mawazo ya Chimerah (1988) kuhusu weledi wa lugha, anatudokezea kuwa weledi hubobea katika uwanja mmoja bali siyo nyanja nyingi. Kwa mujibu wa utafiti huu ukosefu wa

mikakati bunifu ya kuendeleza lugha ya Kiswahili ni kizuizi kikubwa katika kuwaandaa wanafunzi na walimu kubobea katika lugha ya Kiswahili.

Matokeo kwenye dodoso ya wasimamizi yalituthibitishia kuwa, hakuna mikakati ya kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili. Wasimamizi 12 (68.4%) walitaja kuwa hakukuwa na mikakati, kati ya walimu 19 (100%) waliotafitiwa, walimu 17 (89.5%) walitoa kauli kuwa hawajawahi kuhudhuria kozi zozote za mafunzo katika lugha ya Kiswahili. Walipoulizwa sababu za kutohudhuria kozi, walimu 15 (78.9%) walidai kuwa hazijaandaliwa. Mandhari haya ni tofauti na alivyosema (Shiundu na Omulando, 1992) kwamba semina au warsha ni kozi ambazo hupiga walimu msasa. Huwawezesha kufahamu mabadiliko yanayotokea mara kwa mara katika mtaala. Walimu katika shule za chekechea, husalia tu na tajriba za awali waliopata chuoni au katika eneo la utafiti.

**4.5 Changamoto za Matumizi ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea**

Walimu waliulizwa kutoa uamuzi kuhusiana na kauli mbalimbali zilizotolewa. Kauli hizi zilitumiwa kutoa uamuzi kuhusiana na changamoto zinazokabili matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kipimo cha Likert kilitumiwa kutathmini changamoto zinazokabili matumizi ya lugha ya Kiswahili. Jedwali nambari 7, linaonyesha kauli 9 ambazo zinaaminika ni changamoto zinazoathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea. Kulikuwa na kauli tisa ambazo msailiwa alikuwa na hiari ya kuweka alama ya kukubaliana, kukataa au kutokuwa na uhakika.(Taz. Jedwali 7 uk. 73)

**Jedwali 7: Changamoto za Matumizi ya Kiswahili Katika Shule za Chekechea**

| Kauli | Nakubaliana | % | Sina Uhakika | % | Nakataa | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiswahili hakifai | 2 (10.5) | | 0 | 0 | 17 | 89.5 |
| Kiswahili hakina utoshelevu | 12 | 63.2 | 3 | 15.8 | 4 | 21.1 |
| Kiswahili ni lugha ya kawaida | 15 | 78.9 | 2 | 10.5 | 2 | 10.5 |
| Kiswahili hakina nafasi katika ulimwengu wa sasa | 17 | 89.5 | 1 | 5.3 | 1 | 5.3 |
| Ni vigumu kufundisha kwa lugha ya Kiswahili | 11 | 57.9 | 5 | 26.3 | 3 | 15.8 |
| Kiswahili hakijaungwa mkono na washika dau | 2 | 19.5 | 0 | 0 | 17 | 89.5 |
| Sera ya lugha katika shule inapinga matumizi yake | 9 | 47.4 | 0 | 0 | 10 | 52.6 |
| Kiswahili kinahusishwa na watu wa tabaka la chini | 11 | 57.9 | 3 | 15.8 | 5 | 26.3 |

Tanbihi: Kwenye mabano ni asilimia

Watafitiwa 17 (89.5%) walikataa kukubaliana na kauli ya kwanza ambayo ilisema kuwa Kiswahili hakifai. Watafitiwa 2 (10.5%) kutoka katika shule za kibnafsi ndio waliokubaliana na kauli hiyo. Inadhihirika wazi kuwa, hawa wawili waliongozwa na sera ya lugha iliyokuwa kinyume na matumizi ya lugha

ya Kiswahili, kwa hivyo twaweza kusema kuwa Kiswahili kinadhaminiwa na kutumiwa na jumuiya pana ya chekechea katika eneo la utafiti.

Kauli kuwa Kiswahili hakina msamiati toshelevu, iliungwa mkono na watafitiwa 12 (63.2%) huku watafitiwa 4 (21.1%) wakipinga, ilhali 3 (15.8%) wasijue la kusema. Yamkini idadi kubwa iliyokubaliana kuwa Kiswahili hakina msamiati toshelevu inaweza kuhusishwa na ukosefu wa nyenzo, vielelezo, majarida na vitabu katika shule zilizotafitiwa. Kuna uwezekano kuwa, walimu wa chekechea hutumia Kiswahili chepesi kinachofaa umri huu wa wanafunzi. Ingawa Omulando (2002) hakutafitia shule za chekechea bali mchango wake kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili ulifaa utafiti huu, kwa sababu baadhi ya walimu walidai kuwa lugha ya Kiswahili haina msamiati faafu. Matokeo kwinginepo, yameonyesha ya kwamba ndiyo lugha itumiwayo kwa mapana katika mandhari ya chekechea. Matokeo haya yanaonyesha kuwa, matumizi ya lugha ya Kiswahili japo yapo, yanakumbwa na changamoto ya kutokuwa na msamiati toshelevu.

Watafitiwa waliuzwa watoe uamuzi wao kuhusu matumizi ya Kiswahili, watafitiwa 17 (89.5%) walikiri kuwa Kiswahili ni lugha ya kawaida. Kati ya waliosalia, 1(5.3%) alipinga huku mwingine asijue la kujibu. Ukawaida wa lugha ya Kiswahili, unaweza kutokana na mazoea ya matumizi yake mapana katika eneo la utafiti. Haya yanadhihirisha kuwa, lugha ya Kiswahili japo inatumiwa katika mafunzo ya chekechea, haijapewa hadhi inayostahili ndiposa ikaonekana kama lugha ya kawaida.

Dai kwamba Kiswahili hakina nafasi katika ulimwengu wa sasa, liliungwa mkono na jumla ya watafitiwa 17 (89.5%), huku 1 (5.3%) akipinga, ilhali 1 (5.3%) aliyesalia akikosa uamuzi mahsusi. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, suala la Kiswahili kukosa nafasi katika ulimwengu wa sasa limeungwa mkono na watafitiwa wengi, matokeo haya yanaoana na yale ya Barasa (1997) ambaye anadai kuwa licha ya Kiswahili kuwa maarufu miongoni mwa wanafunzi, hakiwezi kutegemewa kufundishia hata chembe katika ulimwengu huu wenye ushindani mkubwa. Mitazamo sawa na hii imepingwa vikali na Simala (2001) alipotetea lugha ya Kiswahili kwa kusema kuwa, matumizi yake yanaweza kutegemewa katika sayanzi na teknolojia ilmuradi wapangaji sera wafahamu umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Simala (2001) Anatoa mfano wa nchi ya Tanzania, ambapo matumizi ya lugha ya Kiswahili yameshamiri asasi zote za elimu. Inavyobainika kutokana na utafiti huu ni kuwa, licha ya Kiswahili kutumika kwa kiwango kikubwa katika shule za chekechea, hakidhaminiwi katika ulimwengu wa sasa.

Watafitiwa walihitajika kutoa msimamo wao kuhusiana na dai kuwa, ni vigumu kufundisha katika lugha ya Kiswahili. Watafitiwa 11 (57.9%) walikubaliana, 3 (15.8%) walikataa huku 5 (26.3%) wakikosa msimamo dhabiti. Katika kipengele hiki ndipo palipokuwa na idadi kubwa ya watafitiwa ambao hawakuwa na uhakika wa jawabu. Matokeo haya yanaonyesha kuwa katika shule za chekechea, kuna idadi kubwa ya walimu ambao wanapata ugumu wa kufundisha katika lugha ya Kiswahili, ufichuzi huu unaenda sambamba na matokeo ya awali yaliyoonyesha kuwa, hakuna shule hata moja kulikopatikana matumizi ya Kiswahili sanifu bali kilichodhihirika ni

uchanganyaji msimbo. Swala hili linatiliwa nguvu na Mulama & Matteru (1978), Mkwizu (2002) walipodahili kuwa, kati ya mambo yanayoathiri walimu kwa wanafunzi ni ukosefu wa umilisi katika lugha ya Kiswahili. Athari mojawapo ya hali hii, ni kutopata uelewa wakati wa ufunzaji na ujifunzaji. Kutokana na matokeo haya, inaonekana kuwa walimu wa chekechea hawana umilisi katika lugha ya Kiswahili.

Walimu waliulizwa kutoa msimamo wao kuhusu kauli iliyosema kuwa washika dau wanapinga matumizi ya lugha ya Kiswahili, watafitiwa 11 (57.9%) walikubaliana na kauli hii, ilhali 8 (42.1%) walikataa. Kwa mujibu wa data iliyokusanywa kutoka kwa masaili ya wasimamizi wa shule, ilibainika wazi kuwa 14 (73.68%) walikiri kuwa hakukuwa na mikakati yoyote iliyowekwa ya kuendeleza lugha ya Kiswahili, huku 15 (78.94%) vilevile wakitoa madai kuwa, hakujaandaliwa kozi zozote katika matumizi ya Kiswahili, kwa mafunzo ya shule za chekechea. Watafitiwa walipoulizwa wapendekeza lugha ambayo inafaa kwa mafundisho ya watoto wao, 15 (78.94%) walitaja lugha ya Kiingereza. Huku watafitiwa 4 (21.1%) wakipendekeza lugha ya Kiswahili.

Wazazi wa chekechea walipoulizwa wapendekeze lugha ambayo wangependa watoto wao wafundishiwe, watafitiwa 15 (78.9%) walipendekeza lugha ya Kiingereza, 6 (31.6%) Kiswahili, 1 (5.3%) Lugha mama. Kutokana na tarakimu hizi, matokeo yanaashiria kuwa, lugha ya Kiingereza inapigiwa upatu na washika dau, ni kweli kuwa Kiswahili kinatumika zaidi katika mawasiliano tamkwa, lakini matokeo haya ni kinyume cha matarajio kwa vile si lugha inayoungwa mkono. Matokeo haya ni sambamba na mawazo ya Gardener

(1977). Anaonyesha kuwa mapendeleo dhidi ya lugha lengwa katika jamii ni tatizo lililoenea na yanatokana na mielekeo hasi. Kwa hivyo, katika eneo la utafiti lugha ya Kiingereza ina hadhi kuliko lugha ya Kiswahili.

Mtafitiwa alihitajika kuonyesha msimamo wake kuhusiana na iwapo sera ya lugha katika shule hizi inapinga matumizi ya lugha ya Kiswahili. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo; watafitiwa 9 (47.4%) walikiri kuwa sera ya lugha inapinga matumizi ya lugha ya Kiswahili, huku 10 (52.6%) wakikanusha kauli iliyotolewa. Majibu yaliyotolewa na walimu yalionyesha kuwa hawakujishughulisha na sera ya lugha, bali lengo lao kuu lilikuwa kuwasiliana na wanafunzi. Matokeo sawa na haya yalidhihirika kwenye sehemu ya masaili, kwa vile wasimamizi wa shule walipoulizwa wataje lugha ambazo sera ya lugha inapendekeza; waliotaja lugha ya Kiswahili walikuwa 11 (57.9%), lugha mama 7 (42.1%), huku 7 (42.1%) wakiunga mkono Kiingereza. Habari hizi zinaweza kuambatishwa na uhuru walio nao wa kutumia lugha wapendavyo. Ni bayana kutokana na takwimu hizi za wasimamizi wa shule, kwamba kuna matumizi ya lugha mbalimbali, ingawa katika viwango tofauti. Mtafitiwa 1 (5.3%) ndiye aliyetaja matumizi ya Kiswahili na Kibukusu. Idadi ya waliozipendekeza lugha za Kiswahili / Kiingereza, ilikuwa ya watafitiwa 5 (26.31%). Kwa vile eneo la utafiti linajumuisha watu mseto wanaozungumza lugha mbali mbali mathalani Kiswahili na Kiingereza. Kutokana na matokeo haya, ni wazi kuwa sera ya lugha ipo, bali utekelezaji wake haujasawasishwa, na huenda mapendeleo katika lugha zilizotumika katika shule hizi ilisababishwa na dhima mbalimbali za lugha hizo ambazo zilikuwa zinatekelezwa. Matokeo haya yanaoana na mswada aliouwasilisha

Nyonyontino (1980) uliofichua kuwa kipengele ambacho kingali na mushkeli katika shule za chekechea ni swala la lugha. (Taz. Jedwali 8 uk. 78)

**Jedwali 8: Sera ya Lugha na Maoni ya Wasimamizi wa Shule za Chekechea.**

| **Lugha** | **Idadi** | **Asilimia %** |
|---|---|---|
| Kiingereza | 2 | 10.52 |
| Kiswahili/Kibukusu | 1 | 5.26 |
| Kiswahihi/Kiingereza | 5 | 26.31 |
| Kiswahili | 11 | 57.89 |
| **Jumla** | **19** | **100** |

Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti

Kauli ya mwisho katika sehemu hii, iliwatarajia watafitiwa watoe msimamo wao kuhusiana na Kiswahili kuhusishwa na watu wa tabaka la chini, dhana hii iliungwa mkono na watafitiwa 11 (57.9%), waliopinga walikuwa 5 (26.3%), ilhali 3 (15.8%) wakionyesha hali ya kutokuwa na msimamo. Idadi kubwa ya watafitiwa walikubaliana na kauli hii kuonyesha kuwa, ingawa matumizi ya lugha ya Kiswahili yanashamiri mafunzo ya shule za chekechea bali mielekeo ya walimu kuhusiana na lugha hii inatupelekea kuamini kuwa haijapewa hadhi inayostahili katika jamii.

Matumizi yake yanaonyesha kuwa hawana hiari kwa sababu ndio lugha iliyozagaa katika eneo la utafiti. Waliopinga kuwa lugha ya Kiswahili

haihusishwi na tabaka la chini walikuwa wachache mno, kuashiria kuwa licha ya lugha hi.i kutumiwa, haijadhaminiwa mno katika jumuiya ya chekechea. Matokeo haya yanaenda sambamba na mchango alioutoa Mushingi (1989) kuwa watu huamini kwamba, hakuna haja ya kutumia Kiswahili kufundishia watoto kwa vile tayari wanakifahamu.Ukosefu wa ufahamu miongoni mwa watu kuhusiana na nafasi ya lugha ya Kiswahili inadhihirika wakati ambapo asilimia 15.8 wanaashiria kutokuwa na jawabu kwa kauli hiyo. (Taz. Jedwali 9 uk 80.)

### 4.6 Sababu za Matumizi ya Kiswahili Katika Mafunzo ya Shule za Chekechea

Kipimo cha likert kilitumiwa kutathimini sababu za matumizi ya Kiswahili katika shule za chekechea. Kauli zote katika sehemu hii zilikuwa 10, kulikuwa na viwango vitatu: kukubali, kutokuwa na uhakika na kukataa. Taz. Jedwali 9 uk.80

**Jedwali: 9 Muhtasari wa Sababu za Matumizi ya Lugha ya Kiswahili**

| N | KAULI | Nakubaliana | | Sina uhakika | | Nakataa | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| 1 | Kiswahili ni lugha bora | 8 | 42.1 | 4 | 21.1 | 7 | 36.8 |
| 2 | Lugha ya Kiswahili hutawala mazungumzo | 15 | 78.8 | 0 | 0 | 4 | 21.1 |
| 3 | Ni lugha mama kwa wengi | 10 | 56.2 | 1 | 5.3 | 8 | 42.1 |
| 4 | Ni rahisi kuchanganya msimbo | 16 | 84.2 | 1 | 5.3 | 2 | 10.1 |
| 5 | Ni rahisi kubadili msimbo | 8 | 42.1 | 1 | 5.3 | 10 | 52.6 |
| 6 | Kiswahili kina msamiati toshelevu | 5 | 26.3 | 2 | 10.1 | 12 | 63.2 |
| 7 | Kiswahili ni lugha muhimu | 11 | 57.9 | 3 | 15.8 | 5 | 26.3 |
| 8 | Kiswahili kinaeleweka kwa urahisi | 15 | 78.9 | 1 | 5.3 | 3 | 15.8 |
| 9 | Kuna nyenzo katika lugha ya Kiswahili | 4 | 21.1 | 0 | 0 | 15 | 78.9 |
| 10 | Ni lugha eneo kwa wengi | 19 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 |

Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti

Katika kauli ya kwanza, watafitiwa 8 (42.1%) walikubali kuwa Kiswahili ni lugha bora ya kufundishia walimu 7 (36.8%) walikana, huku 4 (21.1%) wakikosa uhakika wa jawabu. Aidha matokeo hayo yanaonyesha kuwa ufaafu

wa lugha hii si bayana, kwa sababu kulikuwa na tofauti ndogo kati ya waliounga na waliokosa kukubaliana na kauli hii.

Katika kauli ya pili iliyodahili kuwa Kiswahili hutawala mazungumzo, watafitiwa 15 (78.9%) walikubali huku 4 (21.1%) wakikana. Hakukuwa na mtafitiwa hata mmoja aliyekosa msimamo juu ya kauli hii, kumaanisha kuwa lugha ya Kiswahili hutumiwa na wengi katika eneo la utafiti. Matokeo haya yanaafikiana na kipengele katika dodoso ya wasimamizi wa shule za chekechea, ambapo waliulizwa wataje lugha maarufu, wasailiwa 15 (78.4%) walitaja lugha ya Kiswahili. Wazazi wa chekechea walipoulizwa swali kuhusiana na lugha wanayowasiliana na watoto wao, wasailiwa 11 (57.9%) walisema ni lugha ya Kiswahili, ilhali 4 (21.1%) lugha mama.  Idadi iliyosalia ya wazazi ilitaja lugha ya Kiingereza. Matokeo haya yanaafikiana na utafiti uliofanywa na Rubagunya (1994) kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika shule za sekondari. Tofauti kati ya utafiti huu na wa Rubagunya ni kuwa, wake ulijikita katika shule za sekondari katika nchi ya Tanzania, huku mtafiti akijishughulisha na shule za chekechea katika Manispaa ya mji wa Webuye. Matokeo ya Rubagunya yaliashira kuwa, wakati wa ufunzaji na ujifunzaji, walimu walitumia Kiswahili wakati wa somo la Kiingereza. Ilhali matokeo katika utafiti huu yameashiria kuwa lugha ya Kiswahili hutawala ufunzaji na ujifunzaji.

Dhana kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha mama, iliungwa mkono na watafitiwa 10 (56.2%), mtafitiwa 1(5.3%) hakukuwa na msimamo, waliosalia 8 (42.1%) walikana. Tarakimu hizi zinaonyesha kuwa watafitiwa wengi wanakubaliana

kuwa Kiswahili ni lugha mama, idadi inayopinga kauli hii inaashiria kuwa wanatambua lugha zao za Kienyeji kama lugha mama. Makala yaliyoandikwa na Kembo (2002) yanaunga mkono matokeo haya, akizungumzia lugha ya mafundisho katika shule za chekechea za mijini, anataja kwamba Kiswahili ni lugha mama kwa wengi wa wakaazi wa mjini. Majibu ya wahojiwa katika swali hili yaliafikiana na tahadhania za utafiti kuwa watu wa eneo la utafiti huzungumza lugha ya Kiswahili. Kutokana na takwimu hizi, watafitiwa wote hawakuunga mkono dhana isemayo kuwa Kiswahili ni lugha mama, hata hivyo kuna baadhi ya watafitiwa ambao huzungumza Kiswahili kama lugha yao ya kwanza. Kutokana na mawazo haya tunapata kuelewa kuwa lugha ya mama ni lugha ya kwanza ambayo hutumia kuwasiliana na jamii yake.

Dhana kuwa ni rahisi kuchanganya msimbo unapotumia lugha ya Kiswahili, takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa watafitiwa 16 (84.2%) walikubaliana, ilhali 2 (10.1%) wakikataa. Aliyesalia, 1(5.3%) asijue la kuchangia. Ufichuzi huu una mantiki, kwa vile katika shule zilizotafitiwa, ufunzaji na ujifunzaji uliendelea kwa kutumia lugha zaidi ya moja; mathalani Kiingereza, Kiswahili na kienyeji. Matokeo sawa na haya yameshuhudiwa katika utafiti wa Broughton (1980) ulionyesha kuwa kuchanganya msimbo ni kawaida katika asasi za elimu na watumiaji wa lugha hufanya hivyo ili kuwasiliana. Matokeo sawa na haya, yameshuhudiwa katika tafiti zilizofanywa katika nchi za nje. Katika utafiti wenye mada matumizi ya lugha katika vidato vya chini vya shule za sekondari kule Hong Kong, uliofanywa na Gibbons (1989) katika Kennedy (1989). Aligundua kuwa, katika shule zinazostahili kutumia lugha ya Kiingereza kufundishia, kanuni hiyo haikuzingatiwa, badala yake

walichanganya msimbo wa Kichina na Kiingereza. Matokeo ya Gibbons (1989) yanaweza kulinganishwa na asasi za elimu nchini Kenya zinazozingatia wingi lugha katika ufunzaji na ujifunzaji, Kwa vile utafiti wa Gibbons ulilenga matumizi ya Kiingereza katika shule za sekondari. Kutokana na matokeo hayo, inaelekea kuwa ni rahisi kuchanganya msimbo wa Kiswahili na lugha nyengine kama vile Kiingereza au lugha za Kienyeji.

Katika kauli hii, mwalimu alihitajika kuthibitisha matumizi ya ubadilishaji msimbo.  Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo; watafitiwa 15 (78.9%) walikana kuwa si mojawapo ya sababu za matumizi ya Kiswahili, huku watafitiwa 4 (21.1%) wasiwe na jawabu kamili. Data hizi zina mashiko kwa vile katika shule zilizotafitiwa, hakukuwa na ubadilishaji msimbo, bali kilicho kuwa dhahiri ni kuchanganya msimbo. Majibu haya yanaonyesha kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule hizi si fasaha, bali kilichodhihirika ni matumizi ya lugha mseto.

Kiongozi cha uchunzaji kitumiwapo hutupa picha halisi kuhusiana na tukio linaloendelea. Hivyo ushahidi tulioupata nyanjani ulionyesha kuwa katika shule 19 zilizotafitwa, katika shule 6 (31.57%), tulishuhudia matumizi ya uchanganyaji msimbo baina ya Kiswahili na Kiingereza, katika shule 2 (10.52%), Kiswahili na Kibukusu zilitumika katika muktadha mmoja. Shule zingine 11(57.8%) zilizosalia zilitumia mseto wa lugha mbili au tatu mathalani Kiswahili na Kiingereza.

Walimu wa chekechea walitarajiwa kutoa mchango wao kuhusiana na kauli kuwa lugha ya Kiswahili ina msamiati toshelevu. Kauli hii ya msamiati kwa kiwango hiki cha chekechea ni muhimu na ndiyo hujenga msingi wa lugha ya Kiswahili. Watafitiwa 12 (63.2%) walipinga kauli hiyo, 5 (26.3%) wakiikubali. Waliosalia 2 (10.5%) wasijue la kusema. Wahojiwa waliokana yamkini ndio wao ao waliotanda kutoka lugha moja hadi lugha nyengine, utafiti huu ulifichua kuwa, lugha ya Kiswahili ilitumika katika lugha tamkwa kuliko lugha andishi, hali hii inathibitishwa utafiti unaonyesha kuwa nyenzo zilizokuwa na maandishi katika lugha ya Kiswahili zilikuwa chache mno. Huenda watafitiwa waliopinga kuwa hakuna msamiati katika lugha ya Kiswahili walijiegemeza kwenye sababu hii.

Kwa upande mwingine, walipoulizwa maoni yao kuhusiana na umuhimu wa lugha ya Kiswahili, watafitiwa 11 (57.9%) walishuhudia kuwa ni lugha muhimu, watafitiwa 5 (26.3%) walikataa ilhali 3 (15.8%) wasijue la kusema. Idadi kubwa ya watafatiwa kwenye hojaji ilikubaliana na umuhimu wa lugha ya Kiswahili, hili lilitokana na matumizi yake katika mandhari ya chekechea. Wale waliopinga kuwa lugha ya Kiswahili sio muhimu ni wale ambao hawakupenda lugha hii, na pia hawakuwa na chaguo ila walisukumwa na mvuto wa mazingira uliojaa lugha ya Kiswahili.

Swali mojawapo katika dodoso, lilinuia kukusanya maoni ya wazazi wa chekechea kuhusiana na matumizi ya Kiswahili katika mafundisho ya chekechea. Maoni tuliyopata yaliashiria mielekeo hasi, kwa vile wasailiwa 16 (78.9%) kati ya 19 (100%) hawakuunga mkono lugha hii. Wazazi waliotafitiwa

wenye watoto katika shule za chekechea, hushurutisha walimu kuwafundisha wana wao katika lugha ya Kiingereza.  Licha ya lugha ya Kiswahili kutajwa na wazazi kuwa lugha ya mawasiliano, wazazi wawa hawa ndio wanaopinga kwamba lugha ya Kiswahili isitumiwe katika ufunzaji na ujifunzaji. Kutokana na msimamo wa wazazi, tunaelewa kuwa lugha ya Kiswahili inatumiwa katika mawasiliano ya kijamii, bali siyo katika ufunzaji na ujifunzaji wa shule za chekechea.

Kulikuwa na dhana iliyowataka wahojiwa wathibitishe kama kuna nyenzo zenye maandishi katika lugha ya Kiswahili. Watafitwa 15 (78.9%) walikataa kwamba hakuna nyenzo zenye maandishi katika lugha ya Kiswahili huku watafitiwa 4 (21.1%) wakikubali kuwa zipo. Tulipowadadisi watafitiwa zaidi, walikiri kuwa ilikuwa vigumu kutengeneza nyenzo zenye maandishi ya lugha ya Kiswahili. Wengine walinena kuwa nyenzo ziletwazo kama vile picha huwa tayari zimenunuliwa na nyingi yazo ni za lugha ya Kiingereza. Kinaya kilichobainika ni matumizi ya Kiswahili hasa katika mazungumzo, huku lugha hii ya Kiswahili ikikosa kushamiri katika maandishi.

Uwepo wa nyenzo za ufunzaji na ujifunzaji, ni muhimu katika kukuza mtalaa wowote, kwa vile hufanikisha masomo na kuinua kiwango cha ubora katika ufunzaji na ujifunzaji (Oluoch, 2002). Majibu kwenye uchunzaji yalioana na yale ya hojaji kwa vile; yalionyesha kuwa nyenzo zenye maandishi katika lugha ya Kiswahili zilikuwa adimu.  Kwa mujibu wa matokeo haya, nyenzo zenye maandishi katika lugha ya Kiswahili zilikuwa adimu mno.

Nyenzo kama picha, chati ndizo zilizopatikana kwa wingi katika shule za chekechea. Utafiti uligundua kuwa chati zilizoangikwa ukutani zilikuwa zimenunuliwa, kumaanisha kuwa walimu wengi hawakugharamika katika kuzitengeneza. Katika shule 4 za umma, mtafiti aligundua uwepo wa kadi huku idadi iliyosalia ikiwa ni shule za kibinafsi. Shule moja ya umma ndiyo iliyopatikana na maumbo mbalimbali, shule 11 za umma hazikuwa na nyenzo zozote. Baadhi ya walimu walipohojiwa kuhusu ukosefu wa nyenzo, walidai kuwa utengenezaji wa nyenzo za aina ya maumbo huchukua muda mwingi.

Uchunguzi ulibainisha kuwa kulikuwa na michoro katika shule 2 kati ya 19. Michoro hii ilipatikana katika shule za umma na za kibinafsi. Vihesabio vilipatikana katika shule mbili za kibinafsi. Wasimamizi wa shule walipohojiwa kuhusu jambo hili walitoa kauli kuwa nyenzo zipo ingawa walimu wao ndio wanaoweza kueleza kwa tafsili. Hata hivyo mtafiti aling'amua kuwa licha ya nyenzo hizo kupatikana katika baadhi ya shule, matumizi yake yalitiliwa shaka kwa vile nyenzo hizo zilikuwa zimerundikwa katika vyumba vilivyokuwa mbali na madarasa haya, kumaanisha kuwa hazirejelewi mara kwa mara. Kwa mujibu wa (Davis, 1975), nyenzo huwa vielelezo iwapo vinatumika katika uhalisia wakati wa ufunzaji na ujifunzaji.

Kinachojitokeza ni kuwa, njia wanazozitumia kuendeleza Kiswahili katika shule za chekechea si toshelevu, sababu za mtafiti kutaja kauli hii ni nyingi; kuna upungufu wa machapisho katika shule za chekechea, hivyo kuna uwezekano wa walimu kuwa na mawazo haba na kukosa msamiati katika lugha ya Kiswahili wanapofundisha.Vilevile, ukosefu wa nyenzo na vielelezo

wakati wa kufundisha hunyima somo uhalisia, (Msei, 1995) anatoa kauli kuwa vielelezo na nyenzo ndio njia mwafaka ya kufundisha watoto wa chekechea. Msei anaendeleza kusema kuwa, si vyema kwa mwalimu kutotumia virejeleo kwa vile matumizi yavyo hunoa stadi nyengine kando na ile ya kusikiliza, nyimbo na mashairi huvuta mandhari ya mbali darasani na hivyo kuleta uhai kwenye somo. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, Kiswahili hutumiwa katika nyimbo na ushairi wakati mafundisho.

Matokeo haya yanaashiria kuwa wanafunzi hawana nafasi ya kukuwa kwa stadi nyengine ambazo hujenga msingi wa lugha wakati mtoto wa chekechea aanzapo shule.  Kouma (1984) anadai kuwa matumizi ya nyenzo na vielelezo ni njia faafu ya ufunzaji na ujifunzaji. Kwa mujibu wa kauli aliyotoa Kouma, nyenzo zikirejelewa hunata akili za msomi. Kutokana na data hizi, mkinzano wa data unaonyesha kuwa kuna pengo kati ya lugha ya mawasiliano na andishi. (Taz.Jedwali 10 uk.88)

**Jedwali: 10 Nyenzo Zenye Maandishi Katika Lugha ya Kiswahili**

| N | SHULE | NYENZO | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Picha** | **Chati** | **Kadi** | **Maumbo** | **Michoro** | **Vihesabio** | **Vitu halisi** |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 1 | B | √ | _ | √ | _ | _ | _ | _ |
| 2 | U | √ | √ | √ | _ | _ | _ | _ |
| 3 | U | √ | √ | _ | _ | _ | _ | _ |
| 4 | B | _ | √ | _ | _ | _ | _ | _ |
| 5 | U | _ | √ | √ | _ | _ | _ | _ |
| 6 | U | _ | √ | √ | _ | _ | _ | _ |
| 7 | B | _ | _ | _ | _ | _ | _ | _ |
| 8 | B | _ | √ | _ | _ | _ | _ | _ |
| 9 | U | √ | _ | _ | _ | _ | _ | √ |
| 10 | B | _ | _ | _ | _ | √ | _ | _ |
| 11 | B | _ | √ | _ | _ | _ | _ | _ |
| 12 | B | _ | _ | √ | _ | _ | _ | _ |
| 13 | B | _ | √ | _ | √ | _ | _ | _ |
| 14 | B | _ | _ | _ | _ | _ | _ | _ |
| 15 | B | _ | _ | _ | _ | _ | _ | _ |
| 16 | U | √ | √ | _ | _ | √ | _ | _ |
| 17 | B | _ | _ | √ | _ | _ | _ | _ |
| 18 | B | _ | _ | _ | _ | _ | _ | _ |
| 19 | U | _ | _ | √ | _ | _ | _ | √ |
| | | 6 | 9 | 7 | 1 | 2 | - | 2 |

Chanzo: Uchunzaji wa mtafiti.

U Shule ya umma.

B Shule ya kibinafsi.

Katika kauli ya mwisho, wahojiwa waliulizwa watoe maoni yao kuhusiana na Kiswahili kama lugha eneo. Watafitiwa 19 (100%) walikubaliana na kauli hiyo, hakuna mtafitiwa hata mmoja aliyekanusha dai hili. Takwimu hizi, zilienda sambamba na swali kwenye dodoso ya wazazi, iliyowataka wataje lugha wanayozungumza na watoto wao nyumbani. Watafitiwa 15 (78.9%) walitaja lugha ya Kiswahili. Matokeo haya yanaoana na utafiti uliofanywa na Rugemalira (1990) kutathimini maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Matokeo yalionyesha kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo inayostahili, kwa maana ina uwezo wa kupitisha maarifa kwa hadhira kubwa zaidi nchini. Matokeo haya yana mantiki, kwani eneo la utafiti lina watu mseto ambao huingiliana kupitia lugha ya Kiswahili. Hali hii inaonyesha kuwa, Kiswahili ni lugha eneo.

### 4.7 Maswala Ibuka

Sehemu hii inaangazia mambo aliyoyagundua mtafiti akiwa nyanjani ambayo yanaweza kuathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili, lakini hakukuwa ameyashughulikia katika maandalizi ya utafiti mzima. Aliyoyaona yanaweza kuboresha au kudhuru matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mtafiti aligundua kupitia uchunzaji kuwa, baadhi ya walimu wa chekechea walikuwa wameathiriwa na lugha mama kiasi kwamba walitamka maneno ya Kiswahili kwa njia isiyostahili, Kwa mfano katika shule tatu walumu waliponyamazisha watoto wa shule za chekechea walitamka maneno kama vile ‘Nitakujaba’, wewe ‘nyamasa.’

Mtafiti aligundua kupitia uchunzaji ya kwamba walimu wengi walipoteza muda kwa kupiga gumzo kwa muda wa zaidi ya lisali moja, huku wakidai kuwa watoto walikuwa katika mapumziko. Hii inamaanisha kwamba mtaala wa chekechea uliathiriwa na walimu wazembe. Pia walimu walipoteza muda mwingi kubadilisha vipindi kutoka darasa moja hadi lingine.

Ripoti ya Baraza la kitaifa la mitihani nchini Kenya (KNEC, 2003) inasistiza kuwa, ili mwanafunzi afuzu katika mtihani wowote ule, ni lazima hati zake zisomeke kwa urahisi. Uchunzaji ulitufichulia kuwa maandishi yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili hayakusomeka kwa urahisi na hivyo kuwa kizingiti kwa matumizi faafu ya lugha ya Kiswahili katika shule hizi.

Hali nyingine iliyonasa nadhari ya mtafiti ni mazingira ya shule za chekechea. Shule 10 kati ya 19 zilikuwa za majengo mabovu na nyingi yazo zilikuwa katika nyumba za kibinafsi. Kisababishi kilikuwa ni ukosefu wa mapato. Walimu walidai kuwa paa zilizovuja, madarasa yasiyokuwa na komeo yalichangia pakubwa kupotea kwa makala mengi yakiwemo ya Kiswahili, na hivyo kuzorotesha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea.

# SURA YA TANO

## 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza matumizi ya Kiswahili kwa shule za chekechea katika Manispaa ya Webuye. Vigezo muhimu vilivyoshughulikiwa ni namna Kiswahili kinavyotumika, watumiaji wake, sababu za matumizi ya Kiswahili na hatimaye changamoto zinazokabili matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea.

Vifaa vya utafiti vilivyotumiwa katika kukusanya data ni hojaji kwa walimu wa chekechea, masaili kwa wasimamizi na wazazi wa shule za chekechea na kiongozi cha uchunzaji, kilichodhamiria kukusanya hali halisi ya matumizi ya Kiswahili katika mandhari ya chekechea. Sampuli ya utafiti ilijumuisha walimu 19 wa shule za chekechea za Manispaa ya Webuye Wilayani Bungoma Mashariki. Msimamizi na mzazi mmoja mmoja wa shule hizi 19 waliteuliwa katika sampuli. Wanafunzi wa chekechea walishirikishwa katika uchunzaji. Data ilikusanywa kutokana na vifaa hivi kitarakimu na kimaelezo, kando na haya majedwali na vielelezo vilijumuishwa.

Tasnifu hii ina sura tano na kila sura, imegawanywa katika sehemu mbalimbali. Katika sura ya kwanza, usuli wa utafiti ulishughulikiwa, swala la utafiti likaibushwa, malengo ya utafiti yakaainishwa na kufuatiwa na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, tahadhania, nadharia iliyoongoza utafiti na baadhi ya istilahi zilizofafanuliwa katika tasnifu hii.

Sura ya pili ilishughulikia mapitio ya maandishi. Sura ya tatu nayo ilishughulikia nyenzo, vielelezo, njia na mbinu za ukusanyaji data. Katika sura hii yafuatayo yalizingatiwa: muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli ya watafitiwa, nyenzo, mbinu za ukusanyaji data, majaribio ya utafiti na uaminifu wa nyenzo, maadili yalizingatiwa wakati wa utafiti, matatizo aliyokumbana nayo mtafiti na namna ya kuchanganua data.

Sura ya nne ilishughulikia uwasilishaji, uchanganuzi wa data na maelezo kuhusu matokeo. Baadhi ya matokeo ya utafiti huu, yaliafikiana na yale ya wataalamu wengine huku mengine yakipingana. Sura hii ya tano iliangazia mukhtasari, ugunduzi, hitimisho na mapendekezo ya utafiti yameshughulikiwa.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti uligundua kuwa Kiswahili hutumiwa kwa kuchanganya msimbo na hutawala mazungumzo katika mandhari ya darasani na nje ya darasa. Matumizi ya Kiswahili yalishamiri katika mazungumzo kinyume na ilivyo katika maandishi kwa vile matokeo ya uchunzaji yaliashiria ukosefu wa nyenzo zenye maandishi katika lugha ya Kiswahili. Ni bayana kuwa kulikuwa na pengo kubwa baina ya matumizi ya Kiswahili andishi na Kiswahili tamkwa. Ni kweli kuwa lugha iliyotumika zaidi katika mazungumzo ilipasa iwe ndiyo ile ile iliyotumika katika maandishi. Matumizi ya lugha mbili, katika miktadha tofauti ni kizingiti kikubwa kwa ukuaji na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, juhudi zapaswa kufanywa ili kusawazisha jambo hili.

Licha ya lugha ya Kiswahili kujitokeza kuwa maarufu katika shule za chekechea, hakuna shule hata moja iliyopatikana ikitumia lugha ya Kiswahili pekee. Uchanganyaji msimbo ulitawaliwa mno na lugha ya Kiswahili kuliko lugha ya Kiingereza au kienyeji. Uchanganyaji msimbo haukuwaathiri wanafunzi pekee, bali hata walimu walifanya hivyo walipokuwa wakitagusana na wanafunzi. Katika muktadha uu huu, lugha ya Kiswahili ilidhihirika pia katika nyimbo na kughani mashairi.

Matokeo ya utafiti huu yalituibulia ukweli kuwa, lugha ya Kiswahili japo ni maarufu miongoni mwa lugha za mafunzo katika shule za chekechea, ukweli unaodhihirika ni ukosefu wa utaratibu maalum wa matumizi ya lugha katika mandhari ya chekechea. Kutokana na ufichuzi huu, tunagundua kwamba walimu wa chekechea, licha ya kukiri kuwa wanaweza kuzungumza vyema lugha ya Kiswahili, matokeo yanaonyesha taswira tofauti. Sababu ni kuwa walimu 17 (89.4%) walidai kuwa wanamudu lugha ya Kiswahili, ilhali matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa hawana ufahamu mpana wa lugha ya Kiswahili. Lililo bayana ni kwamba, hakukuwa na mikakati mahsusi ya kuendeleza lugha ya Kiswahili. Watafitiwa 11 (57.9%) waliotoa kauli kwamba kuna mikakati, walitaja nyimbo na ushairi. Mikakati muhimu kama vile nyenzo, vielelezo, vitabu na majarida iliungwa mkono na watafitiwa wachache.

Kutokana na sababu zilizodaiwa kuchochea matumizi ya Kiswahili, matokeo yanaashiria kuwa watafitiwa wote waliunga mkono dai kuwa Kiswahili ni lugha eneo. Kauli hii inaenda sambamba na maoni ya watafitiwa 16 (84.2%) waliounga mkono dai kuwa Kiswahili ni lugha inayoeleweka kwa urahisi.

Jambo linalodhihirika ni kuwa lugha inayotawala katika eneo ndiyo inayoeleweka kwa urahisi na lugha yenyewe ni Kiswahili. Matokeo yaliashiria kuwa licha ya lugha hii kutumika, ufaafu wake ungali unatiliwa shaka kwa vile baadhi ya watafitiwa hawakuwa na uhakika kuhusiana na umuhimu na ubora wa lugha ya Kiswahili.

Tuligundua kuwa hakuna nyenzo toshelevu zenye maandishi katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa watafitiwa 15 (78.9%) walikubaliana na kauli hiyo. Watafitiwa 12 (63.2%) walipinga dai kuwa lugha ya Kiswahili ina msamiati toshelevu. Kuna muingiliano wa kauli hizi kwa vile, ukosefu wa nyenzo katika lugha hii, yamkini ulichangia baadhi ya watafitiwa kudai kuwa Kiswahili kukosa msamiati toshelevu. Utafiti huu uligundua kuwa, lugha ya Kiswahili ilitawala miktadha yote ya mitagusano, si darasani si michezoni. Licha ya umuhimu ambao umepewa lugha hii katika mandhari ya shule za chekechea za mjini, ukweli unaobainika ni kuwa wakati wa miktadha hii, watumiaji wa lugha hii ambao ni walimu na wanafunzi hukosa kudumisha uneni mmoja.

Ithibati kutokana na utafiti huu inaashiria kuwa, matumizi ya lugha ya Kiswahili hudidimizwa na matumizi ya lugha nyengine za mafundisho kama vile Kiingereza na lugha mama. Udadisi wetu ulionyesha kuwa sera ya lugha katika shule za chekechea imechangia pakubwa kudidimia kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule hizi. Kwa sababu tuligundua kuwa hakukuwa na mipaka kimatumizi kati ya lugha ya Kiswahili na lugha nyengine mathalan Kiingereza na lugha mama kama ilivyodaiwa na mojawapo ya tahadhania za utafiti.

Tuligundua kwamba, tajriba walionayo walimu ya kuwasiliana na wanafunzi katika lugha ya Kiswahili, ilitokana na kusambaa kwa matumizi ya Kiswahili katika eneo la utafiti. Dhana ya kuchanganya msimbo ilitokana na kuiga matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mazingira yaliyowazunguka.

Utafiti umefichua kuwa kuna upungufu na ukosefu wa nyenzo na vielelezo vyenye maandishi katika lugha ya Kiswahili na hata chache zilizopo zimerundukiwa kwenye magunia. Mmoja wa magwiji wa elimu ya chekechea Froebel (1836) alitudokezea kuwa mtoto si kama udongo ambao unaweza kufinyangwa na mwalimu. Kutokana na maelezo yake, mtoto ana uwezo wa kujua mambo, bali kile anachohitaji ni usaidizi na mwongozo, sawasawa na mmea ambao huhitaji kunyunyiziwa maji. Hivyo msaada huu unaweza kuwa kwa njia ya kumpa mtoto nyenzo na vielelezo vya kuchezea hatimaye hujifunza. Ukosefu wa umilisi wa kutosha katika lugha za mafundisho zilizotumika ulidhihirika kupitia vitu halisi. Dhana hii inatiliwa mkazo na Froebel, alipochangia kuwa ni vizuri kuwapa watoto vitu halisi kama vile mikebe, chati, kadi zenye maandishi katika lugha ya Kiswahili. Kwa vile watoto hujifunza zaidi kwa kuona kuliko kwa kusikia.

Katika miktadha ya matumizi ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji, tulifichua kuwa lugha ya Kiswahili hutawala miktadha yote; michezoni, darasani, wakati wa maankuli na katika mitagusano. Katika miktadha yote hii, tuligundua kuwa, matumizi ya kiwango cha juu yalidhihirika katika mitagusano kwa 73.7% na michezoni 73.6% miongoni mwa waalimu na wanafunzi wa shule za chekechea. Licha ya umuhimu ambao umepewa lugha ya Kiswahili

katika mandhari ya shule za chekechea za mjini, ukweli unaobainika ni kuwa, wakati wa miktadha hii, watumiaji wa lugha ambao ni waalimu na wanafunzi, hukosa kudumisha msimbo mmoja wa uneni wa lugha ya Kiswahili. Tuligundua kwamba, tajiriba walio nayo walimu na wanafunzi ya kuasiliana katika lugha ya Kiswahili, ilitokana na kusambaa kwa matumizi ya Kiswahili katika eneo la utafiti. Hili linaadhihirika kupitia kwa watafitiwa 17 (89.5%) waliodai kuwa hawajawahi kuhudhuria kozi zozote mafunzo katika lugha Kiswahili.  Kinaya kinachojitokeza hapa ni kuwa, asimia iyo hiyo iliyodai kuwa haijawahi kushiriki katika kozi za mafunzo katika lugha ya Kiswahili, ndio iliyo kiri kuimudu vyema lugha ya Kiswahili. Inabainika wazi kuwa lugha yeyote ile hukua kwa wakati, hivyo basi ni dhahiri kwamba walimu hawajapigwa msasa katika lugha ya Kiswahili.

Katika swala la changamoto, utafiti ulidhihirisha majibu ya  kutatanishakwa vile watafitiwa 17 (89.5%) waliunga mkono kauli isemayo Kiswahili hakina nafasi katika ulimwengu wa sasa huku watafitiwa 15 ( 78.9%) wakikubaliana na kauli iliyo dai kuwa Kiswahili lugha ya kawaida. Takwimu hizi zinafichua kuwa, lugha ya Kiswahili haina nafasi katika ulimwengu mpana, bali inachukuliwa kama lugha ya mitagusano. Kwa upande mwingine, watafitiwa 17 (89.5%) walipinga dai hili kuwa lugha ya Kiswahili haifai na vile vile haijaungwa mkono na washika dau. Linalojitokeza ni kuwa lugha ya Kiswahili inadhaminiwa katika mandhari yasiyo rasmi. Udadisi wetu ulionyesha kuwa mitindo ya lugha ya mafundisho au sera isiyo rasmi katika shule za chekechea imechangia pakubwa kudidimia kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za chekechea. Kwa sababu hakukuwa na mipaka

kimatumizi kati ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine, mathalani Kiingereza na lugha mama, ugunduzi huu ulithibitisha mojawapo ya tahadhania ya utafiti isemayo kuwa, hakuna mipaka bayana kimatumizi kati ya lugha zinazo tumika katika shule za chekechea. Utafiti ilifichua kuwa kulikuwa na mielekeo hasi miongoni mwa wasimamizi na wazazi wa shule za chekechea kuhusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Utafiti ulitambua kuwa walimu wa chekechea hawakuwahi kuhudhuria kozi zozote za kupigwa msasa katika matumizi ya lugha ya Kiswahili, bali walipata mwaliko wa semina zenye mada tofauti. Udadisi zaidi juu ya jambo hilo ulifichua kuwa watafitiwa hawakuona haja ya kuandaa semina za aina hiyo. Utafiti uligundua kuwa kulikuwa na mielekeo hasi miongoni mwa wasimamizi na wazazi wa shule za chekechea kuhusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Haya yalidhihirika wakati walipendekeza lugha badala ambayo ni Kiingereza. Vilevile wasimamizi walikiri kuwa hawakuwa na mikakati yoyote iliyowekwa ya kuendeleza lugha ya Kiswahili. Majibu yao yanaashiria kwamba walikuwa na lugha badala ambayo walipendekeza itumiwe, hivyo matumizi ya Kiswahili katika ufunzaji na ujifunzaji hayangeweza kuepukwa kwa vile ni lugha eneo.

Mwisho ni kwamba utafiti ulionyesha kuwa walimu wana muelekeo chanya kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili ndiyo maana wanajitahidi kufundisha katika lugha hii na hata kupendekeza lugha ya Kiswahili itumiwe.

## 5.3 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti huu hitimisho ni kuwa, Matumizi ya Kiswahili katika shule za chekechea yana mushkeli kwa vile yanaambatanishwa na sifa ya kuchanganya msimbo.

Chanzo cha matatizo yanayokumba matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule hizi, ni ukosefu wa utekelezaji wa sera rasmi ya wizara ya elimu, ambayo huwa hairuhusu matumizi ya lugha zaidi ya moja katika muktadha mmoja. Kwa sababu ya kutojua sera ya lugha barabara waliishia kutumia lugha zote tatu, yaani Kiswahili, Kiingereza na wakati mwingine Kibukusu. Washika dau mathalan wasimamizi na wazazi wa shule hizi wamechangia pakubwa kudidimizwa kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Walimu wa chekechea wana matatizo ya kibinafsi kama vile kutotilia maanani umuhimu wa nyenzo zenye maandishi katika lugha ya Kiswahili wakati wa mafundisho. Ingawa wanafunzi na walimu walitumia lugha zote tatu katika mitagusano, ilibainika kuwa walitumia Kiswahili zaidi kuliko lugha zile nyengine katika mandhari rasmi na yasiyo rasmi. Hata hivyo, ilibainika kuwa hakukuwa na mipaka kimatumizi kati ya Kiingereza, Kiswahili na wakati wingine Kibukusu. Kwa jumla matumizi ya lugha ya Kiswahili yanakumbwa na sintofahamu nyingi. Hata hivyo matokeo haya yamejikita katika Manispaa ya mji wa Webuye katika Wilaya ya Bungoma Mashariki.

## 5.4 Mapendekezo ya Mada ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa, matumizi ya lugha ya Kiswahili huambatanishwa na uchanganyaji msimbo. Hali hii ilidhihirisha matumizi mabaya ya lugha ya Kiswahili, yaliyojitokeza katika hojaji na katika kiongozi cha uchunzaji. Kwa hivyo, ni wazi kwamba wanafunzi na walimu wanahitaji matumizi ya msimbo mmoja wa lugha utakaochochea umilisi wa lugha ya Kiswahili badala ya kutanda kutoka lugha moja hadi nyingine. Inafaa jukumu la kila lugha lielezwe waziwazi na K.I.E ili kusiwe na kuchanganyikiwa katika matumizi ya lugha hizo.

Kiwango cha matumizi ya lugha ya Kiswahili kingali chini mno; kinahitaji kufuatiliwa na walimu, wasimamizi wa shule, watakaobuni mwongozo wa matumizi ya lugha ya Kiswahili la si hivyo tunaweza kupata kizazi ambacho hakina umilisi katika lugha iwayo yoyote.

Washika dau wa shule hizi wanapaswa kutilia maanani sera rasmi ya lugha ya wizara ya elimu. Wasimamizi wa shule hizi wanahitaji kuwaelimisha walimu kuhusiana na umuhimu wa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Sera isiyo rasmi ambayo hutekelezwa katika baadhi ya shule inapaswa kukomeshwa. Matumizi ya lugha kama asemavyo Barnes na wenzake (1969) inapaswa kushughulikiwa na kila mwalimu.Vilevile wanafunzi wanapaswa kuelimishwa kuhusiana na umuhimu wa kuwasiliana katika lugha ya Kiswahili wanapotagusana.

Upungufu wa nyenzo za kufundishia shuleni unaweza kukabiliwa kwa njia kadhaa. Walimu shuleni wanaweza kutafuta ufadhili kutoka kwa mashirika mbalimbali ili shule za chekechea zipate fedha za kununua nyenzo hizi. Hatua nyingine ni kuwa shule zilizomo katika mazingara mamoja zikuze ukuruba wa kubuni mpango wa kununua na kutumia nyenzo hizi kwa pamoja hasa zile za oni. Mwisho walimu wanapaswa kuwa na ufaraguzi na waweze kuzua nyenzo zaidi na zenye gharama ya chini.

Iwapo ni lazima lugha nyingine kutumika katika shule hizi ni sharti zitumiwe katika muktadha tofauti bali sio lugha nyingi katika muktadha mmoja. Katika kufanya hivi, hoja zilizofunzwa katika lugha moja zitafafanuliwa kikamilifu katika lugha nyengine, bali sio kufafanua dhana kwa kutumia msimbo tofauti. Utafiti huu unapendekeza kuwa ikiwa hatuna budi kukitumia Kiingereza au kwa uchache lugha mama, basi lugha zote mbili zitumiwe sambamba katika mafunzo yao. Hali hii huleta uhai katika somo.

Lengo kuu la mapendekezo haya ni kuwatia moyo walimu na wanafunzi wa chekechea katika nchi ya Kenya, kuonea fahari matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini na pia kuwa wabunifu kimatumizi. Mtafiti anaamini kuwa muelekeo kama huu, utasababisha utofauti katika matumizi ya lugha katika siku za baadaye, kama somo na vilevile lugha ya kufundishia.

### 5.4.1 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zaidi

Utafiti kuhusu matumizi ya Kiswahili katika mafunzo ya shule za chekechea bado ni mbichi. Mtafiti hawezi kudai kuwa ameshughulikia vipengele vyote

vinavyohusiana na matumizi ya lugha. Hivyo itafaa mno ikiwa tafiti zaidi zingefanywa katika shule za chekechea.

Pendekezo la kwanza ni kuwa utafiti ufanywe kuchunguza uhusika wa wasimamizi wa shule za chekechea kuhusiana na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kwa vile wao ndiyo wenye uwezo wa kuzua sera za lugha za kibinafsi ambazo si rasmi.

Pili utafiti linganishi ufanywe katika shule za chekechea za kibinafsi na za umma kutathmini matumizi ya lugha ya Kiswahili. Matokeo katika shule hizi yanaweza kulinganishwa na kujadiliwa kwa kiwango cha kitaifa, kwa vile yatawakilisha hali halisi kwenye shule za chekechea za umma na na za kibinafsi.

Tatu, mtafiti anapendekeza utafiti wa aina hii ufanywe miongoni mwa walimu na wanafunzi wa shule za msingi, ili kukadiria matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kiwango hiki.

Pendekezo la nne ni kuwa utafiti ufanywe kutambua mitazamo inayoweza kuchochea ufahamu na dhamana iliyopo katika matumizi ya lugha mbalimbali za mafunzo katika mandhari ya shuleni.

# MAREJELEO


Adedeji, T.A. (1982). *The Teaching of African Languages.* Kent: Hudder & Staughton Limited.

Akhusama, J.M.C. (1984). "A Study of Factors that Affect Kiswahili Language Among Primary School Children in Kenya". M.E.D Thesis, Kenyatta University (Haijachapishwa).

Awoniyi, T.A. (1982). *The Teaching of African Languages.* London: Hodder and Stoughton Press.

Baker, C. (1992). *Attitudes and Language.* New York: Multilingual Matters Press.

Bamgbose, A. (1991). *Language of Instructions Policy and Practice in Africa*. Dakar: Published by UNESCO.

Bangunywa, M.K.A. (1980). *Critical Issues in African Education*. A Case Study of Uganda. Nairobi: East Africa Publishing House.

Barasa, L.P. (1997). "English Language Teaching in Kenyan Secondary School: Policy Planning and Practice". University of Hull. (Haijachapishwa).

Barnes, D. Britton, J. & Rosen, H. (1969). *Language, the Learner and the School*. London: Basil Blackwell Ltd.

Best, J.W. & Kahn J.V. (2003). *Research in Education 7th Edition*. New Delhi: Prentice Hall of India.

Bowers, J. (1968). 'Language Problem and Literacy' Katika J.A. Fishman et al (Ed). *Language Problems of Developing Nations*. New York: John Wiley and sons.

Broughton, G. (1980). *Teaching English as a Foreign Language*. London: Routledge.

Bunyi, G. W. (1986). "Language Switching in Std. 4 in Kiswahili, English Medium classrooms". M.ED. Thesis Kenyatta University. (Haijachapishwa).

Chakava, H. (1996) *Books and Reading in Kenya.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Charlotte, S.W.A.(2001). "Reaching Out For Linguistic Identity, the State of Kiswahili in Kenya". Katika N.I. Shitemi et al (Ed). *Kiswahili: A Tool for Development*. Eldoret: Moi University Press.

Chieni S.N. (2001). "Kiswahili a National Language or a Social Class Language in Kenya". Katika N.I. Shitemi et al (Ed). *Kiswahili: A Tool for Development*. Eldoret: Moi University Press.

Child, D. (1973). *Psychology and the Teacher.* London: Holt, Reinhart Press.

Chimerah, R.M (1988). *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons.* Nairobi: Nairobi University Press.

Chimerah, R.M. & Nabea, W. (1987). Defending Ngugi's Theory: "Why Africans Must Keep Their Mother Tongues Alive" Makala katika Daily Nation, 1987: Agosti 3, uk. 12

Cleghorn, A. (1987). "Language Use in the Teaching of Science in Kenyan Primary Schools". Paper Presented At the Bureau of Educational Research Seminar. Nairobi: Kenyatta University. April 7, 1987.

Chumbow, B.S. (2003 "Language and Language Policy in Cameroon". Katika N.K. Kale et al. (Ed). *An African Experiment in Nation Building*. Cameroon: West View Press.

Croll, P. (1986). *Systematic Classroom Observation.* London: The Falmer Press.

Dalen, D.B.V. (1979). *Understanding Education Research*. London: McGraw-Hill, Incl.

Davis, W.J.K. (1975). *Learning Resources: An argument for Schools*. London: Longman Green Co. Ltd.

Fishman, J.A. (1965). “Who Speaks What Language to Who and When?” Katika *Linguistics*, Volume 2 uk. 67-85.

__________. (1972). *Advances in the Sociology Language vol.1: Basic Concepts, Theories and Problems: Alternative Approaches*. The Hague: Morton and Company.

Froebel, F. (1836). *The Education of Man.* New York: Appleton Publishers.

Gardener, R.C. (1977). *Motivation in 2nd Language Acquisition.* London: Edward Arnold Publishers.

Gibbons, J. (1989). “The Issue of the Language of Instruction in the Lower Forms of Hongkong, Secondary Schools”. Katika C. Kennedy; et al (Ed) (1989). *Language Planning and English Language Teaching*. London: Prentice Hall.

Giles, H. Taylor, D.M. & Bourhis, R.Y. (1973). *Towards a Theory of Interpersonal Accommodation Through Speech: Language in Society*. London: Prentice Hall.

Good, C.V. (1972). *Essentials of Educational Research.* New York: Appleton-Centuary – Crofts.

Halliday, M.K. (1970). *Exploration in the Function of Language: Exploration in Language Study*. London: Edward Arnold Publishers.

Ipara, O. (2001). “Uwezekano wa Kiswahili Kuwa Lugha ya Kufundishia ya Pili Katika Kiwango cha Juu cha Shule za Msingi”. Katika N. I. Shitemi, et al (Ed). *Kiswahili: A Tool for Development*. Eldoret: Moi University Press.

Johnson, R. (1976). *Language Teaching: A Scientific Approach.* Newyork: McGraw-Hill Inc.

Kabiru, M. & Birich, M. (1995). "Early Childhood Teacher Education", In Report of the Proceedings of the Teacher Education Conference, Held at Egerton University, Njoro from 5th to 9th Dec. 1994, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kabiru, M. (1992). "The Status of Early Childhood in Kenya". A Paper Presented at the Symposium of B.E.D Program Held at Mombasa Beach Hotel.

Karega, M. (2001). "Kiswahili and Economic Development". Katika N. I. Shitemi et al (Ed). *Kiswahili: A Tool for Development*. Eldoret: Moi University press.

Kembo-Sure, E. (1991). "Language Functions & Language Attitudes. A Case of Diglosia in Kenya". Proceedings of a Seminar on the Role of Language and Literature in the School Curriculum, Nairobi.

____________ (1994). "Language Attitudes, Use and Proficiency". A Sociolinguistic Study of English' D.Phil. Thesis, Eldoret: Moi University (Haijachapishwa).

Kembo, J.A. (2000). "Inferencing in 2nd Language. How Far is Language Proficiency a Factor?" Katika V. I. C. Webb na E. Kembo-Sure. *African Voices: An Introduction to the Languages and Linguistics of Africa.* Oxford: Oxford University Press.

_________ (2002). "Using African Language of Learning and Instruction": Katika V. I. C. Webb na L. Gangla et al (Ed). *Intricate Questions and Issues*. Oxford: Oxford University Press.

Kennedy, C. (1989). *Language Planning and English Language*. London: Teaching Prentice Hall.

Kerlinger, F.N. (2004). *Foundations of Behavioural Research.* New Delhi: Surjeet Publishers, 2nd Edition.

Kihore, Y.M. (1983). "Nafasi ya Kiswahili Barani Afrika" katika Mulika Nambari 15, *TUKI*, Chuo Kikuu Dar es salaam. Teachers College.

Kimui, V.W. (1988). "A Study of Availability and Use of the Learning and Teaching Resources in Primary". Teachers Colleges in Kenya. Ph.D. Thesis, Kenyatta University. (Haijachapishwa).

King'ei, K. (1997). "Kiswahili's Rightful place". Katika Daily Nation Aprili 19 uk. 16.

KNEC (2003). *K.C.S.E Report.* Nairobi: Government Printers.

Kothari, C.R. (2003). *Research Methodology: Methods and Techniques.* 2nd Edition. New Delhi: New Age International (p) Ltd Publishers.

Kouma, F. (1984). "A Study of Problems Faced by Teachers of English in Congo" P.G.D. in Curriculum Development. University of Nairobi. (Haijachapishwa).

Lang'at, P. (1997). "Kiswahili Kimedunishwa" Katika Taifa Leo, Machi 20, 1997 uk. 2.

Matundura, E. (2008). "Kiswahili Kupewa Hadhi". Katika Gazeti la Taifa Leo 6/3/2008 Alhamisi.

Mazrui, A. & Mazrui, A. (1995). *Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbaabu, I. (1991). "The Impact of Language Policy on the Development of Kiswahili in Kenya". (1930-1990) PhD. Thesis Howard University (Haijachapishwa).

_________(1996). *Language Policy in East Africa. A Dependency Theory Perspective*. Nairobi: Education Research and Publication.

McDonough, S.H, (1995). *Strategy and Skill in Learning: A Foreign Language*. London: Edward Arnold.

McGregor, G.P. (1971). *English in Africa*. London: Heinneman Publishers.

Meerkotter, D. (2002). “Markets Language Socio-Economic Stratification and Teachers in Schooling” A Paper Presented at Workshop on Language of Instruction in South Africa. 22- 24th October 1987.

Merrit, M. (1987). “Language of Instruction and Instruction of Language”. Report of the Workshop on Schooling, Cognition and Work. Educational Research McGill University Workshop, Kisumu, Mei, 1987.

Mkwizu, M.A. (2002).”The Pedagogical Implications of Using English in Teaching English Civics in Tanzanian Secondary School”. A Paper Presented at a Workshop in Morogoro: Private Printers.

Mohammed, A.M. (1988). The Introduction of Kiswahili as A medium of Instruction in Tanzania Secondary School. A Diagnosis and Evaluative Study. M. A Thesis Chuo Kikuu Cha Dar-es-salaam.

Msanjila, Y.P. (2005). “Kiswahili Kutumika Katika Umoja wa Afrika: Changamoto na Mikakati ya Utekelezaji katika Kiswahili”. *Juzuu 68 la 2005*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Msei, I. (1995). “A Survey of Resources for Teaching and Learning Kiswahili in Some Selected Primary Schools of Central Division, Iveti South Machakos District”. M.ED. Project University of Nairobi. (Haijachapishwa).

Mugenda, M.O. & Mugenda, A.G. (2003). *Research Methods, Quantitative & Qualitative Approaches: African Centre for Technology Studies. Nairobi: Acts Press.*

Mukuria, D. (1995). “Kenyans Language Policy Development, With Special Emphasis on Kiswahili”. Katika K. Senamu na D. Williams et al (Ed). *The Creative Use of Language in Kenya.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mulama, J. (1994). htt: //uregina. ca/vginrich/2f99. htm. Accessed 14/9/2006.

Mulama, P. & Matteru, M. (1978). “Haja ya Kutumia Kiswahili Kufundishia Elimu ya Juu”. Minutes of the Annual Heads of Secondary Conference, 12th-16th Oct. 1987.

Munyua J.G. (2002). "The Emerging Viswahili and Kiswahili Research". Katika I. Simala (Mha.): *Utafiti wa Kiswahili.* Eldoret: Moi University Press.

__________ (2007). "Isimu na Mwalimu wa Sarufi ya Kiswahili: Umuhimu wa Maarifa ya Kiisimu Darasani". Katika F. E. M. K Senkoro (Mha.). *Lugha na Fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki*. Dar es Salaam. Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki.

Muruguru P.S. ( 2000). "Students Performance in Kiswahili: A case Study of Selected Secondary schools in Nakuru District". M.Phil. Thesis. Eldoret Moi University.( Haijachapishwa).

Mushingi, T.S. (1989). "Vernacular Languages as a Media of Instruction: The Case of Kiswahili in Zaire" Ph.D. Thesis, Georgetown University.

Nabwire, B.O. (2002). "Factors that Influence the Learning of Kiswahili Among Lower Primary Schools in Eldoret" M. Phil. Thesis. Moi University (Haijachapishwa).

Ngugi, wa Thiongo (1987). *Decolonizing the Mind: The Politics of Language in African Literature.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Nkapa, N. (1997). *Educational Research for Modern School.* Enugu: Forth Dimension Publishing Company Limited.

Nyaga, C.M. (1994)."Motivating Factors for Kiembu-Kiswahili-English Code Choice and Code Switching: A Case Study of Kavutiri Secondary School Embu" M.phil. Thesis, Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

Nyonyontino, R.M. (1980). "The Origin and Operations of Pre-School Education in Kenya". A Paper Presented at the Research Committee of Education, Conference Held in Nairobi.

Obanya, P. (1999). *The Dilema of Education in Africa*. Dakar: UNESCO – BREDA.

Obura, P.A. (1990). "Language in Conflict in Education in Anglophone". Katika P.H. Nelde et al (Ed). *Language Attitudes and Language Conflict*. Dakar: Pluringua Bonn Printers.

Oluoch, G.P. (2002). *Essentials of Curriculum Development.* Nairobi: Birds Printers, Office Stationery and Equipment Ltd.

Omulando, C. (2002). ”The Effect of Kiswahili on the Use of English as A Medium of Instruction in Selected Secondary Schools in Bungoma District” M.Phil. Thesis. Eldoret: Moi University. (Haijachapishwa).

Oppenheim, A.N. (1992). *Questionnaire Design and Attitude Measurement.* New York: New Edition Continuum Ltd.

Peil, M. (1995). *Social Science Research Methods: A Handbook for Africa* Nairobi: East African Educational Publishers.

Pluckrose, H. (1982). *Starting school: The Vital years*. Stockholm: Begs fortag.

Prasad, D.R. & Reddy, K.M. (1983). *Research Methods in Social Sciences.* New Delhi: Private Press.

Ramsden, P. (1988). *Improving Learning: New Perspectives*. London: Reagan Ltd.

Republic of Kenya (1964). “The Kenya Education Commission Report (Ominde Report)”. Nairobi: Government Press.

Republic of Kenya (1976). “Report of the National Committee on Educational Objectives and policies (Gachathi Report)”. Nairobi: Government Press.

Rubagunya, C. (1994). *Language in African Classrooms.* Clevedon: Multilingual Matters.

Rugemalira, J.M. (1990). *Reflection of Recent Development in Language Policy in Tanzania.* Dar es Salaam: A Froplus Industries Ltd.

Ruth Falhman, B.& Chud, J. (1985). *Early Childhood Education for Multi-Cultural Society*. Colombia: University Press Limited.

Sampath, K. (1990). *Introduction to Education Techniques*. New Delhi: Sterling Publishers.

Sedlack, R.G.& Stanley, J. (1992). *Social Research: Theory and Methods.* Bouston: Allyn and Bacon.

Selinger, H. and Shahomy, L. (1989). *Second Language Research Methods.* Oxford: Oxford University Press.

Shiundu, J. & Omulando, S. (1992). *Curriculum Theory and Practice in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

Simala, I. (2001). "Kiswahili katika Sayansi na Teknolojia". Katika N. I. Shitemi et al (Ed). *Kiswahili: A Tool for Development.* Eldoret: Moi University Press.

_______ (2006). "Kiswahili in East African Community Education, Challenges and Opportunities". Katika E. Kembo Sure, et al (Ed). *Language Planning for Development in Africa*. Eldoret: Moi University Press.

Singleton, R.A. (1993). *Approaches to Social Research.* New York: O.U.P.

Tuckman, B.W. (1978). *Conducting Educational Research.* New York: Harcourt Brace Jonavovich Inc.

UNESCO (1987). "Facilitating the Adoption of African Languages as Educational Instrument in the African Countries. Guidelines to Case Studies and Synthesis". Regional Office for Education in Africa. Darkar, Senegal.

Wardhaugh, R. (1987). *Languages in Competition: Dominance Diversity and Decline.* Basil: Basil Blackwell Printing Press.

Williams, E. (1996)."Reading in Two Languages at Year Five in African Primary Schools". Katika *Applied linguistics* Vol. 17/2 uk 182-209.

Williams, G. (1992). *Sociolinguistic: A Social Linguistic Critique*. London: Routledge.

Wolff, H.E. (2006). “The Language Factor in Discourseon Development and Education in Africa”. Katika E. Kembo Sure, et al (Ed): *Language Planning for Development in .Africa.* Eldoret: Moi University Press.

## VIAMBATISHI

## KIAMBATISHI I

## BARUA YA UTAFITI

Kwa Mwalimu,

Mimi ni mwanafunzi wa uzamili katika chuo kikuu cha Magharibi. Ninafanya utafiti kuhusu matumizi ya Kiswahili katika mafunzo ya shule za chekechea. Nimechagua kutumia hojaji kwa sababu kifaa hiki kitanipatia data za kuaminika nyanjani. Hojaji hii inalenga kukusanya habari kuhusu matumizi ya Kiswahili kwa mafunzo ya shule za chekechea. Habari zitakazokusanywa zitatumiwa tu kufanikisha utafiti wala si kwa matumizi mengine. Tunatarajia kuwa utafiti huu utasababisha mapendekezo mapya kwa wapangaji sera. Ningeomba ushirikiane nami katika utafiti huu.

Kwa mukhtasari haki zote za wahojiwa zitahifadhiwa.

Weka alama ya mkwaju (√) kwa majibu yaliyo sahihi.

Asante

Wako mwaminifu



Martha Liambila.

## KIAMBATISHI II

## HOJAJI KWA WALIMU

**A.** Aina ya Shule

a) Umma ☐ b) Binafsi ☐

**B. <u>Namna Kiswahili Kinavyotumika:</u>**

**1) Kuna Matumizi ya Kiswahili katika shule hii?**

Ndio ☐ la ☐

**2) Kama jawabu ni "ndiyo", Kiswahili kinatumika vipi?**

a) Kwa ufasaha ☐

b) Kuchanganya msimbo. ☐

c) Kubadili msimbo ☐

d) Nyingine. ☐ Taja……………………….

**Je, Kiswahili hutumika katika njia zifuatazo?**

a) Nyimbo ☐

b) Ushairi ☐

c) Semi ☐

d) Mitagusano ☐

**C, Watumiaji wa Kiswahili Katika Shule za Chekechea:**

(Weka alama ya √ kwa jawabu sahihi)

**3) Ni nani wanaotumia Kiswahili?**

| **Watumiaji** | **Ndio** | **La** |
|---|---|---|
| **Walimu** | | |
| **Wanafunzi** | | |

**4) Je, wanafunzi wako wanaweza kujieleza vyema katika lugha gani?**

Kiswahili ☐ Kiingereza ☐ lugha mama ☐

**5) Mnatumia Kiswahili katika miktadha gani?**

a) Michezoni ☐

☐

b) Darasani

c) Wakati wa mankuli ☐

d) Wakati wa mitagusano ☐

e) Wakati mwingine ☐

**7) Je, unamudu vyema lugha ya Kiswahili?**

a) Ndiyo ☐

b) La ☐

**8) Ni mikakati ipi imewekwa kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili inapewa msingi unaostahili?**

a) Nyenzo na vielelezo ☐

b) Nyimbo na ushairi ☐

c) Vitabu na majarida ☐

d) Mingine________________________ taja

## D. Sababu za Matumizi ya Kiswahili:

**9. Zifuatazo zinaweza kuwa sababu za matumizi ya Kiswahili. Umepewa kauli tano za kukubaliana, weka alama ya (√) kuonyesha makubaliano yako.**

| Nambari | Sababu za Kiswahili kutumika. | Nakubali ana sana | Nakubali ana | Sina uhakika | Nakataa | Nakataa kabisa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **5** | **4** | **3** | **2** | **1** |
| 1. | Kiswahili ni lugha bora | | | | | |
| 2. | Lugha ya Kiswahili hutawala mazungumzo | | | | | |
| 3. | Ni lugha mama kwa wengi | | | | | |
| 4. | Ni rahisi kuchanganya msimbo | | | | | |
| 5. | Ni rahisi kubadili msimbo | | | | | |
| 6. | Kiswahili kina misamiati toshelevu | | | | | |
| 7. | Kiswahili ni lugha muhimu | | | | | |
| 8. | Kiswahili kinaeleweka kwa urahisi | | | | | |
| 9. | Kuna nyenzo katika lugha ya Kiswahili | | | | | |
| 10. | Ni lugha eneo kwa wengi | | | | | |

**E. <u>Changamoto zinazokabili lugha ya Kiswahili:</u>**

**10. Zifuatazo zaweza kuwa changamoto zinazokabili matumizi ya Kiswahili, umepewa kauli tano za kukubaliana, weka alama ya ( √ ) kuonyesha msimamo wako.**

| Nambari | Changamoto zinazokabili lugha ya Kiswahili | Nakubali ana sana | Nakub aliana | Sina uhakika | Nakataa | Nakataa kabisa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 1. | Kiswahili hakifai | | | | | |
| 2. | Kiswahili hakina misamiati toshelevu. | | | | | |
| 3. | Matumizi ya Kiswahili si ishara ya usomaji | | | | | |
| 4. | Kiswahili ni lugha ya kawaida | | | | | |
| 5. | Kiswahili hakina nafasi katika ulimwengu wa sasa. | | | | | |
| 6. | Ni vigumu kufundisha kwa Kiswahili | | | | | |
| 7. | Kiswahili hakijaungwa mkono na washika dau. | | | | | |
| 8. | Sera ya lugha katika shule inapinga matumizi yake | | | | | |
| 9. | Kiswahili kinahusishwa na watu wa tabaka la chi | | | | | |

## KIAMBATISHI CHA III

## UTARATIBU WA KIONGOZI CHA UCHUNZAJI

Utaratibu huu utajazwa na mtafiti huku akiwa anahudhuria kipindi mojawapo katika shule za chekechea. Umuhimu wa kifaa hiki ni kubainisha mandhari ya matumizi ya Kiswahili katika shule za chekechea.

A. Je Kiswahili hutumika katika njia zifuatazo?

1. Nyimbo

2. Ushairi

3. Semi

4. Mitagusano

B. Lugha gani hutawala mawasiliano?

1. Baina ya wanafunzi

2 .Baina ya walimu na wanafunzi

**Uchunzaji wa Matumizi ya Nyenzo katika Lugha ya Kiswahili.**

| **Nyenzo** | **Kuwepo** | | **Matumizi** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Ndiyo** | **La** | **Ndiyo** | **La** |
| **Picha** | | | | |
| **Michoro** | | | | |
| **Maumbo** | | | | |
| **Kadi** | | | | |
| **Chati** | | | | |
| **Vihesabio** | | | | |
| **Vitu halisi** | | | | |

## KIAMBATISHI CHA IV

## DODOSO KWA WASIMAMIZI WA SHULE ZA CHEKECHEA.

Wasimamizi wa shule zilizoteuliwa walihojiwa kwa kutumia dodoso hii Iliyonuia kukusanya habari kuhusu matumizi ya Kiswahili katika mafunzo ya shule za chekechea

1. Lugha ya Kiswahili hutumiwa katika mafunzo?
2. Sera ya lugha inapendekeza lugha zipi?
3. (a) Walimu huudhuria kozi zozote kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahilii?

   (b) Kama jawabu ni 'la' kwa nini?
4. Ungepewa nafasi, ungependekeza matumizi ya lugha ipi?
5. Lugha ipi iliyo maarufu katika shule yako, na kwa nini?
6. Kuna mikakati yoyote iliyowekwa ya kuendeleza matumizi ya Kiswahili?
7. Kama jawabu ni 'ndio' ni mikakati ipi?


## KIAMBATISHI V

## DODOSO KWA WAZAZI WA SHULE ZA CHEKECHEA.

1. Huwa unawasiliana na watoto wako kwa lugha gani?
2. Ungependa mtoto wako afundishwe kwa lugha gani?
3. Una maoni gani kuhusu mafunzo katika lugha ya Kiswahili?
4. Ungepewa nafasi, ungependekeza matumizi ya lugha ipi?
5. Moja wapo ya sababu zilizokuvutia kuhusiana na shule hii, ni lugha ya mafunzo, unakubaliana na kauli hii?

**KIAMBATISHI VI**


**RAMANI YA WILAYA YA BUNGOMA MASHARIKI**




Chanzo: Ramani ya Wilaya ya Bungoma Mashariki (2008-2030)

## KIAMBATISHI VII

## RAMANI YA SHULE ZA CHEKECHEA KATIKA MANISPAA YA WEBUYE.




Chanzo: Ramani ya Shule za Chekechea za Manispaa ya webuye (2008-2030)

## KIAMBATISHI VIII

## ORODHA YA MAJINA YA SHULE ZA CHEKECHEA

**Shule za Umma za Chekechea**

U1_ Nabuyole

U2 – Salvation Army

U3 – St. Joseph's

U4 – Matulo R.C

U5 – Webuye DEB

U6 – Lugulu Day

U7 – Webuye Central

U8 – Mukhuyu

**Shule za Kibinafsi za Chekechea**

B1- St. Peter's Academy

B2 – Motherland

B3 – Agape

B4 – Bright Fountain

B5 – Webuye Baptist

B6- Webuye Flyover

B7– Railways

B8– Pan Paper

B9 - Dovelight

B10 - Bezalel

B11 - Sunrise

**KIAMBATISHI IX**

**BARUA YA KUIDHINISHA KUFANYWA KWA UTAFITI**

REPUBLIC OF KENYA

**MINISTRY OF SCIENCE & TECHNOLOGY**

Telegrams: "SCIENCE TEC", Nairobi
Telephone: 02-318581
E-Mail:ps@scienceandtechnology.go.ke

JOGOO HOUSE "B"
HARAMBEE AVENUE,
P.O. Box 9583-00200
NAIROBI

When Replying please quote
**Ref. MOST 13/001/ 37C 520/2**

**8th August 2007**

Martha Liambila
Masinde Muliro University
P.O. Box 190
**KAKAMEGA**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on, ***'Uchunguzi wa Matumizi ya Kiswahili Katika Mafunzo ya Shule za Chekechea Katika Manispaa ya Webuye'***

I am pleased to inform you that you have been authorized to carry out research in Webuye Municipality in Bungoma District for a duration of three months ending 30th October 2007.

You are advised to report to the District Commissioner, the District Education Officer and the Town Clerk Webuye Municipality before embarking on your research project.

On completion of your research, you are expected to submit two copies of your research report to this office.

**M. O. ONDIEKI**
**FOR: PERMANENT SECRETARY**

Copy to:

The District Commissioner
**Bungoma District**

The District Education District
**Bungoma District**

The Town Clerk
Webuye Municipality
**Webuye**

**KIAMBATISHI X**

**KIBALI CHA UTAFITI**

PAGE 2

THIS IS TO CERTIFY THAT:

Prof./Dr./Mr./Mrs./Miss. MARTHA LIAMBILA

of (Address). MASINDE MULIRO UNIVERSITY P.O.BOX 190 KAKAMEGA

has been permitted to conduct research in..................

..........................................Location

BUNGOMA EAST ..........................District,

WESTERN ..........................Province,

on the topic UCHUNGUZI WA MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA MAFUNZO YA SHULE ZA CHEKECHEA KATIKA MANISPAA YA WEBUYE

for a period ending 30TH OCTOBER, 20 07

PAGE 3

Research Permit No. MOST 13/001/37C 520

Date of issue. 8.8.2007

Fee received... SHS.500.00



FOR PERMANENT SECRETARY MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY

Applicant's Signature

M.O.ONDIEKI

FOR: Permanent Secretary Ministry of Science and Technology